# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

# CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, TAITA TAVETA CONTITUENCY HEL AT TIMBILIA HIGH SCHOOL

# ON

# MAY 2, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARING, TAITA TAVETA CONSTITUENCY, HELD AT TIMBILIA HIGH SCHOOL ON MAY 02 2002**

**Present:**

1. Com. Prof. A. Idha Salim
2. Com. Domiziano Ratanya

**Secretariat staff in Attendance:**

1. Collins Mukewa - Programme Officer

2. Fidellis Wangatta - Assistant Programme Officer
3. Grace Gitu - Verbatim Recorder
4. Lucy Ake - Sign Interpreter
5.

Meeting started at 9.50 am with Com. Salim in chair.

**Com. Salim:** Tumefurahi sana mimi na mwezangu hapa kuwa mumefika kwa wingi kushugulikia kazi hii lakini kabla hatujaanza kabisa ningependa kama tutafunguliwa mkutano wetu kwa maombi. Yuko Reverend, yuko Pastor ? Karibu tafadhali.

**Pastor:** Baba katika jina la Yesu tunakaribisha tena uwepo wako uwe pamoja na sisi kwa ajili ya siku muhimu sana katika constituency yetu ya Taveta, tukae pamoja tukatoe maoni yetu kuhusu Katiba mpya. Bariki Ma-commissioner, bariki hata waandishi, bariki wahusika wote Bwana, hata sisi ambao tutakaokuwa tukitoa maoni, wacha uwepo wa Roho Mtakatifu uwe pamoja na sisi. Kazi hii tumeiweka mikononi mwako tunapoanza hadi tufikapo mwisho Mungu, tukawe na uwepo wako Baba yetu. Ni katika jina lako Baba tumeomba haya na kuamini, Amen.

**Com. Salim:** Asante sana kwa dua zako na maombi yako tuombe Mwenyezi Mungu akubali maombi yetu. Bwana D.O, Bwana Mutali, kwanza ningependa kuwajulisha sisi ni nani. Mimi jina langu ni A. Idha Salim, Commissioner na naibu wa mwenye kiti, na hapa kwa upande wangu wa kushoto ninaye Commissioner Ratanya mwenzangu ambaye pamoja tutashirikiana kusikiza maoni yenu na kuya-record.

Lengo la mkutano huu na mkutano wa kesho kama mulivyosikia kutoka kwa Distict Coordinator wetu ni kukusanya maoni yenu kuhusu kazi ya kurekebisha Katiba. Sina haja ya kuwaeleza mengi zaidi ila kusema kwamba kazi hii ni muhimu sana na kwamba Katiba hii mpya ambayo twataraji kuwa nayo tukikaribia mwisho wa mwaka au mwanzo mwaka ujao ni mkubwa sana. Ni Katiba ya kwanza ambayo itakuwa Katiba inategemea maoni ya wananchi si Katiba ya 1963 ambayo iliandikwa huko Ulaya ikapitishwa bunge ya Uingereza badala ya bunge yetu hapa Kenya na kwa hivyo maoni yenu ni muhimu sana kwa ajili ya kazi hii. Sisi tutaandika lakini tutaandika kufuatia mapendekezo yenu na maoni. Nataraji kwamba kwa njia ya civic education providers, jamaa waliwapa elimu ya raia na pia wenye kamati ya C C C, Constitution Committees za kurekebisha Katiba mulipata elimu ya kutosha kuhusu yaliyomo katika Katiba yetu ya leo na mambo ambayo nyinyi mungependa yabadilishwe au yasisititizwe zaidi kwa nguvu. Lakini kabla ya kuendelea kuchukua maoni yenu, ningemukaribisha mwenye kiti wa hiyo kamati ambayo nimeitaja ambayo bila shaka wanachama wake mwawajua mukihusiana nao katika kazi hii ya kurekebisha Katiba. Kwa hivyo ningemukaribisha chairman mwenye kiti wa kamati mheshimiwa Bw. Munene atujulishe wenzake katika kazi hii na kusema jambo lolote ambalo angependa kusema kabla hatujaanza kukusanya maoni.

**Mr. Munene:** Asante sana Commissioner Prof. Idha na Commissioner Ratanya na D.O na wafanyi kazi wote ambao

mumeandamana nao wasaidizi wenu hapa na wananchi ambao mumekuja kwa jambo hili. Mimi nawakaribisha nikiwa mwenye kiti wa kamati ile ya sehemu hii ya ubunge juu ya mambo hayo ya kurekebisha Katiba. Kamati hii ilikuwa na wanachama kumi ambao watatu walikuwa ni lazima wawe pale kulingana na ile sheria ya bunge iliyopitishwa kwa hivyo wananchi wakachagua wale wengine saba wakatimia kumi. Sasa wengine wako hapa, wengine wako pale nje wanasaidia pale kwa kuandikisha wale wanaokuja lakini nitawataja kwa majina. Kwa upande wa dini kulikuwa dini zile kubwa hapa; ni Islam na Wakristo, tukapata wanakamati mmoja mmoja. Upande wa Islam akachaguliwa Hamad, yule pale. Upande wa Wakristo akachaguliwa Rev. Stephen Noma, yule pale.

Halafu tukawa na upande wa vijana na upande wa wale ambao ni walemavu. Kwa upande wa vijana akachaguliwa Dorogwa, yuko pale nje anaandikisha majina pale. Halafu akachaguliwa upande wa walemavu, Nimrod Kitoshe pia yuko pale nje. Halafu kwa upande wa akina mama ambayo sheria ilikuwa imesema lazima kuwe na akina mama, wasiopungua watatu. Sasa kuna mama ambaye anaitwa Dorothy Njoji Kitavi yuko, anaandikisha watu pale nje,anasaidia pale. Mwingine ni Judith Lenard Leshamta huyu hapa. Halafu mwingine ni Penina, sidhani kama leo yuko yeye pia ni mwenye kiti wa baraza la Taveta Town Council, Penina na Dodi Koleta Halafu na mimi baadaye walipoketi wakanichagua mimi nikawa mwenye kiti wao. Sasa kazi yetu tuliwafanyia mulituona tumewazungukia nyote mpaka sub-location mpaka location kila pahali. Tuliwaelezea kitu ya kufanya leo. Leo si mahali pakuja na hasira zile ulikuwa nazo. Leo ni siku ya wewe kusimama utoe maoni yako. Unaweza kutoa jinsi tulikuwa tukiwaelezea kwa njia tatu; uwe umeandika utapewa nafasi uingize utoe. Mwingine atapenda awe ameandika na anataka ataje mambo mengine kidogo kidogo pale, atapewa pia dakika zake kama tano. Mwingine atasema “mimi sisi sikuandika wala siandiki lakini nasimama niongee na mdomo wangu”, utapewa nafasi ueleze. Kwa hivyo ni hayo ambayo yanatakikana ninyi mufanye na mueleze mambo yanayogusa maisha ya mwananchi ya kila siku namujue sio Katiba ya Taveta munatengeneza, munatengeneza Katiba ya Kenya nzima. Kwa hivyo lile mtasema hapa mujue litagusa mpaka wale wengine ambao hawako hapa. Kwa hivyo mueleze maoni yenu, yatapokelewa. Ni hayo tu na tuko na D.O hapa nafikiri hata yeye pia angetaka nafasi anene. Asante sana.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana mwenye kiti kwa maelezo yako hayo. Kwa hakika umefanya kazi ambayo nilikuwa nafikiri kwamba nahitajiwa kuifanya ya kueleza wananchi hapa jinsi ambavyo tutakusanya maoni umekwisha waeleza. Bwana Munene kama alivyosema yeye kila mmoja wenu atapata dakika tano tu ya kutupa maoni yake akiwa hana memorandum, na akiwa ana memorandum atapewa dakika tatu tu. Hii ni kwa ajili ya wakati mfupi ambao tunao kati ya sasa na saa kumi na moja ambapo labda itabidi tumalize kazi yetu kwa leo. Kwa hivyo samahani ikiwa mwafikiri kwamba wakati huo ni mfupi sana, lakini mtafahamu kuwa hao wamejiandisha kutoa maoni ni wengi, na ikiwa tutampa kila mtu nafasi apendaye yeye, kwa upande wa kazi, hatutaweza kumaliza wote waliojiandikisha kutoa maoni. Nafiri tumekubaliana five minutes only.

Na tutaanza lakini kabla kuanza tumshirikishe Bwana D.O atoe maneno machache kutueleza maana amefanya kazi kubwa sana pia kuisailisha mambo na kuisadia kamati katika kazi zake za kuwatayarisha na kuwahamasisha katika kazi hii ya kurekebisha Katiba. Bwana D.O.

**Mr. D.O:** Asante sana Vice Chairman pamoja na mwenzake Commissioner Ratanya na wananchi kwa jumla, hamjambo?

**Response:** Hatujambo.

Yangu yatakuwa ni mafupi sana. Leo tumepata hao wageni wametutembelea kuchukua maoni kutoka kwenu. Yangu tu ni kuwakaribisha wao wajisikie huru na wajisikie nyumbani. Pili, ningependa kwa upande wa wananchi tafadhalini tuheshimu maoni ya mwenzetu. Kila mtu akitoa maoni yake ni maoni yake kama Mkenya hatoi maoni kwa niamba yako anatoa kwa niaba yake. Kwa hivyo tafadhalini tuheshimu maoni ya mwenzetu. Kila mtu akisema yake wacha aseme yake sikiza na wewe utoe yako na mwingine atoe yake.Usianze kusema aaah, nini, nini, kelele na vitu kama hivo.Hatuko hapa kufanya mambo kama hayo. Na pia tuwe na heshima kwa wageni wetu. Tusianze kupiga kelele au vitu kama hivo, tuwe watu ambao tumekomaa.Tatu Ma-commissioners ningependa kuwaambia nyinyi ya kwamba hapa kuna amani ya kutosha. Pengine mtu asiwe na shaka ya kwamba ooh itakuwa hii, itakuwa hii.Yale yaliyotendeka siku ile ya uchaguzi nadhani hayo yalipita na hao wamesahau na hakuna kitu tena mtaona ya aina ile maana ile ilikuwa ni mikutano wakuchagua wale viongozi na wakati wowote kama kuna uchaguzi you expect such things. Kwa hivyo nataka kuwahakikishia kwamba hapa kuna usalama, hapa kuna amani ya kutosha hao watatoa maoni yao vile ambavyo wamepanga na nadhani kila kitu kitaenda vizuri. Kwa hivyo mimi sitasema mengi sana ni kuwakaribisha ninyi na tafadhalini toeni maoni extensively. Usione Taveta vile Chaiman amesema usiangalie Taveta peke yake. Jua ya kwamba Mkenya yule mwengine anataka pia na wewe uchangie pale amesahau, na pale utakumbuka wewe na wewe uchangie pia. Kwa hivyo tafadhalini toeni maoni ya Taveta na nje ya Taveta. Kwa hivyo nasema asante sana karibuni sana. Asante.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana D.O kwa mashauri yako mazuri kuhusu jinsi ambavyo ni muhimu tufikirie democrasia na uhuru wa mtu kujisemea binafsi na kupewa heshima hiyo ya kujisemea bila ya kukatwa maneno yake. Nafikiri mwenzetu pale ataka kuuliza jambo.

**(Question inaudible)**

**Com.Salim:** Wajua tuna uongozi au guidelines tulizopewa, na lazima tuzifuate. Tusipozifuata itakuwa kila mtu kusema kwamba mimi nahitajia nusu saa wengine robo saa na tukifanya hivyo hatutaweza kuwamaliza wote ambao wamejiandikisha. Lakini kama alivyonidokezea mwenzangu hapa Bwana Ratanya, ikiwa una jamaa anayesema mambo ambayo labda tunaweza kumuongezea dakika moja mbili, tutafanya hivyo. Lakini kwa jumla lazima tuwe na very strict timing guidelines. Uongozi wa wakati lazima tuufuate kadiri tuwezavyo lakini hakuna haja ya kubishana juu ya jambo hili. Hebu tuanze na tutaona jinsi mambo yatakavyokuwa. Sawa? Asanteni.

Na sasa bila kupoteza wakati ningependa kumuita mwenzetu wa kwanza aliyejiandikisha kutoa maoni yake naye ni Bwana

Justin Fundi. Na tafadhali utaanza kwa kutaja jina lako. Tunanasa kila neno linalosemwa. Si kwa sababu yoyote nyingine, ni kuhakikisha kwamba maoni yako tumeyaandika na pia kunanasa kwenye tape ili tukirudi tusiwe tumesahau jambo tape itatukumbusha. Karibu.

**Mr. Justin Fundi:** Asante. Kwa majina yangu naitwa Justin Fundi Nkiratu. Na ninatoa maoni yangu juu ya kurekebisha Katiba hivi leo tarehe mbili mwezi wa tano 2002. Maoni yangu ni kama ifuatavyo;

Katiba ya Kenya inahitaji kuwa na utangulizi, na utangulizi huo uwe na muundo wa kitaifa. Kila kabila lililoko katika nchi ya Kenya ni lazima liheshimiwe na ni haki lipewe nafasi katika uongozi wa nchi ya Kenya hasa wa kisiasa na hasa ubunge.

Bunge la Kenya lisiwe na uwezo wa kubadilisha Katiba ya nchi kwa asilimia yoyote bila kuhusisha wananchi. Tuendelee kuwa na muundo waserikali ya Uraisi.

Serikali ya Kenya iwe na Rais na Waziri Mkuu.Serikali ya Kenya itakayoundwa, iwe na muundo wa majimbo. Serikali ya Kenya itayoundwa wakati ujao iwe na muundo wa umoja wa kitaifa.

Wabunge wafanye kazi wakifuata maagizo na mapendekezo ya wananchi waliowachagua. Ili mtu ahitimu kupigania ubunge, ni muhimu awe na umri wa mtu mzima kama miaka 41 na kuendelea wala si chini yake.

Mishahara na marupurupu ya wabunge ipunguzwe kwani sasa iko juu sana na wananchi washirikishwe katika kupanga mishahara na marupurupu hayo.Raisi aongoze kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano, majukumu ya Rais yaelezwe katika Katiba.

Utawala wa mikoa uendelee kama yalivyo sasa yaani Wazee wa mitaa, Manaibu wa Ma-chief, ma-chief, ma-D.O ama wakuu wa tarafa, ma-D.C ama wakuu wa wilaya, ma-P.C ama wakuu wa mikoa. Na napendekeza kwamba wazee wa mitaa wapewe marupurupu na serikali kwa ajili ya kazi nzuri zile ambazo wanafanyia serikali.

Mayor na wenye viti wa mabaraza ya miji wachaguliwe moja kwa moja na wananchi. Elimu ya chini kwa madiwani iwe darasa la nane na kwa wabunge iwe darasa la kumi na mbili.Uteuzi wa wagombea viti vya udiwani au ubunge ufanywe kwa wakati mmoja kwa vyama vyote vya kisiasa vinavyopigania uongozi katika jimbo la uchaguzi.

Katiba ya nchi ilinde kila mtoto anayefikisha umri wa kwenda shule na hasa apate elimu ya msingi bure. Uwezo wa kumiliki ardhi uachiwe wananchi wazalendo wazaliwa wa eneo hilo.Wananchi wafaidi moja kwa moja kutokana na faida ya mali iliyotoka katika eneo lao, ama kutokana na kazi inayofanywa katika eneo lile iwe inafanywa na serikali ama shirika lolote lile. Wakenya wasiwe na haki ya kumiliki ardhi kiholela popote pale.

Msimamizi na mkaguzi mkuu wa fedha za uma achaguliwe na bunge. Mali ya asili ifaidi mwananchi yule anayeishi pale mahali asili hiyo inapatikana. Serikali kupitia kwa wananchi ihusishwe katika kutekeleza sheria za uhifadhi mazingira. Mwananchi apewe uwezo wa kumiliki mali asili yote aliyo nayo.

Katiba isimamie usambazaji wa huduma za mashirika ili huduma hizo zifikie wananchi wote kuanzia kata dogo. Katiba ya nchi ya Kenya ilinde makabila madogo kutokana na unyanyasaji wa makabila na ugangamizaji wa makabila makubwa yaliyoko nchini Kenya. Katiba ipatie wanawake nafasi za kutosha bungeni na katika uteuzi wa uongozi katika nyadhifa bali bali katika nchi yetu ya Kenya.

Hapa Taveta ardhi kubwa ni ya watu binafsi kwa mfano Basil Criticos, Muhoho, Mama Ngina Kenyatta. Kwa hivyo tunaomba serikali itoe sehemu kama 20km mraba ili wananchi wapewe kwa ajili ya maendeleo ya Wataveta. Kwa ufupi maoni yangu ni hayo na ni meyatoa kwa kikundi cha watu ambao nimewaandikisha hapa.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana Justin Fundi kwa maelezo yako hayo na maoni yako. Na swali moja hapa kuuliza ya kufafanua tu. Wasema Parliament isibadilishe Katiba bila kuwashauri wananchi. Vipi Parliament yaweza kuwashauri wananchi? Kwa njia gani?

**Mr. Justin Fundi:** Kwa njia ya maoni.

**Com. Salim:** Yaani referendum? Referendum,asante.

**Com. Ratanya:** Umesema kwamba unapendelea serikali ya majimbo.Sasa hukutueleza vile unataka majimbo yapangwe. Ni kuwe na Central Government ama kuna mpangilio unataka ya majimbo?

**Mr. Justin Fundi:** Kwa sababu mimi sina utaalamu wa aina hiyo, kwa sababu nimetaja hivyo ninajua kwamba wataalamu wa kupanga uongozi wa aina hiyo wako.Kwa hivyo nikitaja hivyo watajua wafanye nini kwa ajili ya manufaa ya wananchi.

**Com**. **Ratanya:** Asante sana.

**Com. Salim:** Sasa namuita Bwana Gabriel Kichikiro. Karibu.

**Mr. Gabriel Selevai:** Kwa majina yangu matatu naitwa Gabriel Selevai Kichikiro, na niko hapa kwa ajili ya kutoa maoni yangu katika kuunda Katiba mpya ya Kenya. Na naanza kama ifuatavyo.

Kwanza ningependa Katiba hii itambue wazee wa kila constituency ama kila kabila, ili kwa ajili ya kusaidia serikali katika mambo ambayo wanaweza kuwa wanataka kuyafanya katika sehemu ile.

Na pili kila kabila katika Kenya iwakilishwe katika bunge. Lingine, kwa mfano, kuna makabila yale madogo ambayo si rahisi kutoa mbunge awawakilishe katika bunge. Kwa hivyo kama kutakua hakuna mbunge wa kabila hilo, katika uteuzi wa wabunge, paangaliwe lile kabila ambalo halijawakilishwa pale ndio ateuliwe ili kuwezesha makabila yote Kenya kuwa na mwakilishi katika bunge la Kenya.

Na katika constituency, yeyote yule atakayetaka kugombea kiti cha ubunge ama u-councillor ni lazima awe amechaguliwa na wale wazee ambao ni kabila zalendo wa pale. Wao ndio watamuidhinisha ili aweze kugombea hicho kiti.

Katika uchaguzi wa mayor au chairman wa mabaraza, ningependekeza kwamba achaguliwe na wananchi. na kama councillor ama Mbunge, kama atakuwa ametuliwa na wananchi lakini akawa hasaidii wananchi ama hafanyi mambo ambayo yanaweza kupendeza wananchi basi wananchi wawe na uhuru wa kumpigia kura ya maoni ya kumwondoa katika ule wadhifa ili wachague mwingine.

Serikali iwe na uwezo wa kutumia ardhi ya mtu binafsi kama kutakuwa kuna umuhimu, kama kuna kitu cha maendeleo kinataka kufanyika katika ardhi ya mwananchi. Lakini kuwe na ridhaa, kuwe na malipo ambayo si serikali tu impatie vile inavyotaka lakini kwa maelewano ili iweze kumridhisha yule mwananchi. Pia katika umilikaji wa ardhi kuna wananchi wengine katika Kenya wana mashamba makubwa makubwa, mahekari nyingi wakati kuna wananchi wengine hawana ardhi. Basi ningependekeza kwamba kiwango cha juu cha mwananchi wa Kenya kuwa na ardhi kubwa iwe haizidi heka mia moja.

Na pia ningependekeza kwamba kuwe na sheria au kanuni za umilikaji wa ardhi. Pasije tu mtu yeyote kutoka katika kabila lingine ama constituency ingine na kuja kumiliki ardhi mahali kwa sababu pengine ana pesa anaweza kununua ardhi kubwa. Pawe na sheria za umilikaji wa ardhi ambayo mamlaka zaidi yatakuwa yamependekezwa na wale wazee wa ile sehemu na pia wananchi wa pale ndio waweze kumruhusu yule mtu. Na ningesisitiza pia hapo kuwe na vizuizi vya kumiliki ardhi sio tu mtu yeyote kwa vile ako na pesa ama kabila yeyote anaweza kuja tu na kukaa na kumiliki ardhi popote pale. Kuna zile sehemu ambazo zinajulikana kwamba ni mahali kitovu pa lile kabila la pale basi mtu tu mwingine kabila lingine lolote lisiruhusiwe kumiliki pale.

Na ningependekeza katika Katiba hii mpya, pawe na serikali ya majimbo. Na pia katika uchaguzi kuwekwe sheria kwamba ni lazima kila Mkenya akate kadi ya kura na kama hujakata kadi ya kura pawe na sheria ambayo itakuadhibu. Na pia katika kupiga kura kuwe na lazima ya yule yeyote ambaye amekata kadi ya kura kupiga kura.Kama hatapiga kura pawe na sheria ambayo itamuadhibu. Mtu asiruhusiwe kupiga kura mahali ambapo yeye sio mzalendo wa hapo. Yaani kama wewe si Mtaveta pengine umekuja hapa Taveta kibiashara ama kikazi kwa vile swala la kupiga kura ni la kitaifa ikifika wakati wa kupiga kura

uende ukapigie kule kwenu mahali umetoka.Wale wananchi wa pale na kabila ya pale iweze kupiga kura ndio wanaweza kuchagua vizuri yule mtu ambaye watamtaka ataweza kuwasaidia.

**Com. Salim:** Umekaribia kumaliza?

**Mr. Gabriel Selevai:** Ndio.

**Com. Salim:** Uko karibu kumaliza?

**Mr. Gabriel Selevai:** Ndio. Katiba ya sasa iangalie sehemu za mipakani kwa sababu sehemu zote za mipakani katika Kenya ni sehemu ambazo ni nzuri kwa biashara, hivyo basi makabila mengi yanakuwa pale. Na wakija pale wengine wanajitambulisha kwamba wao ndio wa eneo ya sehemu hilo.Basi Katiba ichunguze kwamba hizo sehemu karibu na mipakani kabila la Pale linalo wazaliwa wa Pwani ni kina nani?

Na pia katika mali ya asili maji, misitu, national parks, maziwa ama lakes na ufuo wa bahari. Kama kuna pesa za kigeni ambazo zinaletwa na watalii kuangalia sehemu hizo, tafadhali wale wenyeji wa pale pia wawe na asilimia wanapata.

Katika uteuzi wa mabarozi, ma-permanent secretaries na ma-directors kuwe kunaangaliwa pia makabila hata yale madogo yaweze kuteuliwa.

Katika mambo ya elimu ningependekeza kwamba isambazwe vizuri katika sehemu zote ikiwezekana kila mkoa upate chuo kikuu.

Na katika interviews pengine kuchagua ma-askari, askari jeshi na kadhalika, pasichaguliwe tu kwamba tunaenda pale Taveta tunaenda kuchukua watu kumi. Ningependekeza kwamba kila kabila ambalo liko Kenya, kuwe na percent ambayo kila kabila lazima lichukuliwe liwakilishwe. Tofauti na vile ambavyo utakuta katika jeshi la Kenya kuna kabila fulani ndizo ziko na wakilishi wengi.

**Com. Salim:** Saa zimekwisha.Una memorandum au ni zako kwa mdomo? Kwa maoni yako?

**Mr. Gabriel Silivei:** Eeh. Ni maoni yangu kwa mdomo.

**Com. Salim:** Eleza tafadhali kwa haraka.

**Mr. Gabriel Silivei:** Ningependekeza umeme na maji ziko juu sana hivyo basi mwananchi wa kawaida hawezi kumudu.

Iwekwe katika hali ile ya mwananchi wa chini sana anaweza kuweka umeme na pia kunywa maji safi. Na pia Katiba hii iangalie sehemu zote barabara zitengenezwe. Kwa ufupi hayo ndiyo maoni yangu ambayo nimekuwa nayo.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana Gabriel kwa maoni yako tafadhali utaji-register pale kuonyesha kwamba umetoa maoni yako na kama muonavyo mpaka sasa tumeanza vizuri sana. Kila mwananchi ana maoni juu ya mambo tofauti tofauti, maswala tofauti tofauti na ndivyo tungependa kuendelea leo. Uwe na swala maalum ambapo wewe una mapendekezo juu yake, badala ya kueleza ile background na historia ya lile tatizo na kulalamika na kushtaki, tupe maoni yako juu ya maswala yako. Moja baada ya moja. Asanteni.

Tukiendelea mbele tunaye dada yetu wa kwanza kutupa maoni yake, Dorothy Mnene ambaye pia nafikiri ni member wa kamati. Na hili ni swala muhimu kweli kwamba ningependa maoni kutoka kila sector kwa wananchi; kina mama, wazee, vijana, walemavu na dini tofauti tofauti ili kwamba tusije tukalaumiwa baadaye kwamba tumewasikiza wanaume peke yao wengi kuliko kina mama. Karibu Dorothy Mnene. Tafadhali utaanza na jina lako.

**Dorothy Kitavi:** Mimi naitwa Dorothy Njoji Kitavi. Mimi ni mkazi wa Taveta Bomeni location natoka sub-location ya Mahovu.

Nilianza na haki za makabila madogo madogo. Bunge; kuwe na sheria ya kulinda haki za makabila madogo kuona ya kwamba makabila yote yaliyoko Kenya sauti zao zinasikika bungeni na mwenyeji wa sehemu hiyo ndiye anayeingia bungeni maana Kenya ya sasa, ni wengi wape na wanyonge wanasahaulika na haki zao hazitiliwi maanani. tunataka sheria ya kutetea wanyonge, kila mwenyeji atetee kiti cha bunge ili sehemu aliyotoka iwe na sauti.

Serikali za mitaa. Viti vyote vya mabaraza viwe vya wenyeji wa sehemu ile hata kazi zote katika mabaraza hayo ili kulinda haki za wanyonge na (?) madogo ambao pia ni wenyeji.

Muundo wa aina ya serikali: Tufuate muno muundo wa majimbo ambapo mamlaka ya nchi na bunge yamegawanywa baina ya serikali kuu na majimbo. Muundo huo utahakikisha kwamba mali na rasilimali iliyoko hapo itafikia wananchi wa sehemu hiyo badala ya kwenda juu ndiyo irudishwe chini. Na kufanya hivyo itasaidia kulinda makabila madogo.

Ukuu wa Katiba: Wabunge wasiwe na uwezo kabisa wa kugeuza Katiba. Wananchi wawe ndio wanahusika katika kubadilisha Katiba kupitia mikutano ya maoni. Mikutano ya maoni iongozwe na tume maalum itakayoteuliwa kufanya hivyo.

Bunge: Bunge lipige msasa na darubini uteuzi wa maofisa wafuatao; mawaziri, ma-permanent secretaries, wakuu wa majeshi, ma-Judge wakuu, watafiti tofauti tofauti na kadhalika kulingana na elimu yao na uwezo wa kuendesha hiyo kazi isiwe wewe nakujua au ni rafiki nakupa kazi.

Hatua maalum za kuongeza kushiriki kwa wanawake bungeni yani affirmative action iwepo ili kusaidia kuona akina mama wengi wameingia bungeni. Nominated MPs wengi wawe akina mama au viti vigawanywe viwe sawa kati ya wanaume na wanawake. Mishahara na marurupu, wananchi wawe ndio wataoamua kwamba wabunge waongezwe kiasi gani ama wasiongezwe.

Tuwe na muundo wa vyama viwili au idadi ya vyama viwili cha utawala na cha upinzani maana vingi katika Kenya sasa ni vya kikabila.

Rais awe na uwezo wa kura ya turufu kuzuia sheria iliyopitishwa na bunge ikiwa hiyo sheria inagandamiza wananchi au itahatarisha nchi au italeta kutoelewana.

Mamlaka ya nchi: Raisi awe na kipindi maalum cha kuongoza na viwe ni vipindi vitatu vya miaka mitano. Baada ya hapo asiruhusiwe kusimama tena yani iwe ni vipindi vitatu vya miaka mitano mitano. Raisi awe mbunge wa kutoka sehemu fulani.

Haki za akina mama, affirmative action. Sheria hiyo iwekwe ili kuona kina mama wamepewa haki sawa katika bunge na kazi zingine zozote. Affiliation Act irudishwe tena ili haki za akina mama zilindwe na yeyote atakayetia msichana mimba amlee huyo mtoto mpaka atimize miaka ishirini na moja ambapo atakuwa amemaliza chuo kikuu.

Usawa: Kuwe na usawa kati ya wanaume na wanawake na haki za kina mama zilindwe katika kila ngazi.

Taxation yani kuridhiwa au kuridhi mali. Sheria za kimila zinazo bana akina mama ziangaliwe, zilizo baya zitolewe na nzuri ziachwe kama vile kutahiri wasichana hizo ni mila ambazo zimeisha wakati wake. Akina mama wasirithiwe kwa nguvu. Mama awe ndiye anayerithi na kusimamia mali ya bwana kwa niaba ya watoto na ikiwa mama hana maadili mema serikali ichague watu watakaosimamia mali hiyo ama jamii ya mji ule wawajibike

Kuachana ama divorce: Mke na mume wanapoachana mali iliyoko kwenye mji igawanywe sawa kwa sawa. Ndoa marriage.Ndoa zote zikubaliwe. Ikiwa ni ya kienyeji, ya kanisa, ya D.C, Kiislam, Kihindu na njoo tukae or come we stay. Maana utaona wasichana wengi sana wameolewa, mtu ameolewa na mvulana wameketi naye kiasi cha miaka mitatu baada ya miaka mitatu kwa ajili ni come we stay anamfukuza. Nafikiri ndoa kama hiyo pia ilindwe ili wasichana kama hao wasiwe wananyanyasika.

Kuoa mke wa pili. Baba wengi sana huwa wanaoa wake wa pili. Ikiwa mwanamume ataoa mke wa pili, haki ya mama wa kwanza ilindwe na ikiwezekana mali ile ya kwanza iwe ni ya bibi wa kwanza. Atakapooa mke wa pili wachume naye mali ingine ile ambayo itagawanywa kati ya hao watatu.

Mali za familia, family property; Mali za familia  majina ya mume na mke lazima yaandikwe yote pamoja katika vyeti vya kumiliki mali hiyo.

Martenity leave: Mapumziko ya uzazi yawe ya miezi mitatu siku za kufanya kazi.

Mahali: Iwe ni uwezo wa kijana au mapatano kati ya kijana na wazazi wa msichana.

Domestic violence yaani vita vya kinyumbani. Serikali iwe na sehemu maalum ya kuwahifadhi hao wamama mpaka watakapoweza kujisimamia wao wenyewe. Katika kituo cha usalama kuwe na sehemu ambayo imetengwa kusikiza malalamiko ya aina hiyo maana mama wengi sana wanapoenda polisi huwa wananyanyasika kwa yale maswali ambayo wanaulizwa ambayo hayafai. Waume wenye kutenda vitendo kama hivyo washtakiwe na kufungwa.

Ubakaji, incest, sodomy: Atakaye baka msichana chini ya miaka kumi na nne afungwe maisha, kutoka miaka kumi na tano kwenda juu afungwe miaka kumi na mitano. Mtu wa ukoo atakapotenda kitendo hicho afungwe maisha yaani incest. Na atakayefanya kinyume cha sheria afungwe maisha yani sodomy. Na wakati wa kufanya mambo hayo ya juu na alikuwa anajua ana ukimwi anyongwe, maana sasa yule ashamuua yule mwingine.

Haki za ardhi na mali ya asili. Kila mwananchi awe na haki ya kumiliki ardhi na mali yoyote ikipatikana katika ardhi yake na pia ahusishwe kama vile madini na vitu  kama mafuta, maana serikali ndio inamiliki vitu kama hivyo.

Mbuga za wanyama ziwe game reserve ili wananchi wa sehemu hiyo wafaidi na ikiwa haiwezekani asilimia hamsini iingie wilayani husika.

Maji: malipo ya maji yailipwe kulingana na eneo maji yametoka, na eneo yanapopelekwa yatofautishwe maana kwa mfano hapa Taveta maji yanatoka Taveta. Kwa nini nilipe kama mtu anayepelekewa maji Mombasa? Unaona kwamba hapo pia kuna unyanyasaji wa aina fulani maana maji ikiwa inatoka eneo langu inategemea kwamba maji yale mimi nilipe pesa kidogo kuliko yule anayepelekewa kutoka ile sehemu ambayo maji yametoka.

Elimu: Elimu ya msingi iwe ya bure  na ya secondary iwe kiwango wananchi wanaweza kujimudu na ya chuo kikuu isimamiwe na serikali kama vile zamani ili watoto wanaotoka katika jamii maskini waweze kusoma.

Ajira.Wakati wa ajira kuwe na usawa kijinsia na kikabila. Kwa mfano utasikia majeshi yanachukua watu. Ukienda sehemu ingine wanapewa watu mia moja. Ukija sehemu kama hii wanapewa watu ishirini kweli kuna usawa? Hakuna usawa. Sasa tunataka ikiwa ni kuandikwa kazi kuwe na usawa kwa kila district au kwa kila tarafa ama division.

Matibabu yawe ya bure kabisa kwa kila mwananchi hasa mama wajawazito, wazee, watoto na walemavu. Asanteni. **(clapping).**

**Com. Salim:** Asante sana Bi Dorothy Mnene kwa maoni yako. Sasa tutamuita Hamadi A. Mnene.

**Mr. Hamadi Mnene:** Kwa majina jina langu mimi ni Hamadi Anael Mnene kutoka uwakilishi bungeni Taveta. Maoni yangu nilikuwa nimeandika kwamba mimi sitatoa maoni kwa mazungumzo, ni written. Kwa hivyo nitapeana tu hii makala.

**Com. Salim:** Sawa lakini unazo dakika zako tatu utupe zile points kwa ufupi.

**Mr. Hamadi Mnene:** Okay. Katika upande wa maoni yangu muundo wa serikali ningependa serikali ya majimbo ambapo mamlaka ya nchi na bunge yamegawanywa baina ya serikali kuu na serikali ya majimbo maalum.Kwa sababu kabila ndogo hazinufaiki na serikali kuu ya uraisi isiyokuwa na majimbo hivyo basi kila jimbo litatawaliwa na governor wake na raisi atakuwa ndiye kiongozi au mwenye kiti wa serikali kuu.

Kwa upande wa mamlaka ya nchi raisi awe na kipindi maalum cha uongozi kipindi hicho kiwe baina ya miaka mitano kwa vipindi viwili.

Kadhi mkuu lazima awe na elimu ya dini ya kutosha ya Koran na awe na shahada kwa elimu hiyo ya sheria na pia lazima achaguliwe na waislamu wenye taaluma wenye elimu sio Raisi. Mahakama ya kazi iruhusu washtakiwa kukata rufaa ama rufani.

**Com. Salim:** Inaudible

**Mr. Hamadi Mnene:** Sheria za vagrancy zirudishwe kwa sababu watu wamekuwa wakizagaa zagaa nchini ovyo ovyo bila kazi maalum nchini hivyo bila kuwa na kazi watu wengi wanavunja sheria na vitendo vya uhalifu vinaendelea.

Kwa upande wa serikali za mitaa: Mayor mwenye kiti wachaguliwe na wananchi. Mwananchi awe na haki ya kumrudisha mbunge nyumbani na diwani wake kwa kupitia kwa chama kilichomchagua. Atakayekata kauli ya marupurupu ya wabunge awe mwananchi.

Muundo wa uchaguzi: Wagombea viti wanaokosa kuteuliwa na chama kimoja wasiruhusiwe kuhama vyama vyao na kwenda katika vyama vingine. Kuhusu uhamaji wa kutoka chama kimoja hadi chama kingine, vyama vya upinzani kujiunga na chama cha serikali, ni lazima akubali kuapishwa kwamba hata hama tena kwenda chama kingine.

Haki za kimsingi. Raisi ndiye anayepasa kuwa na jukumu la kuhahakisha kwamba Wakenya wote wanafurahia haki za msingi

kama vile usalama, afya, maji, elimu, makazi, chakula na ajira.

**Com. Salim:** (inaudible)

**Mr. Hamadi Meme:** Kwa hivyo hizi nilikuwa natoa ni points. Kwa hivyo niwe nimemalizia hapo.

**Com. Salim:** Maliza lakini points in short (?).

**Mr. Hamadi Mnene:** Serikali itoe chakula kwa shule na hospitali na vinginezo serikali itoe miradi kwa wananchi wa mashambani ili wawe na miradi ya maji kuzuia njaa badala ya serikali kupeana vyakula kwa wananchi. Hivyo wananchi wa sehemu zilizo na mashamba mazuri wapewe maji ili waweze kujihudumia wao wenyewe.

Elimu: Swala la elimu iwe bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne na wanapofika chuo kikuu wawe wanapewa elimu kwa marupurupu kidogo.

Makazi: Swala la makazi linastahili kutiliwa maanani sana kwa kuwa kuna shida kwa watu wanaotoka sehemu zao za asili na kwenda kukaa katika ardhi za watu wengine ambao ardhi hizo huwa wamezitenga kwa ajili ya vizazi vyao vijavyo kwa hivyo wenyeji wapewe uwezo wa kulinda sehemu zao. Nafikiri kwa hayo nashukuru.

**Com. Salim:** Asante Bwana Hamadi Mnene kwa maoni yako. Sasa ni Bwana Raphael M. Mesula.

**Mr. Raphael Mesula:** Mimi ni Raphael Mesula Masamu, kwa kabila ni Mtaveta. Na nimeandika maoni yangu sikutaka nizungumze lakini kwa kuwa nimepewa zile dakika tatu nitagusia sehemu kama tatu.

Muundo wa serikali: Ningependa serikali ya majimbo sababu ni kwamba katika kila jimbo kuna makabila ya asili yanaoishi katika kila jimbo na kukiwa na majimbo tutazuia watu kuhama hama kwa kabila kutoka jimbo lingine au wilaya ingine kwenda wilaya ingine na jambo ambalo linasuzusha ugomvi wa kikabila.

Jambo lingine ni kama hivi leo tunatoa maoni ya kurekebisha Katiba. Mila hii imeanzishwa sasa na tunaomba iendelee ili mwananchi ajisikie ana changia katika kuunda maongozi ya nchi.

Utoaji wa uraia: Jambo hili tungeomba Katiba ya sasa ilinde sana na ichunguze sana hali ya kutoa uraia kwa sababu serikali ya sasa inatoa uraia kiholela holela na hata utakuta majambazi wengine wamefanya uhalifu huko kwao wanakuja pia wanadai kuishi na sisi katika sehemu yetu kisha wanazusha ujambazi.

Mtoto akizaliwa katika sehemu ningependelea kwa maoni yangu, akishafika umri wa miaka kumi na minane hapo ndipo afikirie

kuitwa raia wa pale kama wazazi wake walihamia, siyo mtu anakaa miaka mitano anaitwa raia wa pale.

**Com.Salim:** Ungependa miaka mingapi?

**Mr. Raphael Mesula:** Miaka kumi na nane, aishi pale kwa lile eneo ndio sasa aitwe raia wa pale.

Vyama vya kisiasa. Mimi kwa maoni yangu nilikuwa napendelea vyama ikiwezekana visizidi vyama viwili au vitatu, sababu yenyewe tumeona mfano wa hivi vyama ambavyo viko vingi sasa, vimekuwa ni vyama vya kikabila wala havina malengo au mwelekeo wakutetea haki za wananchi.

Bunge: Ningependelea kusema kwamba ingawa twasikia eti vijana wapewe uongozi wa kuongoza mimi ningeomba kijana ama mtu atakayeweza kugombea ubunge awe na umri wa miaka thelathini na sita au arobaini. Na mtu akitaka kugombea uraisi awe na umri wa miaka hamsini sio mtu wa miaka arobaini anataka uraisi au wa miaka arobaini na tano. Miaka hamsini hiyo mtu akili yake imeanza kukomaa na anaweza kuwa na maamuzi yenye hekima na busara.

Katika masharti ya wagombea viti vya bunge hata uraisi, nina mashati kadhaa hapa; Kwanza, mtu awe na elimu ya kiwango cha kidato cha nne na kwenda mbele. Pili, mgombea asiwe amewahi kupatikana na hatia ya mauaji, wizi, ufisadi, ulevi, asiwe ni mtu mlevi au mnyang'anyi.

Mamlaka ya nchi. Ningependa vipindi vya Raisi viwe viwili miaka mitano mitano, sababu ni kwamba watu wengine wakishashika kiti anapenda kukaa pale hata akiwa na makosa anapenda azidi kukaa pale aweze kuyafunika yale makosa.

**Com. Salim:** Dakika zako tatu zinakaribia kuisha.

**Mr. Raphael Mesula:** Wacha nimalizie ya mwisho ambayo ni ya muhimu.

Kuhusu ardhi, napenda kusema ya kwamba Wataveta hawana ardhi. Naomba Katiba ya sasa igawanye sehemu ya mbuga la wanyama National Park, ikate iwapatie Wataveta sababu sehemu kubwa ni ya Muhoho na sehemu kubwa ilikuwa ni ya Basil Criticos. Asante.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana Mesula kwa maoni yako na memorandum yako. Bwana Mesula tafadhali kabla hujamaliza pale, swala moja au maswali mawili kutoka kwa mwenzangu Bwana Ratanya.

**Com. Ratanya:** Bwana Mesula, ni kuhusu umri wa MP, unasema lazima awe miaka 36 kuchaguliwa. Unapendekeza mwisho? Na vile vile President unasema 50 years kuanza, unaweza pendekeza kiwango cha mwisho?

**Mr. Raphael Mesula:** Asante sana. Kiwango cha mbunge, vile nimesema umri wa miaka 36, yamaanisha ujana wa mtu unaanzia miaka kumi na nane mpaka 36 unaisha. Sasa kuanzia 36 anaanza kuingia kiwango cha utu u1zima ndio ninapendekeza aanzie hapo mwisho itategemea uhusiano wake na raia. Raisi kwa kuwa nimeshataja vipindi viwili vya miaka mitano mitano vya Raisi kuhudumu, sasa hivyo vipindi hata nisiposema mwisho, vitamwondoa.

**Com. Ratanya:** Swali lingine, umesema National Park imekuwa kubwa zaidi, unataka kupendekeza ni kiasi gani ya National Park unataka ipatiwe Wataveta, ni sehemu gani? Kama nusu, kama vile vile unataka iwe nini?

**Mr. Raphael Mesula:** Asante sana. Kwa vile sasa kizazi cha Taveta kinaongezeka na ukweli ni kwamba sehemu hizi mbili zimeshamilikiwa na watu binafsi wawili.Wataveta wamesongwa sana na kama ingewezekana tukipewa kama hekari elfu mia moja ili tusije tukiomba omba na kesho tuombe na kesho tuombe. Hekari elfu mia moja zipewe Wataveta. Nasisemi eti makabila yanayoishi Taveta, nasema makabila asili ya Wataveta waweze kupatiwa hiyo sehemu.

**Com. Salim:** Umesema kwamba ungependa desturi hii ya kurekebisha Katiba iendelee, iendelee vipi kwa njia ya elimu ya raia kwa vipi hasa?

**Mr. Raphael Mesula:** Elimu hii ya kutoa maoni ya raia kwa tume ya marekebisho ya Katiba ningependa kama wakikaa, serikali ikikaa au bunge likihudumu kwa muda wa miaka pengine kumi na mitano, ishirini, wakiona kuna jambo linatakikana kurekebishwa isiwe ni bunge au wabunge kiholela holela kule wanaenda na wanatoa kipengele fulani wanakirekebisha bila wananchi kuhusishwa kwa sababu wabunge wengine wanaweza kuwa na sababu zao za kibinafsi kutetea masilahi yao na hayahusu raia ama uma, basi wakakimbilia tu kurekebisha. Katiba ya sasa imesharekebishwa zaidi ya mara thelathini na tano.Mwananchi hajahuzishwa na yale waliyoko pale pengine hayamhusu mwananchi wala hayamsaidii mwananchi ndio ninatoa sauti.

**Com. Salim:** Yaani ikiwa kuna haja kurekebisha Katiba ni wananchi ambao wataulizwa kwa njia ya..

**Mr. Raphael Mesula:** Ya maoni.

**Com. Salim:** Referendum?

**Mr. Raphael Mesula:** Yaah

**Com. Salim:** Okey, Asante. Bwana Jomo Sikiondo.Karibu.

**Mr. Jomo Sikio\ndo:** Mimi ni Jomo Sikiondo mimi natoa maoni yangu.

Kwa ubunge: Mbunge awe ni raia wa kabila la Taveta (**Interjection)** awe ni mwananchi wa Taveta. Ningependekeza kwamba elimu ya kuanzia darasa la kwanza mpaka std 8 liwe free. Lingine ni mambo ya hospital. Hospitali tunataka iwe bure kwa sababu tumeona kwamba hatuna uwezo wa kuweza kulipa hiyo bill ya hospitali kwa sababu tunaona karo ni kubwa sana na hatuna chochote kile cha kuweza kulipa hospital. Hospital iwe bure.

Halafu pili, mambo ya ardhi. Ardhi tunataka kuomba tuko na ardhi kama hii ya Basili inatakikana iangaliwe upande wa wananchi, kama ni kugawanyiwa wagawanyiwe mtu apate ardhi kulingana na kama heka mia moja , isizidi mia moja heka kila mtu apate.

**Com. Salim:** Hao walio na zaidi ya mia moja?

**Mr. Jomo Sikiondo:** Ipunguzwe.

Halafu tunataka serikali ya majimbo kwa sababu serikali ya Moi sisi tumeona kwamba tukiangalia kama sehemu za Pwani hatuna hata chuo kikuu. Kwa hivyo tunaona kwamba endapo tutakuwa na serikali ya majimbo, kuna vitu kama chuo kikuu tutapata na hata mambo mengi tutapata. Lakini tukiwa serikali moja hii inaitwa kama chama cha KANU hatuwezi kuambatana na (?). Tunataka serikali ya majimbo ili kila mwananchi apate mkate kutokana na serikali iliyoundwa ya majimbo.

Halafu kuhusu ma-chief, ma-chief mimi ningependa kwamba wapigiwe kura.

Pili ningependekeza kwamba kuwe na maendeleo ya akina mama. Maendeleo ya akina mama iangaliwe mbele kwa mkazo zaidi kwa sababu unakuta mradi unakuja kama sehemu moja tu kama hapa huwezi kufika. Kwa hivyo tunataka miradi kama hiyo inayotolewa iletwe moja kwa moja mpaka kwa sehemu inayotakikana iwafikie wananchi. Yangu ni hayo kwa sasa.

**Com. Ratanya:** Hii sehemu ya mwisho unasema maendeleo ya wanawake unaweza kufafanua kwa sababu hatukuelewa vizuri?

**Mr. Jomo Sikiondo:** Maendeleo ya wanawake unakuta pesa kama ile inatolewa na serikali unakuta ile pesa haikufikia wananchi, wa kile kikundi. Ile pesa labda serikali imetoa imegawanywa kila mradi ipate, kama Taveta ipate sehemu zingine zipate lakini unakuta kikundi kama hii ya hapa Taveta haiwezi pata hiyo pesa

**Com. Ratanya:** Yaani branch ya maendeleo ya wanawake wapate hiyo pesa?

**Mr. Jomo Sikiondo:** Yaah, branch ya maendeleo ya wanawake wapate mazao hiyo yote inayotoka kwa serikali. Tena ma-chief napendekeza wawe wakichaguliwa na wananchi. Na wasaidizi wake kama hao wengine watawala wengine kama D.O, D.C, na kuenda juu kama P.C, hao tu wawe wakichaguliwa na serikali lakini hao wengine kama Ma-chief mtu tunakaa naye karibu lakini unakuta saa zingine, labda kumekuwa labda mgwaruzano na watu kwa hivyo amekaa kwa muda mrefu kwa hiyo kipindi. Kwa hivyo angetakikana ili abadilishwe kwamba kutakua na mwingine apate hiyo hatamu, kwa hivyo asiwe ni yeye kwasababu akiwa ni yeye, atazidi kufunika mambo mengine. Kwa hivyo awe kwa kipindi, kama ni kupigiwa kura apigiwe kura kwa kipindi, kama ni miaka mitano, aendelee na hiyo akimaliza, apigiwe tena kingine miaka mitano, isizidi kumi.

**Com. Salim:** Asante Bwana Sikiondo kwa maoni yako. Tukiendelea mbele twamuita Bwana Shadrack Kumberi.

**Mr. Shadrack Kumberi**: Mimi ni Shadrack Makau Kumberi, ni Mtaveta halisi. Mimi nataka serikali iwe ya majimbo. Mbunge kijijini, mashambani na awe ni mwenyeji asili.

**Com. Salim:** Mwenyeji asili wa Taveta au popote?

**Mr. Shadrack Kumberi**: Mtaveta awe asili wa hapa.

**Com. Salim:** Endelea.

**Mr. Shadrack Kumberi**: Serikali za mitaa. Wagombea viti lazima wawe wenyeji asili. Ndovu akiingia kijijini raia wamuue.

**(Noisy interjection)**

**Com. Salim:** Pembe zake wazifanye nini?

**Mr. Shadrack Kumberi:** Pembe zake wapeleke kwa D.O, kwa serikali.

**Mr. Shadrack Kumberi:** Wazee wa board wawe ni Wataveta asili.

**Com. Ratanya:** Endelea.

**Mr. Shadrack Kumberi:** Imeisha.

**Com. Ratanya:** Imeisha.

**Mr. Shadrack Kimberi:** Yaah, asante.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana Shadrack Kumberi.Bwana Wilson Sagurani? Wilson Sagurani?

**Mr Wilson Sagurani:** Mimi ni Wilson Sagurani na natoka Bomeni location.
Mwanzo nataka serikali ya majimbo. Upande wa ubunge, lazima kuwe na masharti ndiyo mtu apiganie kiti cha ubunge. Kwa mfano, sehemu za mashambani kama hapa Taveta, sioni sababu kwa nini mtu ambaye siyo mwenyeji asili aruhusiwe kugombania kiti cha mahali kama hapa. Mimi nasema hivyo maana unakuta kuna karibu miaka 35, Mtaveta ameshindwa kujichagulia mtu wake kutokana na udogo wake. Sasa wahamiaji wamekuwa wengi kiasi kwamba wao wanaungana wanapitisha Mbunge wao wanamnyima Mtaveta asipate nafasi yake ya kuchaguliwa.

Pia ningetaka raia wawe na ruhusa ya kumrudisha Mbunge wao nyumbani kama hatawajibika kutokana na ahadi zake alizo ahidi. Wawe kupitia chama kilichomchagua.

Ningetaka kuwe na serikali ya mseto kama hakutakuwa na chama kilichoshida kwa idadi kubwa inachokiwezesha kuunda serikali. Na chamber za bungeni ningetaka ziwe mbili, senate na hiyo sehemu ya wakilishi wa sehemu fulani

**Com. Ratanya:** Rudia hapo

**Mr. Wilson Sagurani:** Ningetaka chamber za bunge ziwe mbili. Kuwe kuna Senate ambayo ileitakuwa ni ya ma-governor, na kuwe kwa hiyo mtu amechaguliwa katika eneo lake.

Mamlaka ya nchi. Ningetaka utawala wa mkoa uwe chini ya governor. Governor naye aweze kuchagua hao wengine wanaofuata chini kama kina D.C, D.O, na Ma-chief. Na hasa kwa watu kama ma-chief na ma-sub-chief ningeomba wawe ni wenyeji asilia wa sehemu hiyo au tarafa hiyo.

Serikali za mitaa: Wagombea viti vyote katika serikali za mitaa ningetaka wawe wenyeji asilia wa hiyo sehemu.

Muundo wa utaratibu wa uchaguzi: Mbunge ama Councillor yule atayekuwa na kura nyingi awe ndiye mshidi. Lakini kwa uraisi, ningependelea lazima apate kura nyingi kiliko wenzake na pia awe amepata asilimia thelathini kwa mikoa sita nchini Kenya.

Haki za kimsingi. Masharti kuhusu haki za kimsingi hayatoshi. Kwa hivyo ningeomba yaongezwe. Moja ya hayo ningependa yaongezwe ni kama haya. Haki ya kila kabila kuwakilishwa bungeni. Haki ya kila kabila dogo kuchagua councillor wao bila kuingiliwa na watu wa makabila mengine wanaoishi katika eneo hilo.

Haki ya ardhi na mali. Ardhi yote iwe mali ya wenyeji asilia. Serikali isiwe na uwezo juu ya ardhi ya mtu binafsi. Mtu akiwa na shamba kubwa zaidi ya hectare mia moja na yeye sio mwenyeji asilia wa eneo hilo ningependelea alipe kodi wenyeji asilia.

Makabila mengi Kenya walikuwa na wazee ambao walikuwa na mamlaka juu ya ardhi ya eneo lao. Huo uwezo ulikuja ukapokonywa, ma-D.O wakauchukua huo uwezo na ma-chief wakachukua huo uwezo. Ningeomba hawa wazee warudishiwe huo uwezo wa kusimamia ardhi yao. Kwa mfano kama hapa Taveta kuna wazee tulikuwa tunajua, tulikuwa tunawaita wazee wa njama ndio walikuwa wanauwezo juu ya ardhi yote hapa Taveta. Hao wazee ningeomba wapatiwe uwezo wa kusimamia ardhi ya mahali kama hapa Taveta.

Title deeds: ningependelea zitolewe kiwango cha tarafa. Sio Title deed inatoka Nairobi wewe umekaa hapa Taveta mtu anatoka na title deed Nairobi hujui ameipata vipi anakuja anakwambia hapa ni kwangu. Sasa unashindwa kuelewa kwamba huyu mtu amepata Title deed vipi na mimi ndiyo nilikuwa nikiishi hapa pahali kwa muda wa miaka arobaini hata zaidi.

Mkenya aruhusiwe kumiliki ardhi popote alimradi hiyo ardhi awe ameipata kihalali. Kwa mfano kama ameinunua awe ana haki ya kuimiliki.Lakini, kuna baadhi ya watu mtu anaenda eneo la wenyeji anaenda tu anaingia anajikatiasehemu ya ardhi na kisha huyo mtu anataka apatiwe cheti ya kumiliki hiyo ardhi. Hiyo ndio ningesema haiwezekani ikataliwe. Watu kama hao ambao huenda kwa maeneo ya wenyewe na kujikatia masehemu ya mashamba wakidai hao ningeomba serikali iwarudishe yaani hiyo sheria ilikuwa ya kurudisha watu vagrant irudishwe.

Haki za jamii: Ningeomba Katiba ilinde haki za jamii yani makabila madogo yalindwe. Na ningeomba yalindwe kivipi? Kwa mfano kuna makabila ambayo ardhi kwao either kutokana na wingi wao hiyo ardhi yao imekuwa kama haiwatoshi ama pengine ardhi yao inakuwa ni kame. Hao watu wanakimbilia kwa eneo la wengine wanavamia mashamba wanajigawanyia na wanadai hapo mahali. Ukimuuliza anakwambia mimi ni Mkenya nina haki ya kumiliki ardhi yote lakini hakuipata kwa njia halali.Ameipata kwa ile kwamba ameenda pale kwa vile yeye ni Mkenya. Sasa kitu kama hiki serikali iangalie sana iwe inalinda makabila madogo dhidi ya kunyanyaswa na watu kama hao.

**Com. Salim:** Umekaribia kumaliza?

**Mr. Wilson Sagurani:** Eeh. Pia ningesema upande wa ndoa: Mtu akioa bibi, certificate za marriage ziwe zinatolewa tu hapa kwa D.O sio lazima kotini au sio lazima kila mtu aende kwa D.C, D.O hapa awe anaruhusiwa kupeana marriage certificate.

Pia ningeomba serikali isiwe kama inalemea upande wa dini moja. Maana ukiangalia serikali hairuhusu mtu aliye wa bibi wawili kupata marriage certificate ila mtu mmoja. Ambao kama kwa dini ya Kiislamu inaruhusu mtu apate marriage certificate kama ameoa bibi hata mpaka wa nne. Sasa ningependa mtu aliye wa bibi mmoja ama wawili wote wapatiwe marriage certificate.

**Com. Salim:** Muislamu na asiye Muislamu?

**Mr. Wilson Sagurai:** Muislamu na asiyekuwa Muislamu. Ni hayo. Nimemaliza.

**Com. Salim:** Sagurani ngojea kidogo kuna swali moja.

**Com. Ratanya:** Kuna swali moja ya kufafanua hapa kuhusu marriage. Unasema mtu akioa hata wanawake wengi apatiwe marriage certificate kulingana na wale ameoa. Ungetaka kupendekeza kiwango gani kwa sababu Muslims ni wanne kulingana na sheria yao ama dini yao?

**Mr. Wilson Sagurai:** Ndio mtu aoane, ndio mtu aoe au mwanamke huyo akubali kuolewa lazima kuna masikilizano. Kwa mfano kama mimi nimepata wanawake hata sita nimesikizana nao kwa nini nisipatiwe marriage certificate?

**Com. Ratanya:** Ungetaka waoe wangapi?

**Mr.Wilson Sagurai:** Sitaki kuwekea mtu kikomo. Maana mila zetu za Kiafrica hazijawekea mwanamume kikomo cha kuoa mabibi.

**Com. Salim:** Asante Bwana Sagurani. Bwana William P. Samson.

**Mr. William Samson:** Kwa jina naitwa William Motika P. C. Samson. Na maoni yangu kwa Katiba hii mpya leo tarehe mbili mwenzi wa tano 2002, ningetoa maoni bila kuandika. Hivi kwamba, hao waliopita wote kwanza nimewaunga mkono. Kitaveta tunasema majimbo kwanza.

Sasa nasemea upande wa watoto shuleni. Kwanza jambo la kwanza shule ndizo zinatuudhi zaidi. Nimetoa ngombe zangu zimekwisha, kwa shauri ya watoto shule. Na serikali ndiyo tajiri ingesomeshea angalau hao wadogo hapa skuli za chini mpaka darasa la nane, halafu lile la juu nijisaidie mwenyewe kuwatetea. Hiyo ni elimu.

Sasa jambo la pili kwa upande wa bunge. Hii Taveta yetu tumekaliwa. Sijui kama huwa ni kwa halali au kwa bernaamij za ndani ndani, miaka thelathini bado ni wageni vipi? Naona kama kuna njia fulani hapa labda haziendi sawa lakini hatujapata Mtaveta. Tunataka Mtaveta sisi sasa. Isitoshe tunadharauliwa tena zaidi ya kiasi. Tunafanywa kutukanwa na njia tukienda kwamba sisi hapa ni wakuja. Sijui huyo aliyekuja na nchi yake ni yupi hapa tunaambiwa mfanya kuja tukawa hata mbunge hatupati.

**Com. Ratanya:** Pendekezo?

**Mr. William Samson:** Pendekezo tunataka mbunge Mtaveta hasa.

**Com. Ratanya**: (*Inaudible*)

**Mr. William Samson:** Ndio katika pendekezo mbunge nafikiri tungesaidiwa sisi wananchi tujitawale wenyewe tufanye mambo yetu kizee, kinjama kama ilivyokawaida tangu zamani zetu. Hapa sisi tulikuwa tuanaenda through njama hatufanyi mambo kiholela holela. Njama hii ndio kama msimamizi wa uchaguzi. Wapendekeze mtu fulani apandishwe yeye awe ndiye atakayepigania kiti.

Jambo la ni pili la tatu hilo nilikuwa nimesema habari ya mashamba. Nafikiri tumekaliwa sana bila kuwa na ….Hata mashamba tungesema kwamba hiyo njama ikalie upande wa mashamba pia. Hata sasa tunaona watu wageni ndio wanaosimamia mashamba yetu kila siku tuna ugomvi, kila siku tunaenda kwa Mungu apoeshe hasira apoeshe ugomvi kwa sababu ya kukaliwa ni watu wa nje. Tukiona wakija hapa hawana vitambi vile wana vitambi, tutakubali vipi?

Nafikiri lingine ni lipi? Kwa upande wa rais. Ningemwambia kama ikiwezekana rais wetu awe na kipindi cha miaka kumi na mitano yaani vipindi vitatu. Mbunge akiwa Mtaveta hata miaka kumi na mitano pia achukue direct.

**Com. Salim:** Umetosheka?

**Mr. William Samson:** Eeh mimi ni hayo tu nasikia kidogo roho imepoa.

**Com. Ratanya:** Kuna swala moja Bwana William. Kwa sasa unaona kwamba parties zinatumika kuchagua wale ambao watagombea. Kuna parties unajua kama KANU, DP, FORD Kenya na hizi zote. Sasa unataka njama ichukue nafasi ya hizi parties? Na tena ningetaka kujua njama hapa ni nini, ni council ya wazee, ama ni nani njama?

**Response:** Council ya wazee

**Com.Ratanya:** Okay sasa unataka wachukue hiyo nafasi ya parties?

**Mr. William Samson:** Kama vile maoni yetu tunatuma kwa njama, njama inapokea inamchagua kiongozi ambaye atatuongoza

**Com. Ratanya:** Na vile vile kugawanya mashamba ama kukubali mgeni aingie lazima apitie kwa njama?

**Mr. William Samson:** Apitie kwa njama

**Com. Ratanya:** Okay.

**Com. Salim:** Na tuseme councillor pia apitie kwa njama au ni mbunge peke yake?

**Mr. William Samson:** Wote.

**Com. Salim:** Asante Bwana Samson kwa maoni yako. Bwana Othiniel Nene.

**Mr. Othiniel Mnene:** Mimi naitwa Othiniel (?) Mnene. Ni Mtaveta asili hapa. Nitaanza na utawala. Utawala wa wabunge, madiwani na ma-chief, na manaibu wao uachiwe wenyeji asili.

**Com. Salim:** Bwana Mnene naona memorandum yako ni ndefu. Kwa hivyo tafadhali utupe points peke yake.

**Mr. Othiniel Mnene:** Points, ndio. Serikali ichukue ma-chief kupitia kwa wazee.

**Com.Salim:** Njama?

**Mr. Othiniel Mnene:** Eeh njama ndio.

Elimu: Mwanafunzi kupitia darasa la nne awe ameshachunguzwa na walimu kujua somo ama masomo yanayomfaa. Yaani kama somo lake ni moja hilo ndilo atakaloendelea nalo peke yake mpaka amalize form 4 nalo. Hiyo itamsadia mwanafunzi kutopoteza wakati wake kuchukua masomo mengine ambao haitamasidia katika maisha yake.

Utawala uwe ni rais, bunge na wazee ishirini wa njama, wazee asilia wakichanganyika na ma-chief na madiwani. Hawa ndio wataachiwa ardhi na Vagrant yani kule kusafirisha watu maana wao ndio wanakaa na wale watu hapo ndani, kwa hivyo wao ndio watajua kwamba yule mbaya ni nani na yule mzuri ni nani. Kama ni jambazi kama ni mtu amekuja tu, wao ndio wanajua kwa hivyo wao ndio wanajua background wawasiliane na serikali wakati wanataka kumsafirisha mtu yeyote kwao.

**Com. Ratanya:** Ulianza kwa kutaja Rais (?).

**Mr. Othiniel Mnene:** Nasema ile chain, Raisi, bunge na wazee ishirini, wakichanganyika na madiwani na ma-chief.
Nafasi za kazi zote za serikali pamoja na nafasi za vyuo vikuu zote zipelekwe bungeni zikagawanyiwe wabunge huko bungeni halafu wao ndio watakuja kusimamia wakati wale watu wanachukuliwa.

Sehemu yote mwananchi anayokaa iwe ni yake bila hata hati yoyote. Title deeds zisichukuliwe kama ni kitu kilichoteremushwa

kutoka mbinguni kwamba haiwezi kuvunjwa. Lazima kama kutakuwa kuna malalamiko kwamba hiyo title deed ni mbaya basi itupwe nje mpaka yale malalamishi yaishe.

Na katika hali ya kuinua maisha ya watu wa hali ya chini Katiba iweke sheria kwamba bunge lipitishe kiwango cha kiasi cha pesa kiasi kadhaa kitakachowekwa katika benki kama Kenya Commercial Bank kwa mikopo ya watu wa hali ya chini kwa masharti nafuu sasa kama ni vipindi vitatu ama vinne bunge lingeweza kusimamisha tenampaka wakati mwingine. Lakiniiwe iko ndani ya Katiba kwamba wakati wote inaweza kuendelea.

**Com. Ratanya:** Itumiwe kwa?

**Mr. Othiniel Mnene:** Kwa kuwapatia mikopo watu wa hali ya chini kwa masharti nafuu kama majuakali wataendelea kidogo na nduka ya makaa, ya masanduku na ya machuma ambayo hayawezi kuingia katika soko la kimataifa.

Kiongozi yoyote wa kisiasa awe sasa ana sifa nzuri kwa manufaa ya wananchi, asiwe mlevi, asiwe msherati, awe ni mcha Mungu.

Kugawanya mamlaka katika serikali kati ya makabila makubwa na makabila madogo kama rais ametokea katika kabila kubwa, basi waziri mkuu atokee kwa kabila dogo na zifuate hivyo.

Mali ya asili kama mawe ya thamani. Leseni ya mali ya asili kama mawe iondolewe kabisa. Maana hii ni kama kusibisha polisi njiani wanachukua yale mawe na huku hawapeleki hata kotini kumstaki yule mtu. Sasa ni kama wanazidi kumpatia yule mtu matatizo.

Kupiga kura: Kila mwananchi anaye piga kura aende akapigie kura kwao kama ameshindwa kwenda kupiga kura kwao. Yaani kama ni Mkamba, kama ni Mkikuyu kama ameshindwa akae hivyo hivyo. Na vile vile kila mtu achukue kitambulisho kwao maana hana huko ndiko anajulikana ukoo wake. Kwa sababu wakati huu kuna watu wanajifundisha lugha na kisha yeye anasema ni kabila fulani kumbe ni mtu wa taifa lingine.

Kuwe na bunge la matajiri ama upper house, halafu ligawanyike mara tatu: Theluthi ya kwanza iwe ni wale wabunge wakurithiwa. Theluthi ya pili iwe ni ya wabunge wa maisha. Na theluthi ya tatu iwe ni ya wabunge wa kukaa pale miaka ishirini na tano.

Mfanyikazi yeyote wa serikali ambaye ashawahi kufanya kazi katika serikali kwa cheo cha juu asiruhusiwe kuingia katika bunge hili.

Raia yote atakayepatikana kumiliki kiwanja cha mtu ama shamba ambalo si lake au labda ametafeli (?) ama amehongana akapata ile hati, afungwe miaka kumi na apigwe faini ya shilingi milion moja.

**Com. Ratanya:** Hiyo ni, fafanua hapo.

**Mr. Othiniel Mnene:** Raia yeyote atakayepatikana na hati ya kumiliki shamba la mtu akadai kama ni lake lakini katika sheria si lake, basi afungwe miaka kumi pamoja na faini ya milion moja maana mtu huyu lazima atakuwa ni tajiri.

Wakati mwingine mtu anaweza kuwa amenyanyasika akakosa mahali pa kushika akipata mbunge anashidwa (?) sasa bunge liwe na utaratibu mzuri kama mwananchi amenyanyasika anaweza kuandika barua yake moja kwa moja kwa bungeni ili wale wabunge wakereketo wanaweza kumsaidia wakati zile nakala zinasambazwa kule bungeni.

**Com. Salim:** Tafadhali maliza maliza.

**Mr. Othiniel Mnene:** Kidogo tu namaliza.

**Com. Salim**: (Inaudible)

**Mr. Othiniel Mnene:** Vyama vya kisiasa viwe vitatu. Ni lazima kuwe na kura ya kuchagua mwenyekiti wa chama kila baada ya miaka miwili. Hiyo iwe ni lazima maana kuna vyama vingine vya kisasa, yule anaye chair kile chama hataki kutoka pale, wala hataki kupingwa pale, anataka abakie pale sasa anasema ni demokrasia ambayo demokrasia ameshindwa pale ndani ya chama chake.

**Com. Salim:** Asante Bwana Mnene. Sasa namuita Bwana Ngurui Tayara.

**Mr. Nguruvi Taraya:** Mimi naitwa Nguruvi Mitiaki Tataya.

**Com. Salim:** Taraya au Tayara? Taraya?

**Mr. Nguruvi Taraya:** Ndio.

**Com. Salim:** Samahani majina yenu mengine yameandikwa vibaya hapa. Endelea basi.

**Mr. Nguruvi Taraya:** Mimi maomi yangu ni kuhusu ardhi. Ardhi hii land inadhulumu wakulima sana. Sababu kesi kidogo tu inamaliza miaka kumi.

**Com. Salim:** Ungeonelea nini?

**Mr. Nguruvi Taraya:** Mimi ningeonelea kwamba wanyang'anywe hicho cheo kipewe kama ni wazee wa njama kama zamani wawe wanaendesha biashara ya ardhi.

**Com. Salim:** Kuendesha biashara au kutatua?

**Mr. Nguruvi Taraya:** Kutatua kesi za ardhi.

**Com. Salim:** Si kuuza na kununua?

**Mr. Nguruvi Taraya:** Ni kutatua. Na siku yoyote ambazo serikali itatafuta mahali pa kutoa mashamba, hao watu ambao watakutwa na hiyo sehemu wawe ndio watagawanyiwa. Sio kwamba patoke watu wengine kama Kisumu wapi wapi, hao wenyeji wagawanyiwe kwanza.

**Com. Salim:** Endelea.

**Mr. Nguruvi Taraya:** Pia Katiba sasa hivi twaomba itusaidie habari ya maji sababu tuna maji ya mfereji lakini inadhari karibu kufikia mafuta ya taa.

**Com. Salim:** Endelea.

**Mr. Nguruvi Taraya:** Pia serikali kuanzia D.O mpaka P.C iendelee hivyo hivyo. Mtu kama sub-chief achaguliwe na wananchi, na chief pia achaguliwe na wananchi. Pia Katiba izuie sababu Chief hanaruhusa kuingiza ardhi mtu mwingine aitumie katika desturi ya kitaveta. Watu walikuwa na uwezo wa kutoa ardhi ni wazee wanaitwa njama

**Com. Salim:** Na sasa wataka?

**Mr. Nguruvi Taraya:** Sasa nataka kwamba hao wazee wa njama warudishiwe uwezo huo. Pia hawa wazee wa mtaa wanafanya kazi kubwa lakini hawalipwi chochote ningeomba pia Katiba iwaangalie.

**Com. Ratanya:** Hao ni hawa tu wazee wa njama ama …?

**Mr. Nguruvi Taraya:** Wazee wa mtaa, kuna wazee wa njama na wazee wa mtaa. Naona nimefikia mwisho.

**Com. Salim:** Asante sana tena, hao wazee wa njama kazi yao unafikiria imechukuliwa na nani? Kwa sababu walikuwa na hiyo kazi zamani. Kazi ya mashamba, kazi ya makesi ya mashamba. Lakini siku hizi hiyo kazi yao inachukuliwa na nani?

**Mr.Nguruvi Tayara:** Serikali kuu ndiyo imewanyima,

**Com. Salim:** Na kuwapa nani?

**Mr. Nguruvi Taraya:** Ikawapa hii land, ambayo inaitwa board, sababu mtu wa board yeye akija anajua jinsi anavyofanya hana uchungu na hapa.

**Com. Salim:** Asante Bwana Taraya ungefika pale ukapige saini kabla hujakaa chini. Asante. Justin Saliando. Na Bwana Justin Suliando maoni yako juu ya (?) dakika tano mawazo, mapendekezo hapa .

**Justin Saliando:** Mimi naitwa Justin Saliando mzaliwa tena Mtaveta. Kwa maoni yangu katika Katiba hii.

Ya kwanza, nikiwa kama Mkenya na Mtaveta ambaye ni wa mwenyeji. Wakati wa uchaguzi wa bunge, ningependekeza katika Katiba achaguliwe mwenyeji wa sehemu ile. Sababu,

**Com. Salim:** Awe mbunge?

**Justin Suliando:** Awe bunge, sababu ni kwamba katika Taveta hii kwanzia saa hii hatuna mbunge ambaye anatuwakilisha kule, ndiposa hatuna maendeleo yoyote katika Taveta. Lakini tukiwa na mbunge anatuwakilisha pale tutasikika kama Mkenya na tutakuwa na maendeleo.

Ya pili. Katika hali ya masomo, katika Katiba hii ningependelea mtoto anapoanza Std 1 afike darasa la nane, kwa ajili ya yule mnyonge ambaye hataweza kumsomesha pia huo mtoto apate kibali pale katika shule. Na pia hiyo itaonyesha yule mzazi kwamba amepata uhuru katika Kenya yake.

**Com. Salim:** Yaani elimu ya bure?

**Justin Suliando:** Elimu ya bure. Ya tatu. Nikiwa Mtaveta katika sehemu hii ambayo nawakilishwa bungeni ina sehemu nyingi za mbuga za wanyama ambayo iko sehemu yetu. Lakini, unakuta kwamba ule ushuru unaotoka katika sehemu ile Taveta Division hatupati. Inapofikia wakati wa kugawanya inakuwa asilimia dogo ndiyo tunapata ambayo haiwezi kuinua sehemu ya Taveta.

**Com. Salim:** Na mapato hayo yapewe nani?

**Justin Suliando:** Yapewe Council. Council ndiyo itagawanya na wakati wanagawanya hiyo mapato kupitia kwa council wawe na wazee wa njama wa sehemu ile ili wajue mapato yanayotokana katika ardhi yao.

Ya nne ardhi. Ardhi katika Kenya hii kila mmoja amezaliwa akiwa na jina la mahali alipozaliwa. Kwa hivyo mzaliwa huyo ana haki ya kutumia ardhi hiyo, kwa ajili ya kuigawanya yeye na jamii iliyoko mahali pale. Aidha, itakuwa labda mtu anaweza kuwa apatwe na shida, auze na akiuza anauzia mtu wa nje. Yule mtu wa nje awe na haki wakati anaponunua, familia ile iwe katikati ya wazee wa njama ni kwa sababu gani anauza? Na yule mtu atakaa pale kulingana na vile alivyogawanyiwa, ili baadaye asije tena akaanza kumnyanyasa yule mtu kupanua ile ardhi.

Ya tano. Kuna jambo hili ambalo mimi nikiwa kama Mtaveta linaniuma ningeliomba kulitia katika Katiba. Kitu Taita Taveta imetuumiza kwa muda mrefu ningeliomba Katiba hii iondoe jina Taita Taveta iweke Taveta ili wawe na uhuru wao wa kujenga sehemu yao bila kugawanyana gharama.

Sita. Ma-P.C, ma-D.O wachaguliwe na serikali sawa, lakini naibu wa chief na chief wachaguliwe na raia maana ndio wanaomtambua vile anavyoweza kuongoza sehemu ile kama mzaliwa wa pale.

Saba. Katiba tungeliomba iondoe vyama vingi iwe na vyama viwili kwa sababu hiyo inaondoa vita, wivu, uchafuzi na pia kukosoana.

Nane. Nikiwa kama Mtaveta katika jamii ya Taveta, Katiba hii kuna mali za asili nyingi ambazo wazee wetu wa zamani kama njama walikuwa wakitandika pale na panaleta mvua vyakula kwa kuwasaidia wananchi wa pale. Katika tandiko hizi zimeingiliwa na wageni wanatandika tofauti na vile ambavyo ilikuwa ikitandikwa zamani na unakuta sehemu nyingi zinaharibika kwa sababu ya kukataa mila ama kuondoa mila. Mila irudi na sehemu zilizotengwa na wazee wa njama wa sehemu ile ziweze kufanya kazi. Kama zimeshachukuliwa, Katiba ya sasa iondoe hicho kipengele na yule mtu aondolewe pale kama kuna gharama atarudishiwa.

Tisa. Ikiwa katika kikundi chochote kama vile jua kali, hivyo ni vikundi ambavyo vimeteuliwa na vimesajiliwa, utakuta yale marupurupu yanayogawanya na wafadhili hayafiki mahali pale kwa mfano hapa Taveta. Pesa nyingi zinaletwa na wafadhili, wakati zinapogawanywa hazigawanywi katika lile baraza, zinagawanywa katika mabaraza mengine na unakuta inatangazwa kwamba pesa zimetolewa milion kadhaa katika Taveta aidha jua kali ama kina mama lakini division kama ya Taveta hakuna kitu huwa kinafika. Ingestahili wakati zinagawanywa namna ile igawanywe kila division kama ni council waende wakae walete hizo

pesa mahali ambapo zinahitajika katika kikundi kilichosajiliwa kama social hall kama hio.

**Com. Salim:** Uko karibu kumaliza?

**Justin Suliando:** Karibu kumaliza, bado moja.Ya mwisho ni katika hali ya mabarabara, biashara aina yoyote ile, kama ni jambo limetokea la kuweza kutengeza sehemu kama hizo. Katiba hii pesa zinapotengwa na serikali, zipelekwe katika zile division ambazo zinazohusika na hayo mabarabara kama ni tender, wao wenyewe watachagua ni nani atakayefanya lile tender ili ile kazi iweze kufanyika. Sababu ni hivi, kwa sasa hivi kama Taveta kushatolewa tender nyingi lakini hakuna chochote kinachofanyika. Unakuta tu pesa zinaliwa na wajanja kwa sababu hatuna mwakilishi yeyote anayesimamia jambo hili. Kwa hayo machache kwa amani…

**Com. Salim:** Biashara unasema nini? Fafanua.

**Justin Suliando:** Biashara kuna pesa hutolewa saa ingine za kuisaidia sehemu fulani, biashara dogo dogo lakini unakuta biashara ndogo ndogo zile hazifikii wananchi wengine wa kawaida walio wachache kama Taveta.

Ya mwisho. Ni katika shule zetu na mahospitali, wale ambao husimamia sana katika mahabara ya aina yoyote ile unakuta kama hospitali kwa mfano, madawa yanakuja na yanapokuja yanasimamiwa na wale watu ambao wamechaguliwa wakiwa nje ya Taveta. Sasa yale madawa badala ya yahakikishiwe na wenyeji wa sehemu ile kwamba madawa yamefika na yanatosheleza muda huu mpaka muda fulani, unakuta yakishaingia pale yanafungiwa ndani wale wafanyi kazi ndio wanagawanya gawanya huko ndani, kesho kufika hakuna dawa zimeisha na tumesikia zilikuja. Kwa hivyo ingestahili kuwe na kamati ya sehemu ile upande wa health kutoka nje aidha council ama wazee hawa wa njama, hawa maana mali ni yao wahakikishe kwamba haya madawa yanafanya kazi kwa njia inayostahili.

Ya mwisho. Pawe pia mfanyikazi katika sehemu ile ambaye kama ma-doctor, nini (?) lakini pawe mwakilishi wa sehemu kama hii wawe wakiwa wanafanya kazi pale ndani. Maana atapiga picha aone ubaya uko wapi akiwa kama Mtaveta hapataharibika kitu. Asante.

**Com. Salim:** Nina swali, hapo umesema mashule na hospitali, sasa unasema je juu ya shule kwa sababu hospitali umesema mambo ya dawa?

**Justin Suliando:** Ndio tunasimamia shule zetu sisi kwa mipango ya majengo na vifaa vingine vingine. Lakini utakuta kuna sehemu zingine kama bursaries zinaweza kuwa zinatoka, lakini utakuta ile bursary inayotoka sasa itaenda kwa yule mtu ambaye pia yeye ni mzito ana uwezo na yule mdogo alioko hapa asipatiwe bursary mtoto wake akaendelea. Ingeliwezekana hiyo bursary ikitoka pawe na uchunguzi ni wapi ni nani aliye chini zaidi ameshindwa mtoto wake huenda ikawa ni mtoto wa kilema

amezaa akiwa kilema lakini hawezi kumsomesha yule mtoto. Hiyo pesa iwakikishe kwamba kamati ya hiyo bursary imetoka katika sehemu ile ya Taveta na inawakilisha vizuri na huyo mtoto anapita hiyo ni shule.

**Com. Salim:** Na tena hao wazee wa njama ni wazee wa akina mama na akina baba?

**Justin Suliando:** Hapo siwezi kata uwongo ni kwamba wakiwa pamoja na ma-councillors wamechanganyika. Lakini wakiwa ni wa njama peke yao, hiyo njama huingia wanaume peke yake.

**Com. Salim:** Swala hili la majina kubadilishwa umependekeza kwamba Taita Taveta iwe ni Taveta peke yake, na Taita ifanywe nini, iwe ni separate?

**Justin Suliando:** Hapana ikiwezekana, kama haiwezi kuwa Taita Taveta iwe separate iwe Taveta, basi ..

**Com. Salim:** Yani district mbili?

**Justin Suliando:** Isiwe district mbili, basi, (?) tuwe Taveta Taita, No,

**(Noisy interjection)**

**Com. Salim:** Wasema iwe Taveta District?

**Justin Suliando:** Taveta District na Taita District

**(Interjections inaudible)**

**Com. Salim:** Tafadhalini kidogo tutulie tupate kusikiza maoni zao

**Com. Ratanya:** Tulianza kwa kusema mtu akitoa maoni yake ni yake.

**Com. Salim:** Na sasa tutamuita mama Sophie Jumamosi Mathew.

**Sophie Jumamosi:** Mimi ni Sophie Jumamosi Samson. Mimi maoni yangu ni juu ya watoto wetu. Watoto wangu kama mimi ninavyoona kwamba waweza kubashiri (?).

**Com. Salim:** Inua sauti kidogo mtu kule nyuma hawezi kusikia.

**Sophie Jumamosi:** Haya, nasema hivi. Mimi ninasema juu ya watoto.Watoto wetu kama watoto wangu mimi wanakwenda kuzaa bila ya mume, na watoto wao tena wanaenda kuzaa bila mume.Tunapata taabu kubwa hapa nyumbani. Hapa Mahoho Taveta yetu hii, sijui huko kwingine ni watoto wengi sana hawaendi skuli. Kwa mfano mtoto wangu ameenda amezaa mtoto na hana mume mtoto wake pia naye azae bila ya mume, ni matatizo makubwa watoto wetu hawawezi kuendelea na skuli.

**Com. Salim:** Ungependelea nini mama?

**Sophie Jumamosi:** Ningependelea hawa watu wa hawa watoto tafadhali wapate mtu mwanamke tena wa umri ambae badala ya hao sijui kama watu wa mission hawa wanaoangalia watoto hao watoto hawajaangaliwa ya kutosha wanataka kama mama mzee si mzee kama mimi …

**Com. Salim:** Na angalie nani?

**Sophie Jumamosi:** Aangalie wale watoto, watapelekwa kotini watashitakiwa lakini huku anaendelea kuzaa. Kwa hivyo naomba serikali iwaingilie sana hawa watoto wetu ili wawe na namna. Hata ningeomba kama wangejengewa mahali ili wapate mafundisho wasizidi kuzaana.Wanatupa taabu kubwa sana na wanabaki bila ya kusoma kwa hivyo mtoto kama amezaa akakimbia akawacha mtoto kwa mfano na si kwa mjani wanafanya, anakimbia ananiachia kama mimi, nitaweza kulea? Siwezi, kwa hivyo tafadhali sana sana ingilieni hilo jambo muweke kina mama, watu wazima kama huyu sasa mfano wa miaka kama hawa wana ambao bado wana nguvu ili wawaangalie wale watoto ambao wamezalia manyumbani. Sasa kama ni kazi serikali kama ni ya kufagia barabara kama ni ya kufanya nini, wawapatie hiyo waweze kulea watoto wao kuliko kukaa bila ya skuli. Hata wakifika angaa 8 watoe ule ujinga maana wengi wetu si matajiri ni maskini, sasa huwezi kujilea wewe mwenyewe halafu na mtoto wa mtoto hilo jambo limeleta matatizo sana Taveta.

Jambo la pili nimesikia limezungumzwa hii ya Title deeds.title deeds, hii (?) mwaka wa sitini na tatu na mpaka leo hii hatujui Title deed ni kitu gani.Sijui mwisho itakuwa je sasa. Sijui sasa sijui urithi wetu namna gani takuwa. Nasema mashamba mengine hii ya scheme, tumepata mwaka yani yani sitini na tatu tume-shift. Lakini sasa leo hii na unasikia wengine moja wao ambao ni hodari walienda Nairobi au hodari wa pesa washapata. sasa ikiwa ni hivyo itakuwaje? Kwa nini na sisi tusipate uridhi wetu wa kupata title deed kwenye mashamba yetu. Mimi naona sina mengine. Asanteni sana.

**Com. Salim:** Mama Sophie hapa amezungumza juu ya mambo ambayo ni muhimu sana na ninaweza kusema kwamba mimi kati ya wenzangu sijasikia pendekezo kama hili na kwamba kina mama wadogo wao wenyewe ni wadogo kisha wakapata na watoto wakawa hawawezi kujitazama wenyewe au kuwatazama watoto wao. napendekeza kwamba kuwe na vituo maalum vya hawa watoto ambao hawajaolewa na watoto wao na kazi wafundishe ili kuendesha maisha yao. Asante mama Sophie, na tukiendelea mbele tutamuita Bwana Jimmy Mwanzia.

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Kwa majina mimi naitwa Jimmy Mwanzia, natoka Kimala sub-location.

**Com. Salim:** Bwana Mwanzia una memorandum, una maoni ya kuandika?

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Eeh, ya group lakini

**Com. Salim: (**Inaudible)

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Lakini yote ni point.

**Com. Salim:** Twenty pages

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Sio twenty.

**Com. Salim:** Sawa tutachukua memorandum, tutaisoma kwa makini kule, lakini kwa sasa wewe ili kuwajulisha hawa wenzako unazungumzia nini, tutakupa dakika tatu kutupa yaliyomo.

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Kisha mtabaki na hii.

**Com. Salim:** Yaah. Kisha uta (?) memorandum (?).

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Sawa.Mimi naanza na ardhi. Adhi ni kitu muhimu kwa jamii..,

**Com. Salim:** Tafadhali Bwana Mwanzia usitusomee maanake utachukua muda mrefu memorandum yako (?) Tupe points. Sema ardhi unataka tufanye nini, kisha uende pointi ya pili tufanye kitu gani. Elimu tufanye kitu gani. Tafadhali, point by point.

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Sawa. Ardhi, jamii ndio inayojua mipaka yao. Ardhi ina umuhimu wa kitamaduni

**Com. Salim:** Ni yako mwenyewe hii memorandum?

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Ya group.

**Com. Salim:** Lakini bila shaka ukiwa ni mmoja wao unafahamu yaliyomo bila kusoma sio? Kwa mfano ardhi bila (?) wapendekeza kitu gani?

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Mambo ya ardhi, imilikiwe na jamii.

**Com. Salim:** Si mtu binafsi?

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Si mtu binafsi.

**Com. Salim:** Point ya pili.

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Tamaduni zetu zilindwe na serikali.

**Com. Salim:** .Zilindwe na serikali, kama?

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Kama njama.Mazingara yetu pia yanatakikana yaangaliwe sana mambo ya uchomaji makaa, kukata miti ovyo yalindwe na serikali.

**Com.Salim:** Na kukata miti na nini,

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Eeh.

**Com.Salim:** Sema habari ya makaa (?).

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Uchomaji wa makaa. Wasichome makaa,wasikate miti wakachoma makaa.

**Com. Salim:** Point ya nne.

**Mr. Jimmy Mwanzia:**Tunapochagua mbunge kila mwezi awe akirudishwa nyumbani kuchukua maoni ya watu na shida za watu.

**Com. Salim:** Ya tano.

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Elimu, watoto wa msingi wanatakikana wasome bure
Sheria mahakamani. Si mimi namaliza. Wacha nisome hii.

**Com. Salim:** Page ngapi hizo, one page?

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Eeh, hii.

**Com. Salim:** Kuhusu mahakama au (?).

**Mr. Jimmy Mwanzia:** Yaah, mahakama. Mahakama ziruhusiwe kutoa kifungo kikubwa zaidi kulingana na kosa la mshitakiwa bila kuingiliwa na serikali ili;

(a) uporaji wa mali ya jamii aliye pora mali ya jamii aadhibiwe vilivyo.

(b) ubakaji usiwe katika jamii.

(c) mwalimu awekapo mtoto wa shule mimba afungwe miaka isiyopungua ishirini

(d) mwanafunzi anapompa mimba mwanafunzi mwenzake afungwe kifungu cha miaka kumi na mbili.

(e) mzazi akibaka mtoto afungwe miaka ishirini.

(f) anayeambukiza ukimwi mwingine kwa makusudi, afungwe miaka ishirini hadi thelathini.

(g) aliyepora mali ya jamii kwa maslahi yake mwenyewe afungwe miaka thelathini na apokonywe mali zake zote

(h) askari atayepatikana na kosa la wizi wa kutumia nguvu afungwe maisha kwani ndiye macho ya jamii.

(i) sheria ya Vagrancy iwepo ili kuzuia uhamiaji ovyo, wizi na u-squatter katika jamii nyingine.

**Com. Salim:** Thank you very much Bwana Jimmy Mwanzia kwa maoni yako tafadhali memorandum utaandikisha na kuiweka hapa. Ronald Sagurani.

**Mr. Ronald Sagurani:** Mimi ni Ronald Sagurani na leo tarehe mbili mbele ya tume hii nina maoni kuhusu marekebisho ya Katiba.

Ninaanza na swala la bunge. Maoni yangu ni kwamba bunge lile la Kenya, kila kabila iwe na haki ya kuwakilishwa katika bunge lile. Licha ya idadi ya watu wake. Pia mbunge atakayechaguliwa ili awaakilishe watu hao katika bunge lile, ingekuwa ni vyema awe ni mtu anayefahamu vizuri mila na desturi na tabia za kabila lile, licha ya kuwa anaweza kuongea lugha ile. Mtu huyo anayetaka kuchaguliwa awakilishe watu wake katika bunge lile ni lazima pia apate ridhaa kutoka katika juko la wazee ambao wametajwa sana wanaitwa wazee wa njama. Wazee wale lengo lake ni kuhakikisha kwamba mtu yule anakidhi maadili ya jamii ile ili aweze kuwawakilisha vyema. Jukumu la wale wazee wa njama ni kuhakikisha kwamba mtu huyu anakidhi maadili ya kabila lile.

Kuhusu utaratibu wa uchaguzi wazee hawa hawa wa njama wao pia, tume ya uchaguzi iwatambue kabla ya mtu yeyote anayetaka kupigania kiti cha ubunge cha mahali pale, kabla hajakuwa cleared na tume ya uchaguzi kuwe na consent kutoka katika wale wazee wa njama kwamba huyo mtu ndiye anayestahili kuwakilisha watu hao katika bunge. Awe amepitia katika wazee wale. Kwa hivyo tume ya uchaguzi iwatambue wazee hawa kabla ya kuidhinisha mtu agombanie kiti cha ubunge.

Swala lingine ni kuhusu serikali. Naona ni vyema kungekuwa serikali ambapo, rais atakuwa kiongozi, na watagawanya mamlaka na mtu anayeitwa waziri mkuu. Kuwe na Waziri Mkuu ambaye watajaribu kugawanya hizo mamlaka namna watatawala serikali ile. Halafu basi, iwapo Rais amepatikana labda kutoka kabila kubwa, huyu waziri mkuu awe anatoka katika makabila yale madogo.

Ardhi: Ardhi zote zile ambazo zilizopatikana nyakati za mkoloni, na sasa hivi bado watu wanaozimiliki wana ile kitu inaitwa lease. Nasema ardhi zote zile zilizopatikana wakati wa mkoloni na sasa bado ziko chini ya lease, ni vyema serikali ingezichunguza ili wenyeji wa mahali pale ambao ardhi hiyo ilipatikana bila ridhaa yao waweze kurudishiwa ardhi yao. Kwa sababu wakati wakoloni wakichukua ardhi hiyo hawakutafuta ridhaa kutoka kwa wenyeji walijichukulia kwa sababu walikuwa na uwezo huo.

Vyeti vya kumiliki ardhi. Wakati vyeti vya kumiliki ardhi vinatolewa hii kitu inaitwa Title deed. Ni vyema kabla ya commissioner wa ardhi hajaidhinisha hiyo title deed lazima ange-lias na wazee wa maeneo yale. Hapa Taveta wanajulikana sana kama wazee wa njama. Wao ndio watajua hakika ya mtu huyo kupewa cheti cha kumiliki ardhi hiyo. Isiwe tu mtu anaenda Nairobi kule kwa sababu commissioner wa ardhi ni mjomba wake anajua Nairobi vizuri, kuliko sisi sote wa mashambani hapa anakuja na karatasi anasema nimepewa nimepewa, sasa nadhani ni vizuri wazee wa pale maeneo hayo waweze kushirikishwa katika jambo hilo.

Kuhusu fidia za mali zinazoharibiwa, labda na wanyama hawa wanaomilikiwa na shirika hili la KWS. Nasema kwamba ni vizuri mnyama akiharibu ama akiua mtu kusiwe na majadiliano bwana. Mali ya yule mtu iliyoharibiwa ilipwe moja kwa koja kulingana na uharibifu, si mambo ya serikali iseme tunaona tukupe kiwango hiki, aaha! Ilipwe kulingana na uharibifu uliotendeka. Si swala la mjadala hilo.

Naongezea pia katika jambo lingine sijui nitaliweka katika sehemu gani, lakini nilikuwa nataka kusema kwamba, hawa wanyama wa kufuga ambao hawaliwi kama vile mbwa ijapokuwa nasikia sehemu zingine watu wanakula mbwa lakini si sana. Sasa mtu anapotaka kufuga mbwa kwa sababu maradhi ya kichaa cha mbwa yameongezeka sana, na ni gharama sana kutibu mtu anayeng'atwa na mbwa, kungekuwa na utaratibu wa sheria maalumu ya mtu anayetaka kufuga mbwa ziwekwe ili, mtu yule sheria hizo zimbane ili aweze kumtunza mbwa yule hata ikitokea atang'ata mtu hakuna hatari ya kumuambukiza maradhi ya kichaa ambayo gharama zake si watu wengi wanaweza ku-afford. Kuwe na sheria ile itakayoweza kumbana mtu anayetaka kufuga mbwa ili apate maagizo fulani ambayo itaweza kupunguza uambukizaji wa viini vya ugojwa huu.

Pia nasema kuhusu serikali tunatayotaka iwepo. Maoni yangu ni kwamba tungetaka serikali ya majimbo. Majimbo tuna amini yatasaidia kulinda haki ya makabila madogo madogo na rasilimali zao na haki zao za kisiasa na haki nyingine yoyote. Majimbo yatakuwa na uwezo huo wa kulinda makabila hayo. Kwa hivyo ningependekeza sana serikali ya majimbo.

Halafu jambo lingine. Kuwe na utaratibu kuhusu hawa wenzetu maaskari. Maaskari wanafanya kazi nzuri sana tunawategemea sana, lakini mara nyingine wanapitisha mipaka. Unaweza kuta askari anapokea hongo hadharani. Askari anaweza akubadilishie kosa ambalo hukutenda ama afanye tendo ambalo wananchi wanaona ni kosa hadharani lakini mwananchi hana nguvu yakuweza kukabiliana naye na anatenda hili kosa wazi wazi mbele ya wananchi kama ishirini hivi. Kuwe na utaratibu fulani ambapo mwananchi naye atawezeshwa ikiwa watakuwa na ushahidi wa kutosha wameona polisi ama askari mwingine amefanya tendo la wazi la jinai, kuwe na namna fulani ya utaratibu ambao mwananchi anaweza akamshika mtu yule na kumfikia kwenye (?) na dola ikamshugulikia kama mhalifu wa kawaida.

Vagrant Act.Tunasema ni vyema hii act irudishwe ama kama ilikuwa haiko iwepo katika maeneo yale ambayo yanahitaji sheria hii. Yale maeneo yanaona kwamba hiyo itawalinda itawasaidia mambo yao, tungependa hiyo irudishwe kwa hao.Kwa hivyo hapa Taveta tunasema hiyo irudishwe tunaitaka, Vagrant Act.

Kuhusu elimu. Nataka kusema tu kwamba elimu ya msingi darasa la kwanza mpaka la nane hiyo kwa kiwango fulani mzazi agharamie. Lakini ili kuwapa watoto elimu itakayo lingana na technologia ya kisasa, secondary mpaka chuo kikuu, serikali igharamie hiyo. Kwasababu watoto wengi wanakwamishwa na elimu ya secondary ambapo pale ndipo elimu inayohitajika sana ili kukidhi hali ya technologia katika dunia ya sasa.

Kuhusu youth polytechnics, tungependa serikali isimamie moja kwa moja vyuo hivi vya kiufundi vya vijana. Moja kwa moja isijaribu kubebesha mzigo huo mtu mwingine. Serikali kwa sababu twataka watoto tulionao wawe na ujuzi na ujuzi huo utawasaidia kupunguza umaskini na kupata ajira. Sasa serikali ijihusishe moja kwa moja na kusimamia hizi youth polytechnic.

**Com. Salim:** Time Bwana Sagurani.

**Mr. Ronald Sagurani:** Asante sana sijui nina dakika ngapi hapo nitaenda mbio mbio.

**Com. Salim: (**Inaudible)

**Mr. Ronald Sagurani:** Moja tu. Thank you. Sasa kuhusu matibabu, matibabu yawe free.

Na la mwisho nataka kusema kwamba hawa maofisa wanaochaguliwa katika mabaraza maofisa wa ma-clerks na wale wengine, mimi napendekeza kwamba wangekuwa wanachaguliwa na wale ma-councillor ambao sisi tumewapeleka pale wa

tuwakilishe, wao ndio wawe wanawachagua ma-clerks pale ndani ya ofisi.

**Com.Salim:** Town clerks?

**Mr. Ronald Sagurani:** Exactly. Ndoa, mtu yeyote akifunga ndoa yake aruhusiwe kupata cheti. Wamefungia chini ya mti wamefungia wapi, bora tu wazee walikuwa pale wakatambua wameridhiana na wale wazazi basi cheti apewe mtu huyo.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana Ronald Sagurani kwa maoni yako sijui mwenzangu ataka kukuliza lolote. Malcom Mukawirondo. Yuko? Mukawilondo, yuko? Ame-register lakini ameondoka. Okay Bwana James Ngisangi.

**Mr. James Ngisiane:** Kwa majina mimi ni James Ngisiane Taabu.
Mimi kwa ufupi nazungumzia juu ya uongozi na bunge.Kwa maoni yangu Mungu aliumba makabila arobaini na mawili hapa Kenya. Na makabila hayo akayaambia wewe utakaa hapa, utazungumza lugha hii, na tamaduni zako zitakuwa hizi. Lakini sasa kwa ujanja uliofanyika mwaka sitini na tatu, wajanja fulani wakabadilisha Katiba wakasema kwamba Mkenya ni Mkenya popote alipo anaweza kuwa kiongozi anaweza kutawala, ambapo hayo ni makosa kabisa.

**Com. Salim:** Pendekezo lako.

**Mr. James Ngisiane:** Pendekezo langu katika ubunge hao ma-councillor. Ni watu wale wale wa kabila lile na sehemu ile wanaongea lugha ile baada ya kuidhinisha na wazee wa njama. Mtu mwingine kabila lingine alioko kwa mfano hapa Taveta lazima anajua anatoka sehemu gani ya wakilishi bungeni huko kwao, anaposikia kiu ya uongozi, aende huko huko. Na ningeliomba tume hiyo Katiba iliyosema Mkenya ni Mkenya popote alipo anaweza kukaa, anaweza kumiliki, anaweza kutafuta uongozi hiyo isirekebishwe. Hiyo ni ya kuondolewa kabisa. Kila mtu atafute uongozi kwao nyumbani. Nimemaliza mimi.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana Ngisiane. Bwana John Ngoyanae. John Ngoyanae.Hayuko? Juma Muslai. Karibu.

**Mr. Juma Muslai:** Asanteni sana kamati ya Wanakatiba, tunawakaribisha Taveta muchukue maoni ya wananchi. Natoa salamu zangu kwenu na kwa wananchi wote waliofika hapa kwa wingi kujaribu kurekebisha Katiba hii.

Nikianza na utawala. Sisi tunajua kwamba utawala unaofaa katika mkoa wa Pwani ni serikali ya majimbo, kuliko kutawaliwa na serikali ilioko mbali. Lakini tukijitawala wenyewe katika jimbo letu wenyewe au katika kila jimbo katika Kenya, itakuwa very much effective kutawala na utawala utakuwa rahisi, na wananchi hawatapata taabu kwa maana watakuwa karibu na watawala kuliko hivi ilivyo sasa.

Pili. Katika jimbo tungependa mtawala mkubwa yaani yule ataangalia hali ya serikali ya majimbo awe na cheo cha governor

ambaye atajibu kutoka kwa Waziri mkuu katika serikali kuu sasa. Na waziri mkuu atajibu kutoka kwa rais, na raisi atajibu kutoka kwa representative house ambapo katika Pwani itakuwa ni senate house. Na tukiwa na bunge letu wenyewe kama Senate, Government itakuwa active zaidi kututendea mema au kutugawanyia haki na mali ya ile jimbo na tutaweza kumiliki mali zetu wenyewe kama wana majimbo.

Nikija katika utawala mdogo, maoni yangu binafsi ningependelea kwamba nikikumbuka zaidi kama miaka kumi na tano au ishirini na tano iliyopita tulikuwa tukichagua ma-chief wenyewe na walikuwa wakifanya kazi nzuri kuliko ya sasa wanachaguliwa na serikali. Tungetaka ma-chief wachaguliwe na raia.

**Com. Salim:** Na sub-chief?

**Mr. Juma Muslai:** Chief na sub-chief, chief na mdogo wake chief, wachaguliwe na raia ndipo wataweza kufanya kazi vizuri. Lakini sasa katika serikali akitaka kufanya hivi katika serikali ya sasa,cbm,/ na Katiba ya sasa hatakuwa na sauti wala hatakuwa na nguvu kwa sababu nyuma kuna mtu anamuangalia kwa macho, fanya hivi, atakuwa yeye anaelezwa la kufanya si lile wananchi wanalotaka wafanyiwe. Na katika serikali za kienyeji na za mitaa kuanzia Chief, Councillor hata mzee wa mtaa awe mzaliwa halisi wa pale pahali. Kwa maana ninavyosema ni kwamba ikiwa yeye ni mzaliwa anajua shida zangu zaidi kuliko wewe mgeni uliokuja unikalie nikitaka ukweli wangu na haki yangu huwezi kunipa.

Nikirudia upande wa mali ya asili, nafikiri kila mtu anelewa mali ya asili ni kitu gani hasa mbuga zetu za wanyama, national parks na game reserves. Tumefanyiwa kwamba hili mbuga letu la wanyama ni national, ni cake ya Kenya nzima kwanini tusiambiwe kwamba hii ni game reserve na sisi tupate faida ya wale wanyama.

Tena inaonekana kwamba serikali inapendelea sana wanyama kuliko yule mwanadamu anamtendea kazi. Kwa mfano, ndovu anakuja anaingia mpaka mashambani yale tunaoata sisi wakaji wa hapa kama chakula chetu, riziki yetu,maisha yetu, wanaharibu. Hakuna mtu aliyelipwa hata mmoja. Lakini leo wewe umemuua mnyama na unapatikana, unafungwa miaka ishirini na unalipa basi tunataka sheria hiyo igeuzwe, serikali ikielezwa na D.O wake au Game wake kwamba mali ya Mtaveta au ya Mkenya wote imeharibiwa wawe tayari kufanya compensation. Wawe tayari kulipa yule mtu aliyeuliwa. Kwa maana serikali imeleta game reserve mpaka ndani ya vijiji, na eneo la wanyama ni kubwa zaidi kuliko lile eneo mwanadamu analoishi. Ningeomba wanapokwenda kujadili, okay si mazuri sana maoni yangu lakini wakadirie kwa nini mnyama anakuwa very much important kuliko mwanadamu? Si mwanadamu Mtaveta, mwanadamu yeyote wa Kenya.

Tunapendelea sana wageni kuja Kenya na vitongoji vingine vyote. Lakini unapotoka kwenu ujue unakuja Taveta wewe kama mwana biashara au unakuja kutafuta kazi uandikwe na serikali, au umeletwa na serikali ufanye kazi hapa ukija stop! Wacha ardhi ya Mtaveta anvyoitenda aitende vile anavyofikiria mwenyewe. Kama ni biashara njoo ufanye biashara, wacha siasa, wacha kupigania u-councillor, wacha kupigania ubunge, hata wengine ni wazee wa mtaa (?) wazee wa mtaa

kwani kumekosekana Mtaveta? Kwani kumekosekana mwenyeji wa nchi hii ya kuangalia ardhi yake, na maadili yake? Wako. Tuliambiwa katika bunge kwamba kuna kifungu kinacholinda kabila dogo lakini hakijatendeka hapa Kenya hapa Taveta, Elmolo kule si ni kwao wakati huo mulisoma kulikua 99 people na walikuwa na sheria zao za kuwalinda. Ukifika kule unaambiwa umekuja biashara, ni biashara. Umekuja U-councillor, kwenda kwenu, mjumge kwenda kwenu. Tu wachache lakini tunao watu wetu ambao anajua shida yangu na ya mwengine. Kwani hapa Taveta isiwe hivyo? Unakuwa transported from up there unaletwa hapa unaambiwa pigania huku. Kwani isiwe na haki ya mtu mchache, kabila dogo lisilojua mbele wala nyuma tumezingirwa na maadui, basi tungeomba sheria hizo zitolewe za mkoloni.

**Com. Salim:** Tafadhali time is up.

**Mr. Juma Muslai:** Na mimi nilikuwa nikijitafadharisha niondoke. Nashukuru sana.

**Com. Salim:** Bwana Elijah Wazaa.

**Mr. Elijah Wazaa:** Jina langu mimi ni Elija Wazao, mimi ni Mtaveta. Katika siku hii ya pili mwezi wa tano, 2002,

**Com. Salim:** Tafadhalini tusikize maoni.

**Mr. Elijah Wazaa:** Kwanza pendekezo langu ambalo ningeomba katika Katiba ya Kenya ni lugha ya taifa ambayo lugha ya taifa ingekuwa ni Kiswahili pote serikalini hadi kotini wala si kama vile kotini ukienda lugha inayotumika ni Kingereza katika nchi yetu hii ya Kenya.

Jambo la pili, Katiba ingeangalia sana hali ya wafungwa. Jela ni mahali pa kurekebisha tabia na wala si mahali pa kutesa watu.Tena kwa ajili ya chakula wanavyopewa wafungwa wapewe vyakula vinavyostahili afya ya binadamu.

Jambo la tatu, serikali isimamie hali ya matabibu mahospitalini. Kwani hii ni ahadi ya serikali iliyo ahidi serikali ya Kenya kwamba ingelisimamia hali ya utabibu kwa sababu wengi Wakenya hawajiwezi kwa gharama zinazotolewa hospitalini.

**Com. Salim:** Ungependelea?

**Mr. Elijah Wazaa:** Ningependelea serikali itoe matabibu yale bure kwa wananchi wasiojiweza wote.

La nne. Ningelipendelea Katiba ya Kenya isimamie watumishi wote wanapostaafu kutoka kazini. Kwa sababu maisha yao yamemalizikia kazini na wanapoachwa kiholela holela na maisha yanazidi kuendelea kupanda watu hao maisha yao huwa mabaya zaidi.

La tano. Ningelipendelea Katiba ya Kenya imlinde sana Rais wa Kenya. Si kila mtu anayeinuka na kumnyanyasa Rais, kwa sababu Rais amechaguliwa ni taifa la wananchi wa Kenya na anaponyanyaswa ni kusema taifa linanyanyaswa. Haheshimiwi, na yeyote atakaye mnyanyasa Raisi achukuliwe hatua ya kisheria.

La sita, Katiba ya Kenya isimruhusu mtu yeyote ambaye ametembea katika nchi ya mwingine kupata kibali cha kusimamia either siasa, utawala wa aina yeyote, maana huyu ni mtembeaji wala katika mazingara yoyote kutoka ya bunge, councillor Katiba ipitishe azimio kikamilifu wala isitoe kibali kwa mtu kama huyo.

La saba Katiba isimamie ardhi ya Kenya. Mkoloni hana haki ya ardhi ya Kenya kwasababu, Uraya hamna Mwafrika yeyote aliye na kipande chochote cha ardhi itakuwaje Kenya mkoloni aseme ana ardhi.

La nane, Katiba isimamie jambo la omba omba serikalini. Katiba isimamie jambo la omba omba nchi za ngambo. Ni aibu katika nchi hii yetu ya Kenya kurudi kuomba omba kwa wakoloni. Katika hali hiyo ya kuomba omba misaada ng'ambo, imeletea nchi hii shida na umaskini mkubwa sana. Kwa hivyo Kenya ijifundishe kujitegemea yenyewe.

Tisa. ningeliomba Katiba ya Kenya iache uchumi huru kwa kila mwananchi na wala si kuwanyanyasa wasiojiweza.

Kumi, Katiba isimamie vyama vya siasa. Kwa upande wangu ningelipendelea Kenya iwe na vyama viwili tu. Hii ni kwasababu ya usalama wa wananchi wanaoishi Kenya.Haya ndio maoni yangu machache.

**Com. Salim:** Asante Bwana Elijah Wazaa, sasa ni Charles Sowene.

**Mr Charles Sowene:** Mimi ni Charles N Sowene. Nikiwa hapa leo tarehe mbili mwezi wa tano tukipapasa papasa habari ya Katiba.

Neno langu la kwanza ni kusema ma-chief na manaibu wao wapigiwe kura. Sababu hasa inamaanisha niseme hivyo, ma-chief walikuwa wakichaguliwa zamani na wenyeji wao. ikaenda kuwa mambo yamegeuka ya kizungu wafanye interview. Interview hizo zimekula wananchi kweli kweli hata ukiangalia utakuta hakuna chief aliye na tumbo dogo, yote imejaa. Na hata kama utathubutu kumweleza lolote chief aweza akakuambia kwamba mimi nilifanya interview, sikuchaguliwa na mtu yeyote kwa hivyo sijali. Utafanya kazi yangu kama nipendavyo.

Nikitoka hapo nitaingia kwa upande wa wabunge na ma-councillor. Niseme ya kwamba wabunge wana haki ya kuwa ni wenyeji wa nchi yao na wachaguliwe na wenyeji wao. Isiwe kwamba ni mtu yeyote kutoka huko aje apigiwe kura katika nchi ya wengine. Nikisema hivyo namaanisha ya kwamba mimi nikiwa mdogo mpaka umri wangu huu Wataita ni wengi sana

Taveta, na Wakamba ni wengi sana Taveta, Wapare ni wengi sana Taveta. Na sijasikia miaka hiyo ingine, sijasikia upuzi wa kuzozana makabila haya ilikuwa hakuna, ilikuwa amani tupu na upendo ulikuwa umejaa. Lakini sasa nikiangalia naona kwamba wamekuwa wengi zaidi nao sasa wanataka watawale Taveta ati sasa nao ni wenyeji kwa Taveta kuliko Wataveta.Hata watu wananyanga'nywa vitambulisho wale Wataveta. Mimi nimewahi kunyang'anywa kitambulisho, mimi Mtaveta mzaliwa wa hapa na babangu, mimi nilinyang'anywa kitambulisho na polisi na alikwenda akajua ya kwamba nitampitia vibaya alikimbiza kitambulisho changu mbio kabisa akaniletee na kunisihi tafadhali. Alinisihi tafadhali nisamehe maana walikuwa ni wanyanyasaji wa Wataveta. Inamaanisha ya kwamba wao sasa wana nguvu kwasababu hata huku makwao walikotoka ni wengi zaidi ya Wataveta. Wataita, Wakamba, Wapare ni wengi. Na hata sasa wameungana imekuwa kitu hicho, kimoja.

**Com.Salim:** Pendekezo lako ni nini. Sasa ungesema unataka nini.

**Mr. Charles Sowene:** Pendekezo langu nimekwishaanza kusema ya kwamba mbunge au councillor apiganie kiti nchini kwao na achaguliwe na wenyeji wake, hapana mgeni kuja. Hivyo nikisema kwamba Wataita walikuwa wengi hapa na Wataveta na kulikuwa na heshima, sasa hakuna heshima tena. Wataita wanatukana Wataveta bwana ,Wakamba wanatukana Wataveta, Wabare wanatukana Wataveta. Na mapenzi yale yote kuwapokea wakae kwa salama mtu ana shamba, amejenga, amefanya nini imekwishatupiliwa mbali.

**Com. Salim:** Una pendekezo nyingine?

**Mr. Charles Soweni:** Kwamba sasa wajijua kwamba wao ni wageni wa Taveta wapiganie viti huko kwao. Huoni mpaka ma-chief wako Taveta wa makabila mengine? Ma-sub-chief wako Taveta wa makabila mengine? Huoni kama walikuwa wanapendana? Na huo upendo basi wameumwaga chini?

**Com. Salim:** Pendekezo lingine?

**Mr. Charles Sowene:** Nimalizie hiyo. Lingine ni kwamba upande wa mashule, Ma-headmaster wamemaliza watu na wao. kwa hivyo Katiba iwachunge ma-headmaster, na ma-receipt yao ambayo si yale ya serikali mule shuleni. Kwa hivyo kama wewe huelewi waweza ukaletewa receipt yako na mtoto ukaona eeh, sawa sawa,la sivyo. Wanaumiza watu na hasa jambo lingine ni..

**Com. Salim:** Ungetaka wafanywe nini?

**Mr. Charles Soweni:** Waangaliwe, ma-headmaster wachungwe na Katiba, wasiwe huru kufanya wanavyopenda.

Ingine la madaktari. Madaktari wamejaza ma-dispensary yao. Watu wanakufa sasa kabisa na ndivyo wanavyopenda watu

waishe siku hizi. Baadaye wao wafanye nini. Na kwasababu wana madawa mengi haya yanaletwa na serikali katika mahospitali kubwa ya serikali, na wachukua wanapeleka kule wewe unakwenda kule mgojwa unaandikiwa unaambiwa nenda ukanunue dawa. anajua mahali dawa zake ziko na hiyo pesa ni yake. Hapa hospitali hakuna pesa. Katiba hii iwaangalie madaktari wamemaliza watu sasa wasikia malaria hasa inatangazwa zaidi kila mahali, watu watatibiwa na nini? Kama huna pesa ya kwenda kununua huko? Waona sasa si wewe ufe tu?

**Com.Salim:** Endelea.

**Mr. Charles Sowene:** Wacha niachie hiyo kidogo

**Com. Salim:** Asante sana. Asante Bwana Charles Sowene kwa maoni yako. Sasa tumuite Bwana Joseph Savai.

**Mr. Joseph Savai:** Kwa majina ni Joseph Savai, na napenda tu kuchangia kuhusu Katiba hii nikianza na tamaduni. Napenda kutoa mchango kwamba tamaduni hasa kwa ujumla haijaliwi na Katiba ilioko sasa. Na napenda kwa sababu tunaitengeneza basi ijali tamaduni za kila kabila nchini Kenya. Ili kwamba tamaduni hizo zitakapokuwa zimejaliwa mzozo wa kabila utapungua, kwasababu kama ni haki za kiuchumi pia zitaenda tu mahali panapostahili kwa hiyo jamii ama kabila ya tamaduni ile.

Na pia kwa upande wa siasa, utakuta tamaduni ile itakapojaliwa na Katiba yule mwanasiasa ambaye anataka kuwania kiti ama wadhifa wote wa siasa, itambidi tamaduni yake imruhusu Kikatiba ama kijamii ili aweze kupata kibali cha kuwania nafasi hiyo. Kwa hivyo napendekeza tu kwamba upande wa tamaduni Katiba ijali sana.

Nikija kwa upande wa serikali. Maoni yangu yanasema kwamba, huu muundo wa vyama vingi umeleta ukabila ama umechangia ukabila mwingi. Na napendekeza kuwe na vyama viwili vikuu vya siasa, kimoja kitakuwa mamlakani, na kingine kiwe ndio kwa upande wa upinzani.

Nikimalizia niseme kuwe na tume. Tumekuwa na shida ya uajiri maana sasa katika serikali ilioko Kenya sijui tuite ni Katiba ama tuiteje, utaona kwamba watu wa maeneo fulani maalum ndio wanapata ajira na wanasahau kwamba hata kule sehemu zingine kuna wasomi pia ama kuna watoto waliosoma. Na kwa hali hiyo sasa napendekeza kuwe na tume ya ajira ambayo itakayo chaguliwa kikatiba na bunge. Nafikiri sikuwa na mengi sana niko na huu uchache tu na hivyo nimemaliza.

**Com. Salim:** Asante Bwana Joseph Savai, na sasa ni Julius Alhamisi. Kwa sehemu hii ya kutoa maoni nafikiri tukidodoka nafikiri Bwana Joseph Kiluda alikuwa ameshaitwa sasa ako tayari kutoa maoni yake na mtaturuhusu kuwa firm kidogo kwa upande wa wakati, dakika mbili tu kila mtu. Lakini tumekubaliana. Tusipofanya hivyo mutaona tutaendelea tuje kumaliza usiku kucha. So Bwana Kiwe utatusaidia uki-summarize au kufupisha maoni yako. Asante.

**Com. Salim:** Asante Bwana Joseph Savai, na sasa ni Julius Alhamisi.

**Mr Julius Alhamisi:** Mimi ni Julius Lenjola Alhamisi, kutoka Jibe location. Maoni yangu kwanza ni kuhusu utamaduni. Utamaduni wa watu ni lazima udumishwe zaidi; kwa sababu unakuta kuna mila za watu na tamaduni zao. Watu kama Wataveta, wenyewe hupasha tohara, ambapo mtu kama hajapashwa tohara, utakuta yeye hayuko kwa fungu la rika fulani. Sasa, tamaduni za tohara kwa Wataveta, zinapasa ziendelee.

Kwa upande wa ardhi, ardhi inatakikana kila kabila liwe linasimamia ardhi yao, kwa sababu uchungu wa ardhi aujuaye ni mwenyewe. Kwa mfano, Mtaveta inatakikana asimamie ardhi yake kupitia kwa wazee wa njama. Kwa sababu kwanzia Taveta ianze kabila lao, wazee wa njama ndio walikuwa wanasimamia ardhi na kulikuwa hakuna matatizo. Ilipovunjwa, ikawa sasa matatizo kila mtu anataka kula, auze ardhi. Ni hayo tu.

**Com. Salim :** Asante. Patrick Mnawe.

**Patrick Mnawe:** Kwa jina naitwa Patrick Mnawe. Na maoni yangu ni juu ya ubunge! Ningependelea kwamba kwanza, mbunge awe mwenyeji, na pia awe ni mwakilishi wa constituency hii.

Kwa swala lingine juu ya mahakama, mahakama ningependelea pia, swala la kifo, liachiwe, yaani tuchague baraza la mahakama ndogo, kabla haijafikia kwenye mahakama kubwa. Wapendekeze, kifo, kiondolewe iwe ni maisha, badala ya kunyongwa.

Na swala lingine ni juu ya utawala. Utawala, ningelipendelea pia, rais akae kwa vipindi viwili tu. Na machifu pia wachaguliwe kutokana na qualifications zao. Swala lingine ni juu ya…

**Com. Salim :** (Inaudible)

**Patrick Mnawe:** Na sub–chief, kuanzia sub–chief mpaka chief.

**Com. Salim :** Achaguliwe na nani?

**Patrick Mnawe:** Achaguliwe na wananchi. Ambao ni citizens. Wa ile area ambayo constituency iliyoko.

Swala lingine ni juu ya haki za misingi. Ni juu ya kwamba ikiwa mtu ataruhusiwa kuvuta sigara, kama tobacco, pia turuhsiwe wale haki za wachache, kama kuruhisiwa watu watumie pia cannabis. Maana pia wako wengi ambao wanaotumia, wawe raia, walioko utawalani katika serikali na walioko pia. Si kitu cha haya, ama ni kitu cha ukweli, wengi wanatumia.

**Com. Salim :** Tafadhalini, ni maoni yake, kwa hivyo tumpe nafasi.

**Patrick Mnawe:** Cannabis ihalalishwe ka vikundi vichacheambao wanaotumia.

**Com. Salim :** Rudia hapo kidogo.

**Patrick Mnawe:** Swala la uraibu, kama vile watu wanavyotumia tobacco, ikiwa inahalalishwa, pia cannabis ihalalishwe. Maana ni uraibu ambao unatumika na wengi, walioko pia raia wote, walioko serikalini na mahakamani pia. Mahakimu pia wanatumia.

Na swala lingine juu ya rasilmali kama mbuga za wanyama. Tungelipenda pia wanyama wa pori, wengine, wahalalishwe watumiwe na raia. Kama vile butchers, zitolewe kama vile wanyama wa misitu, isiwe tu ni watalii wanaotumia huko cannivore, hiyo pia inaruhusiwa pia, wananchi watumie hawa wanyama wa misitu.

Swala lingine ni juu ya vijana, wanaofikisha miaka kumi na nane wapewe loan ya kujiendeleza, na pia kufunguliwe ministry ya sports kwa upande wa vijana. Na upande wa wakongwe wazee, waangaliwe wakati wa uzeeni.

Swala lingine ni juu ya wale wanaoshikwa na ugonjwa wa ukimwi. Nao, waangaliwe, watengewe sehemu zao. Maana pia wamwachwa bila kuangaliwa vizuri.

Swala lingine ni juu ya vijana wazururaji. Wameachwa na serikali inatakikana iwaangalie hao vijana.

**Com. Salim :** Hawa ni street children.

**Patrick Mnawe:** Yes street children.

Swala lingine ni juu ya maji. Maji, katika town, yalipishwe. Lakini mashambani, ihalalishwe, iw ni bure. Hayo ndio machache nilio nayo.

**Com. Salim :** Sylvano Mnene.

**Sylvano Mnene:** Kwa majina mimi naitwa Sylvano Sadalai Mnene, ni Mtaveta, mwenyeji wa Taveta. Kwa maoni yangu ya urkebishaji wa katiba, kwa siku ya leo tarehe mbili, mwezi wa tano, mwaka wa elfu mbili na mbili, ningeanzia na swala la kisiasa. Yaani mwanasiasa yeyote anayegombea kiti cha siasa, kiwe cha ubunge ana cha udiwani, awe ni mwenyeji wa pale,

sehemu anayo gombania kiti hicho.

Pili, naenda kwa upande wa elimu,. Elimu ya msingi, kuanzia darasa la kwanza mpaka la nane, ikiwezekana iwe ya bure. Na kufikia sekondari, iwe kiwango ambacho wazazi wanaweza kumudu. Na mtoto akibahatika kwenda national school, kutoka katika jamii maskini, ikithibitika apewe full bursary. Na viwango vya chuo kikuu, vya maliopo, viwe chini kiasi ambacho pia wazazi wa kima cha chini wanaweza kuwapeleka watoto bila matatizo magumu.

Tatu, swala la afya: ningependekeza kwamba, huduma ya matibabu, ikiweekana iwe bure.

**Com. Salim :** Isipowezekana?

**Sylvano Mnene:** Iwe kiwango ambacho raia wanaweza mudu kwa urahisi. Shule zilizotengewa watoto wasiojiweza, ama destitutes, ama zile zamani zikiitwa shule za watoto wenye uosefu wa nidhamu, ziwe zitahudumia wale watoto kweli wenye ukosefu wa nidhamu, na wale kweli watoto wanaotoka kwenye jamii zisizojiweza. Kwa mfano kama Stareheilitengenezewa watoto wasiojiweza, lakini leo ni ya watoto matajiri.

Swala la nne ni ardhi. Sehemu kubwa ya mbuga hapa kwetu, ni ya wanyama, hali wananchi wenyewe wana sehemu ndogo sana. Ingetengwa, kiwango fulani, hata kama ni asili mia kumi na tano, au asili mia ishirini, ya hiyo ardhi, ipatiwe wale ambao ardhi zao no ndigo ama hawana kabisa. Na wawe ni wenyeji wa kutoka pale.

**Com. Salim :** Endelea.

**Sylvano Mnene:** Swala la maji. Huduma ya maji, ifikie watu vile inavyowezekana kwa kima cha chini. Kwa sasa, iko juu sana kiasi ambacho inabidi watu tena warudi kuchota yale maji ambaye yako contaminated. Kwa hivyo, ikiwezekana, iwe katika kiwango ambacho kinaweza mudiwa na wananchi wote. Naona nitakomea hapo, nipatie wengine nafasi.

**Com. Salim :** Asante Bwana Sylvano kwa maoni yako. Lewanina Achi. Kabla sijaendelea, kuna mlemavu yeyote hapa leo? Hajapata kusema1 labda baada ya huyu ndugu yetu, utakuja wewe. Na, kuna yeyote ambaye ana taabu ya kusikia vizuri? Any deaf person? Maaana tunaye mmoja wetu hapa, ambaye anaweza kumfahamisha na kummueleza, kwa zile ishara ambazo ni sign language yote yanayosemwa. Hapa. Yuko mwenye kuhitaji msaada huo? Endelea Bwana Achi.

**Lewanina Achi:** Mfumo wa utawala uwe kwamba wazee…

**Com. Salim :** Jina?

**Lekwania Achi:** Naitwa Elijah Lekwania Achi, mzaliwa wa hapa Taveta. Naanza kwa kusema, kwanza mfumo wa wa huu utawala, uanzie kwa wazee asilia, waungane na me-counsellor, na ma-chifu, waunde baraza katika kiwango cha sehemu ya chini. Halafu hapo sasa ndio kuwe na mbunge, waziri mkuu na rais. Mbunge awe ni mwenyeji asilia, asiwe ni makabia ya kuja.

Sasa, nikianzia katika baraza, baraza hilo ndilo liwe na jukumu, wawe na majukumu, ya kulinda eneo lao. Wakianzia kwamba, kusiwe makabila yale yanakuja yasiwe yananyakua ardhi ovyo ovyo, bila idhini yao. Wawe ndiowalinda usalama. Kwa mfano, watu wageni wakitoka sehemu mbali mbali, kama wamekuja hapa Taveta, wazee hao, ama baraza hilo, liwe lina nguvu ya kuwapatia vagrant, ya kuondoka katika sehemu hizo ikiwa hawajulikani. Hiyo ni kwa sababu ya kulinda usalama kuwa na wizi, ama ujambazi ambao ndio tishio hapa Taveta. Makabila tofauti, yaheshimu mila na tamaduni za wenzao.

Ardhi ibaki ni ya wenyeji. Visa vya kubuni mashamba viwe ni wenyeji tu wanaweza kubuni. Mtu mwingine awe na haki tu ya kununua, ama kukodisha. Wale ambao wanajiita ma skuota, kusiwe na mtu, Mkamab ama kabila gani, anayejiita skuota hapa Taveta. Mtu ambaye anaweza kujiita squatter, na ana haki ya kugawanyiwa shamba, awe ni Mtaveta pekee yake. Na ukataji makaa, na mbao ambayo ndio tabia imeendeleea sana, baraza la wazee, ndio liwe linaweza kutoa haki ya mtu kukata makaa ama mbao.

Maziwa na misitu na game reserve, robo ya mapato yale ambayo yanapatikana kutoka katika rtasilmali hizi, robo nzima ipwe baraza. Lile kabila ambalo halikuandikiswa mwaka wa sitini na tatu, na sasa linadai usajili, kwamba mipaka yao ijulikane, na eneo lao lijulikane, kama wanataka kujiandikisha katika eneo la wenzao, hilo litupiliwe mbali, kuwa hakuna kitu kama hicho.

Mkenya anaweza kuishi mahali popote, bali tu awe ni mfanyi kazi waserikali ama mfanyi biashara anaweza kuishi, ama pengine kama amenunua ardhi, anaweza kuishi. Haya, mboga na matunda yanayoingia nchini wakati yasipohitajika, yasizidi gharama ya shilingi mia mbili, kwa kila mtu ambaye amebeba uke mzigo.

Siku za taifa zipunguzwe, ibaki ni siku moja tu. Kwa mfano sasa kuna Madaraka day, sijui Kenyatta day. Hizo zote zinafanya serikali iingie gharama sana, maana hapo kuna siku za mapumziko. Serikali inagharamika, kwa hivyo, ibaki ni siku mija ya kitaifa. Na hatuna haja, majambazi walituvamia na sasa tunafukuza, haina haja ya kukumbuka saa hizo ati ya kwamba tulivamiwa. Ibaki tu ni siku ya kitaifa moja.

**Com. Salim :** Unapendekeza siku gani?

**Lekwania Achi:** Zile siku za kitaifa, wacha hizi za kidini. Kama za kitaifa kuna Madaraka, tuko na Jamhuri day, tuko na Moi day, hizo zote ziondolewe. Hizo zote ziondolewe, ibaki siku moja ya kitaifa. Iwe ni tarehe kumi na mbili, Jamhuri day. Mtu kama waziri, au mbunge, ama maafisa wa juu wa serikali, akipatikan na ufisadi, afilisiwe mali zake zote. Uandikishaji wakazi wa serikali, ugawanywe kulingana na makabila.

Elimu iwe ni bure. Viti vya uwakilishaji kama ma counsellor, kama wabunge iwe ni bure. Unaweza kuingia bure, sio uote pesa yoyote. Serikali ipokee maoni ya raia katika budget ya serikali. Kama pengine raia wanataka kuwa na maoni, kwamba wanataka loan kutoka hiyo budget, wasikilizwe. Lakini maoni hayo yapitie kwa mbunge. Yangu ni hayo.

**Com. Salim :** Ahsante sana kwa maoni yako. Tukiendelea mbele, tutamuita Bwana Mgalla Neteso.

**Mugallo Netero:** Mimi naitwa Mgalla Netero, Mtaveta. Nataka kuchangia maoni kulingana na urekebihaji wa katiba. Kwa kweli, tungeomba urekebishaji wa katiba, utazama sana maswala utokaa na hospitalini. Wanyonge na madaktari wanaonea wale wanyonge maanake ukienda kama huna pesa, unaambiwa kwamba huwezi kutibiwa. Sasa tungeomba katiba ijaribu kutimiza hilo.

**Com. Salim :** Kama kufanya nini?

**Mugalla Netero:K**uzingatia madaktari, kuwatibu watu bure.

Swala la pili tungeomba, upande huo huo wa hospitalini, hawa wanaofanya kazi hospitalini, au wenye viliniki, hivyo viliniki waondolewe hivyo viliniki, maanake ndivyo tunakosa madawa, kupelekwa kwenye viliniki hivyo.

Swala lingine tulikuw tunaomba kwamba, kwa upande wa kutafuta wabunge viongozi, tungependelea kwamba, Wataveta wenyewe, ama wenyeji wenyewe, wa eneo hilo, watafute mbunge wao ama kiongozi wao wenyee. Makabila mengine, tungeomba pia warudi kwao wakaombe viti vyovyote vile wanavyovitaka. Sina zaidi, yangu ni hayo.

**Com. Salim :** Ahsante sana. Na sasa umuite Bwana Samiji Fundi ambaye ni mlemavu wa kwanza kutoa maoni yake leo na ingawa wako wengine waliofika mbele ya yeye kufika, nafikiri mtakubaliana na mi, nikimpa yeye nafasi kwanza. Ni sawa?

**Response:** Sawa.

**Samji Fundi:** Mimi Samji Fundi, mimi pendekezo kwanza ninaingilia upande wa walemavu kwanza. Upande wa walemavu, sisi ni walemavu, tunataka tuangaliwe kidogo na sisi vile unaweza kusaidika upande wa walemavu. Sio mimi pekee yangu, mpaka wale wenzangu. Tusaidiwe tu kwa upande wa jinsi tunaweza kuisaidia. Halafu tunaweza kurudi mambo ya katiba, tunataka kila mtu apate haki. Kama ni wakina mama wapate haki haki zao, kama ni wakina baba wapate haki zao sawa. Haya, tukiridi hapa tuna custom, custom hiyo inapata pesa na hiyo pesa haijulikani inaenda wapi.

**Com. Salim :** Umemaliza?

**Samji Fundi:** Naona kama nimemaliza. Ninakohoa hata kama ningekuwa na menginwe ya kuongea. Mambo ya hospitali tujaribu kuangalia. Hata sasa, kuna mtu amelazwa pale ameshikwa, amezuiwa pale, kwa sababu ya pesa.

**Com. Salim :** Unapendekeza nini?

**Samji Fundi:** Tunapendekeza, kitu kama ile itolewe. Saa hii kama kuna mama amelazwa pale, anamapacha, watoto wawili, na amelazwa pale ameshikwa mapacha hawatoki, yeye hatoki, yuko pale. Bwana hana chochote. Saa hii, yuko wadi pale. Sasa, wazee, sijui kama mtaweza kumchangia yule mzee mkamtoe.

**Com. Salim :** Sasa ninaona kwamba wakati ni mfupi sana na waliojiandikisha hapa ni record numbers. Hatujapata idadi ya watu waliojiandikisha kwa wingi kama hapa. Kwa hivyo, itabidi ama tupunguze time kwa kila mtu kusema au itabidi wengine warudi bila kutoa maoni yao. Au wafike kwa Ngina hapo kesho tuna kikao cha pili, Challa High School. Kwa hivyo, taadhilini msikasirike, taabu ni ur time na tutajaribu sasa, maanake tumesikia mengi, na maoni yametolewa kuhusu ardhi, kuhusu dawa na kila kitu. Kwa hivyo, ukiwa na maoni juu ya mambo haya, sema mimi nakubaliana na wenzangu, juu ya jambo hilo, na endelea mbele. Ukiwa na jambo jipya, ndio utasema. Lakini ikiwa hauna jambo jipya, mimi nakubaliana na wenzangu jambo hili na hili, ahsanteni, aje jamaa mwingine. Sawa hivyo?

**Response:** Sawa.

**Com. Salim :** So, tumuite sasa Bwana Richard Chaewa.

**Richard Chaewa:** Kwa jina naitwa Richard Chaewa, maoni yangu ni kama ifuatavyo:-

Kuhusu mambo ya ardhi, naomba katiba mpya igawanye, iangalie mambo ya ardhi; ardhi ya kwetu igawanywe na wazee wa njama. Kama ilivyokuwa hapo mbeleni uongozi wa kisiasa na kiutawala kuanzia viwango vya machifu kuteremka chini, pia wateuliwe na wazee wa njama. Wahamiaji ambao kwa namna moja au nyingine walinyakua kinyume na sheria. Pia wahamiaji ambao huenda wametoka nje ya nchi wasiruhusiwe kuwa na vibali kama vitambulisho vya nchi hii. Kama watakuwa na maeneo yao, sawa. Kama hawatakuwa na maeneo yao, lazima mipaka ya kidraftia iheshimiwe. Vipindi vya uongozi vya rais viwe ni viwili vya miaka mitano mitano.

Nisije nikasahau kwamba ninapendelea serikali ya majimbo. Mabaraza yaongozwe na wenyeji. Asante.

**Com. Salim :** Asante Bwana Richard Chaewa kwa maoni yako. Sasa Bwana. Muhammed Musa. Bwana Mwenyekiti ameniambia ya kwamba huenda wakawa jamaa hapa ambao wana memorandum, hawana haja kuja mbele yetu hapa. Memorandum inaweza kuja moja kwa moja, kwa maafisa wetu hapa. Hamna haja kungojea wakati wenu utajwe. Mmoja mmoja tafadhali! Tafadhalini wale wenye memorandum walete polepole hapa, wale wengine tusikize maoni ya wenzetu! Sasa

Bw. Mohammed Musa, yuko tayari kutoa maoni yake.

**Muhammed Musa:** Mimi kwa jina naitwa Muhammed Musa. Nimekuja hapa mbele yenu kutoa maoni ya Katiba. Kwanza ni elimu. Elimu ya msingi iwe bure, kusiwe gharama yoyote mwananchi atakayodaiwa. Elimu ya upili yaani secondary schools, iwe na kiwango cha kadri ya mwananchi wa kawaida aweze kusomesha mwanawe. Chuo kikuu mfumo wa zamani urudiwe.

**Com. Salim :** Vipi?

**Muhammed Musa:** Kwa mfano kuwe na boom yaani kuwe na marupurupu

**Com. Salim :** Iwe na marupurupu?

**Muhammed Musa:** Ndio. Haya kuhusiana na ajira, kuwe na usawa wa kuajiri na serikali ipangilie kufundisha watoto kazi ya mikono. Na kuwapa mikopo ya kujiendeleza.

**Com. Salim :** Usawa wa kuajiri (?)

**Muhammed Musa: N**dio.

**Com. Salim :** Usawa wa kuajiri . (?) usawa kati ya nani na nani?

**Muhammed Musa:** Wale watoto. Kuna watoto wengine ambao ...

**Com. Salim :** Usawa wa kufuatia kabila? Usawa (?)

**Muhammed Musa:** Eeh, usawa wa kufuatia kabila. Ndio, kusiwe na upendeleo. Kuhusiana na matibabu, matibabu iwe ni ya bure kabisa, kuanzia watoto hadi watu wazima. Ukuu wa Katiba; bunge kubadilisha sehemu yoyote ya katiba ni mpaka iwe imetimia asilimia sitini na tano ya watu wote wa Kenya kw akura ya maoni.

**Com. Salim :** Asilimia sitini na tano?

**Muhammed Musa:** Ndio.

**Com. Salim :** Through referendum only?

**Muhammed Musa:** Sorry.

**Com. Salim :** That is maoni ya raia.

**Muhammed Musa:** Ndio.

**Com. Salim :** Hiyo ni majority. Hakuna haja ya percent?

**Muhammed Musa:** Ni majority ndio. Kuhusu muundo na aina ya serikali, waziri mkuu awe na uwezo wa kuunda serikali iwe na majimbo na waziri mkuu awe na uwezo wa kuchagua magavana.

**Com. Salim :** Nani?

**Muhammed Musa:** Waziri mkuu. Kuhusu haki ya ardhi na mali, jamii ya mahali pale inufaike. Utawala; watawala wote wachaguliwe kupitia kwa kura za wananchi. Kwa mfano D.O., machifu, ma-assistant chief na wote wawe wametoka zile sehemu zao. Isiwe ni mtu pengine ametoka sehemu zingine za mbali anakuja anakuwa chifu wa sehemu fulani, au D.O. ametoka labda kule Kakamega anakuja kuwa D.O. wa Taveta. Inatakiwa mtu wa Taveta awe ndio anakuwa D.O. wa hapa maana ndiye anajua ile mazingara ya ile sehemu. Kusema maskwota, tunataka sheria ipitishwe kuwa maskwota wote walipo katika Kenya, kwa nini wasipatiwe sehemu ya kuishi?

Na mbuga za wanyama zinaweza kugawanyiwa watu sehemu kwa sababu zina sehemu kubwa. Pia wakati wa wakoloni, kuna wazungu walichukua sehemu kubwa wakati wa ukoloni, hizo sehemu nazo pia zigawanyiwe maskwota.

La mwisho, ni kuhusu ugombeaji wa ubunge; mbunge yeyote awe ni mzaliwa wa ile sehemu. Na sio mtu labda kwa mfano ametoka hapo Kibaoni Tanzania anakuja anagombania kiti cha ubunge hapa. Pia hali kadhalika na madiwani wawe wanatoka zile sehemu ambazo wamezaliwa. Ahsante.

**Com. Salim :** Bwana. Lashigoni. Lengereu Lashigoni

**Lengeren Lashigoni:** Jina langu naitwa Lungereu Mwanzia Lashigoni. Mzalendo wa Taveta. Maoni yangu ninayotoa hapa, ni kuhusu kuna kipengele fulani kilichopitishwa miaka iliyopita ya sixties kinasema Mkenya anaweza kuishi mahali popote, na tukiangalia hicho kipengele kina adhibu kabila zingine ndogo katika Kenya. Mimi maoni yangu ni kwamba, hicho kipengele kifutwe. Ikiwa ni Mkenya anaweza kuishi popote aishi, kibiashara aishi kiofisi lakini asiishi kimamlaka. Nikirudi nyuma kabisa nikusema kwamba nitakuwa na maoni ya marehemu mzee Ngala. Alipitisha hicho kipindi miaka zilizopita kwamba Kenya iwe

na majimbo. Lakini natumai hicho kipengele kilipuuzwa na saa hii kinasababisha wachache katika sehemu zao wanapata matatizo. Kwa hivyo mimi ningeonelea kwamba Kenya iwe na majimbo.

Cha pili ni kwamba, hicho kipengele kingine kinachosema ya kwamba machifu wanachaguliwa na serikali, mimi ningeona hicho kipengele kifutiliwe mbali kiwe wenyeji ndio wanaweza kuchagua chifu.

Na nikigusia kidogo kuna kipengele cha hii local government yaani njama. Hiyo njama ninaomba kwamba wapewe haki yao ya kumiliki ardhi kama jadi za zamani. Ahsante.

**Com. Salim :** Ahsante sana Lengereu Leshigoni. Na sasa namuita Bw. Alphonce Mrutu, yuko? Tafadhali tusikie sauti yako! Yuko? Hayuko. Esther M'bele yuko? Hayuko. Kirigisa mrutu.

**Kirigisa Mrutu:** Majina yangu naitwa Kirigisa Mrutu. Maoni yangu ni kama yafuatavyo; ardhi; mzozo wa ardhi lazima uwe unaeneshwa na committee elders ambao ni kama njama. Watu wa nje wasiwe wanakuja kutekeleza mizozo ya ardhi. Walinzi wa ardhi wawe ni committee elders ambao kama njama. Udhibitaji wa ardhi uwe ni wa kila mwananchi lakini awe anatoka katika jamii hiyo.

**Com. Salim :** udhibitaji vipi?

**Kirigisa Mrutu:** yaani mtu yeyote inatakikana athibiti ukubwa wa ardhi anvoweza lakini awe ni wa jamii hiyo hiyo, asiwe ni wa kutoka nje. Yaani kuwa na ardhi kubwa.

**Com. Salim :** Yawezekana?

**Kirigisa Mrutu:** inawezekana mtu kumiliki ukubwa wa ardhi, lakini awe anatoka katika jamii hiyo hiyo asiwe anatoka nje.

Uchumi: maoni yangu ya uchumi ni kwamba, mbuga zetu za wnyama pori, zigeuzwe kuwa game reserve. Na ikiwa haziwezekani, ziwe zinalipa asilimia sitini ya mapato yao. Ziwe tu zinalipia gharama ya kurekebisha maboma, sio kulipa bill kama inavyoendeshwa sasa.

Elimu: Elimu iwe bure hasa kwa walemavu, na pia kwa shule za kienyeji. Lugha za kienyeji kama Kitaveta zifunzwe mashuleni ili kudumisha utamaduni wa jamii hiyo.

Siasa. Ningependelea makabila yote, madogo ya Kenya yawe yanawakilishwa vilivyo bungeni na mbunge kutoka jamii yao. Pili,

ningependa wabunge wa kutoka eneo lingine wasiende kwa eneo lingine kufanya siasa. Tatu, anayegombea kiti cha ubunge, ni lazima apitishwe na wazee yaani community elders. Kwa mfano Taveta, wazee wa njama. Makabila madogo yapewe nyadhfa kubwa bungeni, kama kiti cha speaker.

Sheria. Mahakimu wawe na uwezo wa kuhukumu mtu kulingana na kosa alilotenda bila kuingiliwa na serikali. Kwa mfano, waliostakiwa kwa kosa la Goldenberg, serikali iliingilia na wote wakaachiliwa. Pili, mzazi yeyote ambaye anapatikana na kosa la kumbaka mwanawe, ahukumiwe kifungo cha miaka isiyopungua ishirini hadi thelathini.

Uhaki na uajiri wa watu: Maoni yangu ningeomba ya kwamba, watumishi wote wa serikali hasa polisi, administration police, prison, wawe na chama chao cha kuwatetea maslahi kazini. Pili, ningeomba makabila madogo madogo nchini Kenya yawe yanapatiwa nyadhfa kubwa kazini. Kazi ya serikali kama D.O. D.C. ,P.C. na hata P.C. ahsanteni.

**Com. Salim :** Asante Bwana Mrutu. Bwana Alfred Stoni yuko?

**Alfred Ngaluma:** Kwa majina naitwa Bwana Alfred Stoni Ngaluma. Nataka kuchangia hii hoja ya Katiba.

Nataka serikali iwe ya majimbo kwa sababu ndio itakuwa rahisi kutumikia mikoa yao.

Bunge: Mtu anayetaka kugombea kiti cha bunge au diwani ni lazima aidhinishwe na wazee wa eneo lake yaani community elders yaani njama. Pia hiyo bunge pia ijali yale makabila madogo madogo yaani kabila hilo kama halijawakilishwa bungeni, wateue mbunge kutoka kwa lile kabila ndogo.

Urais: Awe anatumikia vipindi viwili vya miaka mitano mitano.

Ardhi: Ardhi imilikiwe na community elders hasa kwa mfano, kuna zile areas kulingana na vitamaduni, za mwafrika, kuna ardhi zile zilitengwa ambazo huwa zinatandikiwa au kufanyiwa maombipale kwa mfano kuna challa (?) zishanyakuliwa na watu ambapo ile misitu ilikuwa inachungwa hapo ili kuondoa kufanya ile mitandiko, sasa ningeliomba, ama pendekezo langu ile community elders kama njama hivi, wapatiwe uwezo ya zile ardhi ambazo zilinyakuliwa, na ambazo zilikuwa zinalinda watoto wetu kwa wakati yao, hiyo community elders kama njama ipatiwe uwezo wa kuzindisha hiyo ardhi.

Elimu: Elimu ya msingi kuanzia standard one mpaka standard eight iwe ya bure kwa sababu watoto wa maskini wengi hawasomi.

Hospitali pia iwe ya bure kwa sababu watu wengi hufa hata hawana pesa ya kuhudumia jamii zao.

U-mayor na chairman wawe wanachaguliwa na wananchi.

Mazingara kam vile maji, kama vile hapa Taveta naunga mkono yale wenzangu wamesema. Siwezi kurudia hayo. Hiyo nilikuwa natia mkazo tu. Kwa mfano mbuga hiyo ingelistahili K.W.S. ipatie watu wenyeji wa hapo, atleast 60% yale mapato ambayo yanatoka pale. Kwa maana kulingana na hapa Taveta tunanyanyasika sana. Unakuta ile pesa nyingine inatoka hapa inaenda kwa ile mikoa ingine ama inaenda kunufaisha watu wengine wa huko nje. Sisi tunaumia tu. Si serikali, si nini. Yangu ni hayo tu. Asanteni

**Com. Salim :** Asante Bwana Alfred Stoni Ngaluma kwa maoni yako. Sasa Bwana Philip Nzirai. Dakika tatu Bw. Philip.

**Philip Nzirai:** Kwa majina naitwa Phillip Longida Nzirai

Katika kurekebisha katiba, naomba kuwa, tuweke kipengele hichi, yule anayepigania katika ubunge, awe ni mwenyeji wa pale.

Natoa maoni ya kuwa kuwe na malipo maalum ya ulipaji wa maji.

Rais awe na muda wa miaka kumi, au vipindi viwili. Mpiganiaji kitini lazima atoke katika sehemu anayopigania. Yaani mwenyeji, kabila ya hapo.

Muundo wa serikali iwe serikali ya majimbo. Wazee wa mtaa wawe ni wa kabila hilo la hapo mahali.

Ningependelea ya kuwa kuwe na sheria ya kuwa mtu akipachika mtoto wa shule mimba, achukuliwe hatua kali, adhabu. Misaada yoyote ipatikanayo ipelekwe ianzie katika kiwango cha chini.

Wakati wanapochaguliwa katika kazi ya jeshi, polisi kila kabila ipatiwe nafasi. Ndoa za kienyeji zisaminiwe kwa bahati mbaya kama mtu amefariki, lakini akipata uthibitisho kuwa alikuwa ni mke wa mtu fulani (?) zake.

Hospitali, shule ziwe za bure.

Machifu ma-D.O wasiruhusiwe katika ugawanyaji wa ardhi. Kama ipo waachiwe wazee wa mitaa, wazee walioteuliwa. Kamati ya mashamba iwe ni ya wazee wa sehemu hiyo. Machifu wachaguliwe na wenyeji, wananchi. Sina mengi ni hayo tu.

**Com. Salim :** Ahsante Bwana Nzirai. Bwana Edward Lerengesu.

**Edward Lerengesu:** Naam, kwa majina mimi ni Edward Lerengesu. Nina maoni yafuatayo:- Kwanza, katiba ya Kenya iwe na utangulizi, na utangulizi huu utaje mwongozo wa muelekeo wa kitaifa.

Pili. Bunge lisiwe na uwezo wa kubadilisha sehemu yoyote ya Katiba bila kuhusisha wananchi kama inavyofanyika sasa.

Kuhusu raia, serikali isiruhusu uraia wa mtu katika nchi mbili.

Kuhusiana na usalama wa kitaifa, wakati wa uteuzi wa wanajeshi, askari, serikali izingatie usawa katika kila kabila la Kenya.

Kuhusiana na utaratibu wa uchaguzi, serikali ihakikishe kwamba makabila madogo yote ya Kenya yamepata uwakilishi bungeni.

Kuhusiana na haki za ardhi, jamii na watu binafsi wenyeji wa eneo hili, wawe na haki ya umilikaji wote, kando na ile inayomilikiwa na serikali. Kuhusiana na tamaduni,.

**Com. Salim :** Ukisema wenyeji, wenyeji ni watu wote au

**Edward Lerengesu:** Wenyeji wa hapa kwa mfano Wataveta. Ni swala la ardhi. Nitarejea vile nimesema. Jamii na watu binafsi, wenyeji wa eneo hili Wataveta wawe na haki ya umilikaji wa ardhi yote kando na ile inayomilikiwa na serikali.

Tamaduni za wenyeji wa eneo hili ziheshimiwe kuhusiana na mali ya asili, mali asili iliyo katika eneo fulani, iwafaidi wenyeji wa eneo hili moja kwa moja kwa kiwango fulani.

Kuhusiana na haki za kimsingi, serikali ihakikishe kwamba kila kabila linaangaliana katika ajira za kazi mbali mbali za serikali.

Halafu, serikali ihakikishe kwamba kuna matibabu ya bure katika hospitalu za serikali: ahsante.

**Com. Salim :** Asante sana Bwana Edward Lerengesu. Nimrod Kitoshe. Hebu tafadhali muiteni. Yuko mbali sana? Juma Saleri- ameondoka, simeon Kalai Mkalla, ameshapeana. Jeremiah Kimaro

**Jeremiah Kimaru:** Kwa majina naitwa Jeremiah David Polonja Kimaro. Ninatoa maoni yangu kama ifuatavyo. Jeremiah David polonja Kimaro Jeremia D.kimaro.

**Com. Salim:** Endelea

**Jeremiah Kimaru:** Maoni yangu ni kama ifuatavyo. Kwa upande wa urais, ningependekeza kwamba uchaguzi wa rais awe atachaguliwa kwa asilimia ishirini na tano, kutoka katika mikoa mitano. Au asilimia sabini kwa kura zote zitakazopigwa nchini. Rais asiwe mwakilishi wa bunge mahali popote. Awe ni rais peke yake, wala hawakilishi sehemu yoyote katika bunge na asiwe mtu ambaye amehusika katika kashfu za aina yoyote katika maisha yake. Awe na vipindi viwili vya miaka mitano peke yake, awe na uwezo wa mambo yafuatayo peke yake: kumchagua amri jeshi mkuu, pili, waziri mkuu au naibu wa rais.

Bunge liwe na uhuru au na uwezo wa kuchagua wafuatao: mabalozi, permanent secretaries na senior civil servants ama wafanyi kazi wa serikali wa ngazi za juu. Hawa wachaguliwe na bunge na wawe watapitishwa na rais, au wachaguliwe na watu hao watatu walioko juu, rais, amri jeshi mkuu na waziri mkuu ama wapitiswe na mtu wa asili la kabila lile la mahali pale. Maanake kwamba, makabila yote arobaine na mawili yaliyoko Kenya yawe yana mwakilishi moja mmoja na wale wengine wawe ni wa ziada ama ni wa kujazia. Isipokuwa pengine kwenye miji mikuu ambayo ina zaidi ya sehemu mbili za uwakilishi bungeni. Hii itasaidia kuzuia watalii wa kisiasa, kunyanyaswa na kugandamizwa kwa makabila madogo madogo.

Utawala wa mikoa ukianzia ngazi za chini kabisa kama wazee wa mitaa, mpaka kufikia machifu wawe watalipwa mshahara na wachaguliwe na wananchi. Serikali za mitaa, isipokuwa kwenye miji mikubwa kama vile Mombasa, Nairobi na kisumu, kwingine kote wawakilishi wote wawe wa kabila la mahali pale na wenye asili ya pale. Wenye kuzijua mila, desturi tabia na hali ya matatizo ya kimsingi ya mahali pale, wengine wote wafanyebiashara na kazi zao kama jinsi walivyokuwa wakifanya.

Uwakilishi bungeni: Kuna umuhimu wa kabila kuwakilishwa, kila kabilakuwakilishwa bungeni. Usalama na uhalifu: kwa ajili ya kudumisha usalama na kupunguza uhalifu. Sheria ya zamani ya vagrancy and vagabond Act irudishwe na kutiliwa mkazo. Hii si kusema kuwa watu wasiwe na uhuru wa kutembea mahali popote Kenya, ila kila mtu aweze kujieleza wakati na mahali popote anashughuli gani, au anashughulika na mambo gani kimaisha.

Ardhi: Kabila la mahali popote wawe ndio wenye haki ya kumiliki ardhi mahali pale. Ardhi yote. Stateland au kama zamani wakiita, crounland ambayo ni ya serikali, na trustland ya mahali popote pale. Iwe haki ya makabila pale na watu wenye asili ya mahali pale. Kama ni kugawanywa, watu wa kabila lile wenye asili ya mahali pale, wawe ndio watakaopewa kipaombele.

Kiongozi wa ngazi yoyote anayeshikilia mamlaka yoyote ya kiofisi au ya kisiasa, akihusishwa kwenye kashfa ya aina yoyote ni lazima ajiuzulu au aondolewe mamlakani kwa nguvu, mpaka atakaposhinda kesi au shtuma hizo. Viongozi wote wa ngazi zote ni lazima kuorodhesha mali yao yote, na jinsi walivyoipata kabla ya kuingia mamlakani. Serikali ihimize kuhakikisha elimu ya msingi iwe bure kwa watoto wote Kenya.

Pensheni ama malipo ya uzeeni: serikali iweke mikakati ya malipo ya wazee na wastaafu kuwe na aina ya hazina, ya wasio na kazi au ajira, na wazee kwa miaka ijayo. Affiliation Act; vijana au wazaziwa kijana yeyote atakayempa msichana yeyote mimba bila kunuia kumwoa ni wajibu alazimishwe, ama wazazi wake wawajibike kumlea mtoto yule, mpaka atakapofika miaka kumi

na minane. Ni hayo tu niliyonayo.

**Com. Salim :** Asante sana. Cecelia Kionza. Hayuko? Crispin R. Grogan yuko? John Simeon, Joseph Kiloda. Karibu. Kuna shida moja hapo nje, mwenzetu mmoja kumfungia nje mwenzake kwa baiskeli yake, sijui ni nani mwenye baiskeli iliyofunga njia. Yeyote mwenyebaiskeli tafadhali aende a-check ikiwa ni baiskeli yake ndio ampe njia mwenzake. Sasa, tunashauriana hapa, mko wengi na pia kuna haja ya wengine labda kwenda wakala chochote na desturi yetu pia kuwa na dakika chache sisi kuenda kupumzika yawezekana tupumzike kwa muda wa dakika nusu saa, sote turudi kuendelea.

**Response:** Sawa.

**Com. Salim :** Ni sawa.

**Response:** Ni sawa. Tafadhalini mtarudi na tuombe kwamba mtaweza kumaliza. Nyinyi mtaendelea kuwa registered (?) wafanye mlolongo wa ku-register na kuweza kuendelea. Asanteni sana.

**Mr. Joseph Kirote:** Kwa majina naitwa Joseph Kirote, na haya yafuatayo ndiyo maoni yangu. Nina mengi ya kuongea lakini ningependa niingatie machache.

La kwanza. Nikianza na ardhi na mali. Nikiona na maoni yangu, ardhi ama mali inatakiwa imilikiwe na jamii ya sehemu ile, the indigenous people.

Pili upande wa haki za kimsingi. Unapoendelea kuangalia hasa katika taifa unaona street children au machokora wameendelea kuwa ni wengi sana. Sasa ili kuondoa keu ingelikuwa elimu na afya iwe ni bure ili labda hata wale ambao hawajiwezi waendelee kujimudu pia waendelee kuonekana kama Wakenya. Pia nasema elimu na afya ziendelee kuwa bure kwasababu kuna hiki kitu kinaitwa tax. Tuangalie mtu kama chokora hata akinunua ile koo pale dukani huwa kuna tax ambayo huwa inakatwa pale. Sasa basi vitu kama hivyo viwe bure kwa sababu hata yule chokora ana-contribute ile tax.

Haya nikienda upande wa bunge. Ningependa mwakilishi wa bunge awe ni mwenyeji wa jamii ile pale ambapo panapiganiwa ubunge. Na Kadhis kama kuna zile mitihani huwa wanapewa, the languages napendekeza pia wapewe mtihani wa asili ikiwa kama ni Mkamba apewe pia mtihani wa Kikamba, kama ni Mtaveta apewe mtihani wa Kitaveta na ile (?).

Haya tukiendelea upande wa ajira, kwa mfano upande wa forces. Twaona kuwa tunalaliwa sana, kuna kabila zingine zinachukuliwa zaidi kuliko zingine. Sasa ningeliomba kuwe na equal chances. Kuwe na usawa.

Upande wa serikali ningelipendekeza kuwe na serikali ya majimbo ili kuwe na heshima ya kimipaka. Ukiangalia upande hasa wale walioko maeneo ya mipakani kuna hizi nyumba wanaita custom. (?). Tungalipenda zile custom, zile pesa wanazokusanya katika custom pale ziwe zinamfaidi zaidi ile sehemu ya pale zaidi kuliko sehemu zile zingine sasa zote zinakusanywa zinachukuliwa zinapelekwa mahali kama Nairobi. Ningelipendekeza kwamba kitu kama 80% ya zile pesa inufaishe pale labda 20% ipelekwe nje.Pia council iwe hivo.

Halafu kuna hiki kipindi cha bunge hiki wabunge wanaongea jinsi wanaongea katika bunge zao. Mimi ningependekeza kuwe na uwazi yani iwekwe kama kipindi maalum katika redio kama Tanzania. Ili mbunge wangu yule ambaye nimemuchagua nijue anaongea nini pale katika bunge, asiwe anaongea tu matope kule. Kiwe wazi kama vile matangazo nisikie mbunge wangu yule niliomchagua anaongea nini ili akija hapa nimkosoe nimrekebishe. Yangu ni hayo.

**Com. Salim:** Na sasa tutamuita Bwana Jomo Nemrod. Jomo Nemrod yuko? Hayuko? Joshua Elijah? Joshua Elijah? Othiniel Betty Nyoki? Hayuko? Raymond Mnene? Dakika mbili tafadhali.

**Mr. Raymond Mnene:** Mimi naitwa Raymond Mnene. Ningependa kuzungumza kuhusu uraia. Uraia nazungumzia Kenya hii ni kwa mtu ambaye ameamua kuchagua kuwa raia, akishazaliwa, akikaa mpaka miaka kumi na nane katika Kenya hii. Akifika miaka kumi na nane akichagua kuwa Mkenya aruhusiwe kwasababu amekaa miaka kumi na nane.

Kuhusu mwanamke alioolewa kutoka nchi nyingine, mtu akiwa na mkewe ameolewa hapa basi aruhusiwe kuwa raia kamili atakapofikisha miaka tano akiwa na mume huyo.

**Com. Salim:** Jambo hili (?) (inaudible)

**Mr.Raymond Mnene:** Mume asipewe. Mimi nazungumzia mke. Kuhusu Passport yaani Pasi. Iwe kila Mkenya awe anaweza kupata passport isiwe ngumu kama ilivyo sasa walegeze masharti ya kupatia kila raia anayeomba passport isiwe tu kwa wa wasomi na watu wenye biashara matajiri.

Kuhusu aina ya serikali mimi nasema naunga serikali ya federal system yani majimbo ili kuilinda haki za kisheria, za kisiasa, za kiuchumi za wale makabila madogo madogo. Bungeni basi kila mmoja aruhusiwe kuwa na member. Na jambo ambalo ningesema nikitaja bunge ni kwamba sio makabila arobaini na mbili tu labda kuna makabila mia moja hiyo ni kusema kwamba wote waruhusiwe hata kama wako makabila mia moja sio arobaini na mbili ninayosema, waruhusiwe kuwa na mbunge wao maanake viti vya bunge viongezeke na ikibidi mishahara ya wabunge ipunguzwe ili kila mmoja aweze kuwakilishwa.

Kuhusu elimu iwe ni ya lazima na kila mmoja aruhusiwe kuwa na elimu ya msingi yaani primary school, na iwe bure.

Kuhusu umilikaji wa ardhi. Wenye kumiliki na kuwa na sauti ya mwisho ya umilikaji wa ardhi hiyo ni watu wa eneo hilo wazaliwa wa hapo wale wanaitwa indigenous locals, wenyeji wa hapo. Na watu wa nje raia wa nje ambao si raia wa nchi hii, wakiruhusiwa kupewa ardhi wapewe kwa ajili ya vitendo vizuri lakini baada ya kuchunguzwa sana na ardhi zao ndiyo ziwe ni kwamba zimestawishwa na zinaendelea, na maeneo wanayolima yawe pia yana manufaa fulani kwa wale wenyeji wa hapo.

Management ya national resources yaani mali ya asili, isimamiwe hasa kama national parks kama hizi tulizonazo hapa ziendelee kuwa lakini ziwapatie watu waliozizunguka faida zaidi ambayo inawapa kuliko hii ya sasa. Kwa mfano, kwa sasa national parks haiwafaidi sana watu wa eneo hili na ikibidi ikatwe hiyo national park wakati kutakuwa na msongamano wa watu kama sasa na hiyo nikionyesha mfano ni kwamba eneo hili la Tsavo West national park, lingepasa kwa sasa litolewe corridor hapo ya 10 km kushoto, 10 km kulia kuungana na maeneo yale ya kule ili watu waweze kuishi na kuondoa Taveta hapa imekuwa kama kisiwa.

Jambo la mwisho ni juu ya uongozi. Ingetakikana mtu kuzuia ufisadi yani corruption kuwe na yule mtu ambaye wanamuita msimamizi wa mambo ya utawala ambao ni wa haki kwa kingereza wanamuita obdusman. Awepo kwa kuchunguza mambo yote ya ufisadi kama ambavyo zilivyo nchi zingine ambazo wamechukua serikali.Nafikiri yangu ni hayo.

**Com. Salim:** Asante Bwana Raymond Mnene na sasa namuita William Sirai. William Sirai Yuko? Dominic Lekumala, hayuko? Ngodi Ngoira?

**Mr Ngodi Ngoira:** Majina yangu ni Ngodi Ngoira kutoka sub-location ya (?).Yangu ni yafuatayo;

Mtu yeyote ambaye ni mhalifu akifungwa jela na akimaliza kifungo kama si mzaliwa arudishwe kwao na serikali. Mtu yeyote akishikwa na silaha kama bunduki kinyume cha sheria afungwe maisha.

Mnyama wa pori kama ndovu wakiharibu mazao ya mkulima serikali ilipe mazao hayo milion moja. Mtu akiuliwa na ndovu ama simba, alipwe milion tano na akijeruhiwa alipwe milion mbili. Mwalimu wa shule akipatikana amepatia mtoto wa shule mimba afungwe miaka tano. Yangu ni hayo.

**Com. Salimwaka:** Asante Bwana Ngodi kufupisha kabisa maoni yako. Sasa tutamuita Jonah (*inaudible*) Brown Baba? Hayuko. Simeon Mbele?

**Mr. Simeon Mbele:** Asante mwenye kiti wa tume. Jina langu ni Julia Mbele, jina la kwanza ni Simeon. Nimekuja kuwakilisha Wataveta maoni tano na mimi nikiwa secretary nilikuwa nimekusanya maoni yao kama jamii yao. Kwa vile document ambayo nimefanya compilation ni kubwa sana nimeona hakuna haja kutoa maoni mengine ingawa hatukuwa na maoni ya mtu mmoja lakini pia inatakikana. Kwa hiyo nimechagua yale ya muhimu na yale ambayo haijasemwa. Lakini hata hivyo ningependelea sana

kusema jambo ambalo limewauma Wataveta, nikuwa kabila la Wataveta halijaweza kuwakilishwa vizuri katika bunge. Wakati makabila mengine yananafasi kupata sauti katika bunge.

La pili. Majadiliano ya bunge kwa mfano yawe hewani moja kwa moja wakati bunge linapoendelea. Katika constituency ya Taveta, wananchi wameomba Taveta council welfare kama vile imeshaongewa na kusikiza pia yaani njama, iwe na uwezo mkubwa wa ushauri katika kura na katika ufafanuzi wa aliye mwananchi na asiye mwananchi wa Taveta. Maanake Taveta ni nchi imezingirwa na nchi ingine. Imezingirwa na makabila mengi mengine ya nchi ingine na mengine ya kuja hapa kwa hivyo ni vigumu sana kumwonyesha mwanangu Mtaveta ni nani hajui lakini wale wazee wa zamani wanajua. Ndio maanake tungependelea wale wazee wa njama wawe katika soni wakati kuna matatizo. Pia njama ndio iwe na nafasi ya kwanza katika ushauri watakae upiginia ubunge, hasa tukiwa na wagombe wengi wengine kama inavyojulikana wakiwa ni wachochezi tu.

Tumeonelea pia kuwa ma-diwani walioteuliwa wawe ni technocrats yani wawe na ujuzi wasiteuliwe tu kwa vile wanaweza labda kuongea kwa maneno hivi lakini wawe wana ujuzi pia wa kazi ambayo watakayofanya.

Nikiendelea kwa haraka maanake haitakuwa coherent lakini nitajaribu if you are in this hall

(?) inaelekea mwisho kuanzia kwa mfano mwaka 1918 vita vya ,kwanza kana kwa mfano katika Taveta. If you are in this hall jukumu yake yaani mandate yake tuseme imekaribia kuisha. Kwa hivyo mwananchi wa Taveta wanasisitiza sana serikali ijaribu kuweka nafasi ya kwanza ya wale ambao wako katika hii sehemu ambayo ina sehemu ambazo zinaendelea kugawanywa…

**Com. Salim:** Inaudible.

**Mr.Simeon Mbele:** ambazo (?) ambazo zimekuwa zimefanywa mkataba zamani za kale zaenda kwishwa lakini sasa zaenda kwisha utaona kuwa utasikia katika Taveta kuwa mashanba yauziwa watu wengine. Na hali Wataveta wenyewe hawajaelezwa kwamba mashamba inauzwa na wao wenyewe pia wana haja ya mashamba hawana nafasi.

**Com. Salim:** Kwa hivyo?

**Mr.Simeon Mbele:** Kwa hivyo tunaomba kuwe na nafasi kama hizo katika sehemu ambazo ziko karibu na sisi. Sisi wenyewe tuelezwe katika Kenya Gazzette (?) kabla hazijakuwa advertised (inaudible)

Mbuga za wanyama, maji,michechemi, mito, maziwa, uvuvi wa samaki, madeni kama mbolea (?) misitu, Katiba iweke sheria kikamilifu mapato ya mali hizi wananchi na wenyeji wawe na kiwango chao na wawe na share isiyopungua kama 40%.

**Com.Salim:** (Inaudible)

**Mr. Simeon Mbele:** Kidogo. Za muhimu, juu ya sheria nafikiri ..

C**om. Salim:** (Inaudible)

**Mr. Simeon Mbele:** Ndiyo ni ndefu sana tena nashidwa jinsi ya ku…lakini walisema pia wako na haja ya supreme court kufuatana na ongezeko la idadi ya raia katika Kenya. Na maswala mengine ya magojwa ambayo yako tofauti na sehemu zingine ambayo yanakumba wenyeji kama wa hapa kama tryponomiasis, na malaria na bilharzias.Pia kuwe na sheria ambayo (Inaudible).

**Com. Salim:** Shukrani Bwana Simeon Mbele kwa niaba ya wenzako, memorandum yako na maoni yako. Vincent Lasewu. Karibu.

**Mr. Vincent Lasewu:** Kwanza napenda kutoa shukrani kwa ma-commissioner ambao wametutembelea hapa Taveta siku ya leo tarehe mbili, Mimi kwa jina naitwa Juma Lusewu. Ni mwenyeji mkaaji waTaveta asilia. Kwa kuchangia katika mjadala huu ni kwamba mengi ambayo nilikuwa nizungumze yameshazungumza, lakini kuna tu maoni matatu ambayo naomba kuchangia. Na mojawapo ni kuhusiana na dini.

Dini zimezingatia ama zimekuwa chombo ambacho kimeongeza chumvi katika kumtukuza Mwenyezi Mungu. Na katika kuongeza chumvi huko kumefanya dini kutozingatia ule umuhimu wa kumshukuru Mungu, maana dini zimekuwa nyingi na zina haribu mila zetu za asilia.

**Com. Salim:** (Inaudible)

**Mr. Vincent Lasewu:** Pendekezo ni kwamba tungeliomba katika Katiba ifanywe dini zipunguzwe. Kama zamani hapa Taveta palikuwako dini tatu nazilikuwako nzuri sana zikistaani na watu walikuwako wanaelewa vizuri. Kulikuwako hakuna mtu anamuita mamake dada, wala babake ndugu, walikuwa wanajua watoto zamani kwamba baba na mama ndio Mungu wao wa pili. Siku hizi wanaambia sio. Kwa hivyo hiyo tabia imeleta upungufu wa imani katika dini.

Yangu ambayo pengine itakuwa ni kuhusiana na hawa wazee ambao wanatajwa wa njama. Katika ufafanuzi wa njama nafikiri Bwana ma-commissioner hamujaelewa kwamba njama ni nini, munaambiwa kwa jina njama, naomba nieleze njama ni nini kwa ufupi. Hapa Taveta tuko matiti matano. Tufanye iwe njama, mbare tano, kuna Mrutu, kuna Mzirai, kuna Mnene, kuna Ndigiri na kuna Mzuya. Hawa ndio wamafanya jina njama likawepo na ndio chanzo cha Taveta, na ndio nguvu ya Taveta na ndio moyo wa Taveta. Kuvunjika kwa hawa ndio kumetia madhara yote ambayo tunaona tunapata taabu. Mwanzo zamani walikuwa wanachukuliwa sana na serikali. Serikali ilikuwa haipitishi jambo bila wao kupitishiwa hilo jambo na kukubali. Sasa tunaomba

katika maoni haya ya Katiba. Ule mtindo wa njama kurukwa usiendelee, ili wenyeji kupata haki yao njama irudishwe kama zamani.

Nina hakika mutauliza njama ina wanawake ama ina vijana ama ina nani ama ina kilema. Hawa njama ni representatives wa kila ukoo, kwa hivyo hata mwanamke yuko represented pale. Hata kilema yuko represented pale. Hii ni serikali ya ndani. Kwa hivyo unyanyasaji umetokana kwasababu serikali ya ndani ilinyang'anywa yale mamlaka yake ndiposa kuna sababu moja; ardhi waliokuwa wanachunga nailikuwa ni mali yao wakanyang'anywa. Pili walikuwa na uwezo wa kumpeleka mtoto yeyote maskini shule na kumtolea fees. Huo uwezo wakakosa kwasababu hawana pia pesa.

Tatu ni kwamba wao ni wakilishi wa kutizama haki za mnyonge ambaye babake amekufa akiwa mtoto na akaacha mali ambayo hiyo mali ina haki ya kuchungwa walikuwa wanachunga mpaka huyo mtoto anakua na anakabidhiwa ile mali rasmi bila hata kumnyang'anya chochote. Kwa hivyo ndiposa munaona maoni mengi yanatoka kwamba njama ipewe ule wajibu wake kwa hivyo iingie katika Katiba kwamba njama ni uhai wetu hapa kwetu Taveta kama kule Mwatate Taita wanatumia Eni mwana na sisi hapa tunaita njama.

Yangu ya mwisho ni kuhusiana na serikali za mitaa. Serikali za mitaa huduma zake zinastahili ziongezwe ama zisambae kijijini maana zinaishia kufagia soko ama katika town na yule mwenyeji ambaye huhudumia, hutoa senti zaidi ile hudumu haipati sawa sawa. Na ikizidi katika city council town hao ma-chief, sub-chiefs ikiwezekana katika Katiba wachaguliwe na wananchi na wawe wakilipwa mishahara na serikali za mitaa. Na wasichaguliwe watu wa kutoka nje ya njama bali watoke ndani ya njama. Wateuliwe na njama.

**Com. Salim:** Ya mwisho?

**Mr. Vincent Lasewu:** Ya mwisho, mbunge. Mbunge kulingana na mila na desturi, tangu zamani kabla ya uhuru alikuwa anatoka ndani ya wazee wanaitwa njama na hiyo tunaomba kwa wakati huu katika kubadilisha Katiba kusiwe na kuingiliana, kunyanyasana utoke Taita uje kugombeana hapa, utoke Ukambani uje kugombeana hapa. Bali tunataka mtu atoke hapa hapa na atoke ndani ya njama maana tunajuwa huyo tayari ni mmoja ambaye atachunga maslahi ya uraia kamili. Kwa hivyo kwa hayo machache, asante.

**Com. Salim:** Asante Bwana Lasewu na tutamwita Bwana (?) Saidi Shauri? Yuko? Ameondoka. Okay, Elizabeth Maninge yuko? Mtawa Longake, karibu.

**Mr. Mutawa Sikake:** Mimi naitwa Mtawa Saninwa Sikake. Yangu machache kwasababu yamezungumzwa mengi, na mengi yamesemwa yale ningesema lakini nina mawili matatu. Nazungumzia habari ya ardhi. Habari ya ardhi Taveta ilikuwa ikisimamiwa na njama, kama kuna matatizo ya shamba limefanya makosa watu kugombana njama ndio inasimamia kesi hiyo na

inatatua matatizo

**Com.Salim:** Tafadhali Bwana Mutawa (Inaudible)

**Mr. Mutawa Sikake:** Basi wacha hii niruke hii. Nasema hivi, njama inasemekana Taveta ni kitu cha vizazi zaidi ya kumi na tano sio kama njama imeanza sasa. Inazaidi ya vizazi kumi na tano. Kwa hivyo njama ndio inasimamia Taveta kwa hivyo tunaomba iendelee kusikizwa na serikali. Maanake sababu njama na serikali ni kitu kimoja. Na watu wa Taveta wana hakika kwamba wako kalike Kanu wote wakijua kwamba njama inawachunga na serikali ina wachunga. Nafikiri nimemaliza.

**Com. Salim:** Asante kwa kuwa na maoni wazi wazi kabisa na fupi. Asante. Bwana Jason Murutu.

**Mr. Jason Murutu:** Asante sana, kwa wakati huu maoni yangu mimi Jason Murisha Murutu tarehe mbili mwezi wa tano 2002.

Katika viti viombavyo vya kisiasa, tungependa mbunge, councillor, ambaye hatimizi malengo ya wale ambao walimuchagua wananchi wapewe nafasi ya kumwondoa katika hali ya kusema kwamba wamekosa imani na yeye. Hii ni kwasababu wabunge wengine wakichaguliwa wanaenda sehemu kama Nairobi, wanajenga vibanda huko wanasahau wale waliwachagua.

Ningependa serikali yetu iwe ya majimbo, iwe na Governor ambaye atasimamia jimbo. Ningependa pia kusema kwamba pesa zote ambazo zinatoka katika mbuga za wanyama, na bandari zipewe asilimia sabini na tano wale watu wanaozunguka mbuga hiyo ama bandari hiyo kwa kusaidia katika maendeleo

Ningependa pia ugawanyaji wa ardhi hasa plot za mjini zisiende kugawanyiwa sehemu kule kwa wakuu wa wilaya. Wazee ambao wamekuwa wakitajwa hapa wapewe nafasi ya kutengeneza.

Nikiingia kwa pointi ya tano. Uzururaji umezungumzwa tungependa hiyo sheria ya Vagrant iendelee. Ningependa kusema kwamba wakati wa uchaguzi, kura zote baada ya kuchaguliwa, saa za kupiga kura zikiisha kura hizo zisihamishwe kwenda kituo kikubwa cha kwenda kuhesabiwa kura hizo. Zihesabiwe pale kwa kituo hicho hicho ili kuondoa tashwishi na mambo baya ambayo huwa yanaendelea yasiyofaa. Pia nikiwa hapo hapo katika uchaguzi, ningependa kusema kwamba ningependa uchaguzi wa urais, uwekwe siku tofauti na ile ya wabunge na pamoja na councillor, ili kuondosha kule kuchanganyikiwa wa watu katika hali ya siku hiyo moja kuchagua rais na kuchagua councillor na kuchagua pia mbunge. Ningependa siku ziwekwe tofauti ya Rais kuchagua kiti ya Rais peke yake, na siku ya Councillor na Mbunge zisiambatanishwe pamoja.

Na pia Katiba ambayo itatengenezwa sasa isiwe na uwezo wa mtu yeyote wa mamlaka ya aina yeyote kuweza kuibadilisha bila referendum ama idhini kutoka kwa walioifanya.

Pia kwa upande wa elimu ningependa kusema kwamba elimu ya msingi iwe lazima na pia ya bure na katiba inayotengenezwa sasa kuwe kuna kipindi kidogo cha mara moja kwa wiki kitakachofundisha watoto wetu mambo ya Katiba yao.

Ningependa pia kusema kwamba yeyote atakayechaguliwa kama raisi, mbunge, atakayepewa wadhifa kama permanent secretaries na wale wengine wafanye ku-declare their wealth, yaani waseme kile walicho nacho na ikiwa katika kipindi ambacho atahudumu ionekane kuna matatizo ambayo amefanya katika hali ya kunyanyasa ama kuchukua mali ya raia, iweze kuwa atanyang'anywa hiyo mali. Ningependa kukomea hapo asanteni.

**Com. Salim:** Asante Bwana Josan Murutu kwa maoni yako, nafikiri, si ni memorandum hiyo au ni maoni kwa mdomo?

**Mr. Jason Murutu:** Ni maoni kwa mdomo.

**Com. Salim:** Haya. Loira Kadege.

**Mr. Loira Kadege:** Kwa majina naitwa Loira Kadege. Nilizaliwa Taveta. Nina maoni machache ingawa mengi yameshazungumzwa lakini katika hali ya kuchangia. swala nilikuwa nataka kusisitiza ni kuhusiana na mahakama. Naonelea ingekuwa vyema kama mahakama ingewekwa iwe huru, ikitengwa kwa serikali na bunge. Na mkuu wa mahakama awe independent, independent kabisa yani mkuu wa sheria asiwe wa kuchaguliwa ama kuwa-picked na rais, iwe ni bunge inaweza kumuidhinisha na pia aadhibiwe kisheria iwapo atakuwa na makosa tofauti tofauti.

Na kuwe na ofisi ya Waziri Mkuu na wizara pia ya sheria. Na kila eneo la bunge liwakilishwe na mzaliwa wa eneo husika na kama haitawezekana hivyo, imekuwa kwamba eneo fulani mbunge aliyetoka hapo si mzaliwa wa eneo hilo. Katika vile viti vya wabunge watakao teuliwa na rais, basi, atokee mbunge atakayetoka katika kabila lile ambalo ama eneo lile ambalo mbunge hakupatikana wa kabila hilo.

Raisi anahitajika kuajibika kisheria iwapo yeye au yeyote katika baraza lake la mawaziri amepatikana na makosa kama vile mtu mwingine. Kwasababu tumeona ufisadi unatokea kuanzia kwa kadhina juu na ufisadi uwe ni kosa la hukumu kubwa, leo kama ni kosa (?).

Raisi awe na muda maalum wa kuhudumu nafikiri hiyo ishazungumziwa na wenzangu. Uteuzi wa rais uidhimishwe kitaifa kwa asilimia itakayo pendekezwa na bunge. Nikisema hapo ni kwamba Rais akishachaguliwa kuwe na asilimia fulani ambayo ni lazima aifikie ndio aweze kuidhinishwa kama rais.

**Com. Salim:** Asilimia ngapi?

**Mr. Loira Kadege:** Ningependekeza asilimia inayozidi hamsini ama hamsini na tano, hamsini hadi hamsini na tano.

Na katika utawala tulikuwa tunaonelea serikali tulikuwa tunataka izingatie ile ahadi iliyo patiana kwanza kwamba (?) hiyo tunataka ipewe kipo ?) na wizara ambayo (?).

Kwa upande wa elimu tunaona serikali imewacha wasomi wengi wanao mashahada wakifanya kazi holela holela na wengine hata hawana kazi. Serikali iwajibike ya kwamba hao watu walipata hio elimu either wamepewa kazi au wametumwa ama wamerahisishiwa njia za kwenda kutafuta kazi nje. Maana tumeona wazazi wanachukua majukumu kama ni kuuza ardhi, mifugo ili wapatie watoto wao elimu halafu baadaye wanakuta serikali haijali wala kuhusika.

Halafu kwa kumalizia tu ni kwamba ningependelea elimu ya kuhusu Katiba irahisishwe katika kiwango vya watu wote kuanzia shule za msingi, hata watu waliokomaa so waanze kujulishwa Katiba ni nini na kuendelea.

**Com. Salim:** Bwana John Njagi. Alfred Milani, yuko? Alexander Deregesu.

**Mr. Alexander Deregesu:** Asante sana, mimi naitwa Alexander Nando Deregesu. Mimi ni Mtaveta na maoni yangu ni kama ifuatavyo.

Kwamba mara kwa mara hizi sehemu za (?) kienyeji zimepuuzwa, na ningeliomba kwamba hii Katiba iweke maanani sehemu za (?) kiasili kama kule Lake Chaga halafu kuna lingine linaitwa Lake Mapruto, Kidong , Mupuni, Kishota Ng'oji, Barakak hizi sehemu ni zile ambazo zilikuwa zinaabudiwa kienyeji. Wenyeji pengine mvua ikikosekana wanaenda kule wanatandika na baada ya kumaliza, mvua inakunja kwa wingi. Wakati huu watu wamechukua kwamba ati dini tu ndio huomba mvua ama chakula au kitu kama hiyo na ndio unaona vitu vingine vinakosekana.Mimi ningelisisitiza kwamba Katiba itambue sehemu kama hizo na sehemu kama hizo zisiuzwe kwa mtu au kundi la watu kwa sababu ni mahali patakatifu pa interpretation yaani kwa kulingana na jamii ya Kitaveta, paheshimiwe na petengwe kwa jamii hiyo.

Lingine ni kwamba Vagrancy Act ningeliomba kwamba irudishwe. Kwa sababu kuna watu wengine ambao wanaweza kuja na kujibanza banza kwenye nyumba ama kuta za nyumba na kama hakuna sheria ya kuweza kumtoa pale basi yeye anabaki pale anagushiwa anafanya uhalifu mwingi. Ningeliomba kwamba Katiba iruhusu kwamba hii Vagrancy Act irudishwe tena.

Ningeliomba pia kwamba Katiba itambue kabila dogo kama Wataveta kwenda bungeni. Na nikisema Wataveta wakati watu wanapochaguliwa kwenda katika bunge, huyo mtu ambaye anachaguliwa na njama atoke katika hii Barita kama ilivyotajwa na mwezangu hapa yaani Wazirai, Nene, Warutu, Wasuya na Wadigiri. Hiyo ndiyo ina-form jamii ya Kitaveta mbali na huyo ambaye anatoka pengine sehemu ingine, kuja kupigania hapa kiti, pengine amekuja kama mfanyi biashara, tunaomba kwamba

hiyo Katiba ikatae.

Mtu kutoka nje asiruhusiwe kwa kuchukua ardhi au kununua ardhi yoyote isipokuwa tu amepitia katika njia ile inayohitajika. Kwa hayo machache asante sana.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana Delengesu, Benjamin Wayo.

**Mr. Benjamin Wayo:** Kwa jina naitwa Benjamin Wayo Sairobi (?)

**Com. Salim:** Benjamin?

**Mr. Benjamin Wayo:** Wayo Sairobi.

**Com. Salim:** Endelea.

**Mr. Benjamin Wayo:** Kwa kuchangia mjadala wa hii maana ya Katiba naomba Katiba iruhusu mzaliwa wa hapa Taveta apiganie kiti cha uwakilishi bungeni.
Lingine la pili naongezea umilikaji wa ardhi utawalwe na wazee wa njama.
Lingine la tatu, shule ziwe za bure.

**Com. Salim:** Inaudible.

**Mr. Benjamin Wayo:** Lingine la nne medical iwe ya bure.
(?) chokora.

Lingine la sita natetea wafanyi kazi wa mikono wanaofanya kazi ngumu. Walipwe malipo ya juu maana kuna unyanyasaji hapa ndani.

**Com. Salim:** Asante Bwana Benjamin Wayo umejitayarisha kabisa kutoa maoni yako wazi wazi. Naona sasa tumuite bwana Gibson Sayeti. Gibson Sayeti, yuko hapa?

**Gibson Sayeti:** Kwa majina naitwa Gibson Sayeti, mkazi wa Taveta.
Nilikuwa naomba kile kifungu cha Vangrancy kirejeshwe kama ilivyokuwa hapo mbeleni.

Mswaada wangu wa pili nilikuwa nikiomba madhehebu yote yaliyosajiriwa hapa nchini yafuatwe kwa utaratibu na kuwe kuna njia au mnyendo wa kuweza kuyachunguza kabla ya kupewa kibali.

Vile vile maofisa wa serikali nilikuwa nikiomba iwe ama kuwe na njia ambazo wanatangaza mali zao katika hadhara.

Vile vile nilikuwa nikiomba kuwe na tume ya ufisadi na tume ya ardhi (?) hayo.

Makabila madogo madogo yaweze kulindwa.

Ufikapo wakati wa uchaguzi ningeomba pia speaker asimamie nchi mpaka pale rais atapatikana ataapishwa.

Serikali ya majimbo nilikuwa naiomba sana.

Mtu anapopatikana na kosa awe na muda maalum wa kuwekwa rumande isiwe ni miaka kumi au mitatu, iwe na muda maalum. Kama ni miezi miwili au ni mwezi moja.

Na makabila yote nchini yawakilishwe bungeni, isiwe kwamba kila mtu anaweza kuwa (?) na kama haiwezekani basi, nominated MPs watoke small tribes, minority.

National language zisiwe mbili kama ilivyo. Na raisi awe na vipindi viwili vya muda wa miaka mitano zikizidi hapo astaafu.

**Com. Salim:** Umemaliza?

**Gibson Sayeti:** Ni hayo machache.

**Com. Salim:** Asante Gibson Sayeti. Bwana Jackline Elijah. Hayuko. Kinga Kivevero.

**Kinga Kivevero:** Kwa majina ni Kinga Kivevero, na ningalipenda kuwasilisha yafuatayo:

Kwanza bunge lisiwe na uwezo wa nkubadilisha Katiba.

Ya pili Katiba iandikwe kwa lugha ya Kingereza

**Com. Salim:** Nani mwenye ruhusa ya kubadilisha Katiba?

**Kinga Kivevero:** Katiba ibadilishwe na raia kama hivi sasa.

Katiba iandikwe kwa lugha mbili, Kingerza, na Kiswahili.

Pili sehemu ya wakilishi bungeni, iwe na mwakilishi mwenyeji, pamoja na madiwani.

Tatu, wananchi wawe na fursa ya kupanga au kutoa maoni ya marupurupu ya wabunge, isiwe kama hivi sasa.

Chama cha upinzani na chama cha utawala katika nchi kipewe ruhusa ya kuteua mawaziri, vice president kinyume na hivi sasa.

**Com. Salim:** (Inaudible)

**Kinga Kivevero:** Wabunge wa upinzani na wabunge wa chama kinachotawala. Wao waweze kuteua wale mawaziri na wale

wengine ili sehemu zote, ziweze kuwakilishwa.

Kuhusu ufisadi, kwa wale ambao wanaouhujumu serikali, ushirika, vyama vya ushirika, waki (?) wafungwe jela miaka kumi au mali yao kunadiwa yote au vyote viwili.

Elimu. Elimu ningalipenda iwe ya bure kuanzia std 1 hadi mpaka 8. kuanzia form 1 mpaka university, kuwe na cost sharing kwa ajili ya chakula.

Kuhusu afya, hii iwe bure, na sheria za afya kusiwen na hizi private hospitals ambazo madawa mingi ya serikali yameingia kule.

Kuhusu mali ya asili, wenyeji wa pale, wazee, wao ndio wanaangalia zile milki za mali asili vyote. Kwa mbuga za porini, asilimia arobaini ya mapato iingie katika karo ya watoto wa eneo lile.

Kuhusu uraia, kusiwe na kabila ambalo origin yake si Kenya, lisipewe kibali. Kwa hivi sasa hio iko wazi. Kwa hivyo origin ya mtu ambaye anapatikana kama Sudan, Somali, Ethiopia, origin yake kule, hapa Kenya asipate ruhusa.

Kuhusu sehemu za makao ambayo yametengwa, public utilities, trustland na zile zozote, zisiwe mikononi mwa county council kama ilivyo sasa. Ziwe kwa wale elders ambao ni sehemu ile kwasababu sehemu zile zinakuwa zinanyakuliwa, wale ma-councillors wamekuwa ni wazembe hawajui zile haki zetu. Asante.

**Com. Salim:** Asante Bwana Kinga. Willy Ngodi. Willy Ngodi, yuko? Ameondoka. Haberi hamisi. Haberi Hamisi, hayuko. Noel Sainewe. Ameondoka. (?) Okewe. Cicilia Waingida. Cicilia Waingida. Paul Mesula. Paul Mesula. Peter Kamate.Peter Kamate. Hayuko. Ametoa eh, Peter Kamate ametoa, okay. Patrick Shodo. Patrick Shodo yuko? Haya karibu.

**Patrick Shodo:** Mimi naitwa Patrick (?) Shodo. Ni mzaliwa taveta na ni Mtaveta. Maoni yangu natoa hivi kulinga na upande wa ardhi. Upande wa ardhi sisi watu wa Taveta tuna shida. Kulingana na population ya watu na ukiangalia vile ardhi inatumiwa kama mimi wakati huu mtu natumia ya baba na ya Kitovu. Nilikuwa naomba kama serikali ingekubaliana ambao wangetukatia ardhi kama hiyo ya national park angalau tupate ardhi ya kutumia. Tulikuwa tunaona ardhi ya national park ni kubwa na sehemu ingine idadi inayotumiwa hapo ni ya waziri na saa ingine watu wamevamia wanalima lima na ingine ni ya (?)

Ya pili kulingana na upande wa shule tuna taabu sana kwa upande wa watoto unaona wengi zaidi wamekuwa machokora kwa sababu ukiangalia wazazi hawajiwezi. Unakuta mtoto anasoma mpaka darasa la kwanza ama la pili unaona mzazi anakosa karo unakuta yule mtoto anakaa nyumbani.

**Com. Salim:** Pendekeza.

**Patrick Shodo:** Pendekezo tupatiwe sera na serikali watoto wasome bure. La tatu.

Com. Salim: **Com. Salim:** (Inaudible)

**Patrick Shodo:** Eeh, primary zaidi, halafu secondary halafu hapo itakuwa cost sharing na (?) waweze kusomesha watoto.

Halafu ya tatu nilikuwa naomba kama serikalin ingekubaliana kufanya majimbo kwasababu, sehemu kama hii yetu hapa Taveta tumekuwa na taabu sana kulingana na viongozi hawa angalii maeneo ya sehemu yao. Sababukama tungekuwa na viongozi hapa wanaosaidia tungekuwa hata sisi wenyewe tumeshafaulu kama wenzetu

**Com. Salim:** (Inaudible)

**Patrick Shodo:** Ya tatu ni upande wa kazi. Serikali naona watu wanachukua retire wengi, na wanafutwa kazi wengi, halafu baadaye tena wanakuja ku (?) kwenye kazi halafu unakuta watu wengine wengi sana wamesoma na wako manyumbani na hawana kazi. (?) serikali ijaribu kuangalia mtu akisha chukua retire akienda nyumbani, ajaribu tena asirudishwe kazini, mwingine naye aandikwe. Yangu ni nhayo.

**Com. Salim:** Asante Bwana Patrick Shodo. Geoffrey Munene hayuko. Siliwoy Saningo. Siliwoy Saningo yuko?

**Siliwoy Saningo:** Kwa jina langu naitwa Sliwoy Saningo.

Nilikuwa nataka serikali iangalie upande wa ipigaji kura nkuchagua kama ni Mbunge. Sasa unakuta kwamba Mbunge anatoka kutoka chama cha KANU. Anapigania hapo, anataka kiti Na kama umeshindwa tayari kwenye chama cha KANU unajitokeza hapo hapo unaingia kwa chama kingine labda ni cha Ford Kenya ama cha DP.

Toa mapendekezo.

Mimi ninapendekeza, mtu yeyote atakayetaka kupigania kiti cha wabunge apiganie kwa pale mahali anatoka apiganie hapo.

La pili nilikuwa natakaupande wa shule. Upande wa shule tulikuwa tunapendekeza kuanzia darasa la kwanza hadi la nane, iwe kwamba tutasaidiwa na serikali. Kufika mbele tutapambana wenyewe.

Halafu jambo lingine, kuna kitu kama maji hapa Taveta. Unakuta kwamba ile maji tunayopata Taveta tayari tunayalipia. Na sio kwamba tunalipa kama ni hao watu wa water supply, kwamba sisi tunawalipa zile pesa za kuleta vile vya vyombo vya kuleta kama pipe ama meter. Basi ukishalipa vitu hivyo tayari maji ishaletwa lakini bado unazidi kulipia maji. Sasa hiyo pia serikali iangalie kwasababu tunashangaa sana na hiyo stakabadhi.

Jambo lingine, hao ma-chief nao hao chief na sub-chief wake hao wanatakikana wapigiwe kura. Kwasababu saa imebidi chief akusaidie tayari unaweza kujibiwa kwamba hata hii ministry (?) siwezi futwa kwa hivyo nikufanyie kazi nisikufanyie salary yangu yaingia kwa hivyo, (?).

**Com. Salim:** Asante Bwana Saningo. Laurent Kilongoro.

**Laurent Kilongoro:** Asante sana Commissioner kwa kunipa nafasi hii. Mimi kwa majina ni Laurent Kilongoro.

Kwenye mchango huu wa Katiba hii mpya ninayo maoni ya kwamba utawala uwe wa majimbo. Na vile vile ningependa utawala ule wao uitambue sana kabila na tamaduni za watu. Kama hasa hapa Taveta sisi tungependelea zaidi habari ya ardhi hapa taveta iwe kwenye upande wa wazee wa njama kwa sababu wao ndio wanajua uchungu wa ardhi na rasilimali zao.

Vile vile kwenye uchaguzi ama viti tofauti tofauti, tungependelea, Mbunge yeyote yule, apitie kwa wazee wa njama. Kwasababu wazee hawa wa njama ndio wanaweza kujua ni nani anayeweza kuongoza mwenye (?) kwa jumla. Na vile vile kwa upande wa viti vingine vya chini kama vile wazee wa mtaa, assistant chiefs, chiefs, hawa watu wachaguliwe na raia kwasababu raia anajua kwamba (?) ana tabia nzuri na watu na yule anayeweza kuongoza vile ambavyo wanataka.

(Inaudible)

Pia kwa upande mwingine hasa kwa hii Taveta, Taveta tuna shida kwasababu tumetengwa, tumetengwa sana ndio unasikia mara kwa mara tunaitwa Wachaga, mara Wapare kwasababu tuko pembeni sana na wenzetu. Ningeomba kwenye huu urekebishaji wa Katiba hii Taveta, ni vyema kama tungepewa nafasi kichochoro moja kwa moja mpaka sehemu zile za Taita hiils ziko mbali na wenzetu kule tutoke kwenye huu (?) tuonekane kama (?).

Kwa upande wa masomo. Tungependelea hii masomo kuanzia hii darasa la kwanza mpaka darasa la nane serikali isomeshe watoto bure ili kwenye kiasi hicho wanaposoma bure wanapofikia kwenye secondary, tutakuwa wazazi wamejiandaa andaa,kwa kusomesha kule mbele.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana Kilongoro. Oliver Longo. Oliver Longo, hayuko? Ameshatoa? Okay. Noel Ndeseria. Noel Ndeseria, hayuko? Yuko? Chuni Jumale. Ametoka? Jackson Ntinyoki. Yuko nje. Jackson, haya. Utatoa maoni? Haya, au

(?). Umeitwa. Haya karibu.

**Jackson Ntinyoki:** Maoni yangu ya kwanza ni kwamba

**Com.Salim:** (Inaudible)

**Jackson Ntinyoki:** Maoni yangu ya kwanza ningeomba upigaji kura, unatakikana, ningeomba iwe wenyeji wa hapa kuanzia bunge, councillor, iwe wenyeji wa hapa, kabila la hapa. Hiyo ndiyo jambo la kwanza.

Pili, maoni yangu ya pili, nngeliomba rais yeyote wa Kenya awe chini ya sheria ili kama ataharibu, atafanya makosa yoyote, aweze kukabiliwa na sheria.

**(Inaudible intejection)**

**Com.Salim:** Jackson amekuja mbio kutoa maoni mawili wazi wazi, asante. Crispus Meta. Ashaenda. Sijui kama ametoa kule maoni yake? Amepeana. Michael Kigati. Michael Kigati, ameondoka. Joseph Mwakio.

**Joseph Mwakio:** Maoni yangu nilikuwa naomba hivi. Mimi ni Joseph Mwakio.

Tunataka njama yetu iregeshwe. Halafu nilikuwa naomba,

**Com.Salim:** Chama gani, njama?

**Joseph Mwakio:** Yaani njama yetu iregeshwe hapa (?). tulikuwa tunataka maoni yangu mimi vile nataka, njama ipewepesa, ipewe bunduki, bastola ndio itakuwa (?).

**(Inaudible interjections)**

**Joseph Mwakio:** Yaani ya kulinda haki za watu. Ukivuka sheria, mwenzangu asivuke sheria (?) eeh.

**(Inaudible interjection)**

**Com.Salim:** Naona Jackson na Joseph wako pamoja. Wanajua la kufanya. Samson Megori. Samson Megori? Ameondoka? Kinoti Ndosi. Kinoti Ndosi, ameenda. Hey, wamechoka? Ama wameenda kama wameshatoa memorandum? Kinia Mnyama. Kinia Mnyama, pia ameondoka. Lauret Mrema. Lauret Mrema, amepeana? Ingawa hapa amesema (?), maoni

ya mdomo tu. Haya. Bengie Wazimoto. Bengie Wazimoto. Jacob Lokireti. Jacob Lokireti? Pia hayuko. Benson Jumamosi. Benson Jumamosi, yuko? Haya.

**Benson Jumamosi:** Kwa majina naitwa Benson Sayeti Jumamosi.
Maoni yangu ya kwanza, ningependa wananchi wawe wanahusishwa katika mikutano ya kutoa maoni wakati wa marekebisho ya Katiba kama hivi sasa.

**Com.Salim:** (Inaudible)

**Benson Jumamosi:** Yaah. Siku zijazo.
**Com.Salim:** Ikiwa kuna mabadiliko ya Katiba?

**Benson Jumamosi:** Ikiwa yatakuwepo basi…
Ya pili ni uraia. Kwa maoni yangu, napenda serikali ama isiruhusu uraia wa nchi mbili. Hii itaweza kuzuia uharifu wa kisiasa au uchumi.

Ya tatu ni serikali za mitaa. Kulingana na maoni yangu, ningependa mabaraza yatengwe na serikali kuu.

Haki za kimsingi. Shule na hospitali ziwe bure. Upande wa shule kuanzia darasa la kwanza hadi la nane. Pia hukumu ya kifo iendelee ili kuadhibu wale wanaofanya maovu ya kinyama. Pia ningependa katika shule za msingi, somo la sheria lianzishwe ili wananchi waweze kujua sheria barabara. Ningependa pia katiba itambue na kuziendeleza rua zote za kienyeji.

Pia ningependa hiki kipengele cha Vagrant kirudishwe ili wale wahalifu wanaohamia sehemu zingine waweze kurudishwa kwao.

Upande wa ardhi. Kulingana na maoni yangu, raia wote ambao si wa Kenya wasipewe haki ya kumiliki ardhi, bali wapewe ruhusa ya kukondesha na baada ya mkataba huu kuisha, ardhi hiyo irudishwe kwa wazee wa sehemu ile ili wenyeji asili wagawiwe.

Katika bunge, ningependa Katiba iweke wazi kwamba kila kabila iwakilishwe bungeni.
Katika serikali ningependa ma-chief na wadogo wao, kwanza wawe ni wenyeji asili, na pia wachaguliwe na raia.

Ya mwisho ningependa Katiba itambue bunge la wazee, yaani wazee wa njama kabila zote.
(?) watambulike kwa Katiba asante.

**Com. Salim:** Asante Benson Jumamosi. Mathias Mukiva.

**Mr. Mathias Sikiva:** Mimi naitwa Mathias Sitiva. Maoni yangu ni kama yafuatavyo.

Katiba ilinde mwananchi mdogo mkubwa. Na Katiba ilinde mali ya maskini.
Rais asiwe juu ya sheria apunguzwe mamlaka. Bunge lisiruhusiwe kupanga sheria ama kurekebisha sheria

**Com. Salim: (**Inaudible)

**Mr. Mathias Sikiva:** Wapewe na wananchi wenyewe kwasababu hiyoo ndio inaleta ufisadi. Wanajipangia mishaara minono minono wenywe na huku wameajiriwa lazima wapewe hiyo nafasi.
Utawala. Utawala vyeo vya juu kuanzia province mpaka district na division, hawa waandikwe na serikali. Lakini, chief na sub-chief wachaguliwe na wananchi.

**Com.Salim:** Asante Bwana Mathias Sikiva kwa maoni yako, sasa namuita Bwana Francis Sekinoi. Hayuko. Muluwe Pololwa (?). Titus Kageai. Sellis Mlamba. Ameondoka. John Saleli Mtawa. Julius N. Juma. Pia ameondoka.Zacharia Kihado. Ameshaondoka. Steven J Munene. Grace Julius. Agnes Ngingara ametoa pia. Violet Mkelemani. Ameshaondoka. Tito Ngingara. Johnson Makundi. Mary Ngurui. Mercy Savini (?). Ameshaenda.Malika Mbayani. Ameshaondoka. Fundi Saleli.Leshampta Mwakio. Ndathi Chalo, Ndithani Mbethe nafikiri ameshatoa, William Mnene (?), Freddie Reuna na Alfred Amal. Freddie, Haya. Freddie Leuna.

**Mr. Fredy Raina:** Kwa jina ni Freddie Reuna na maoni yangu, ningeonelea kwamba Katiba ilinde mali zote za nchi hii. Kwa mfano hapa Taveta tuna ndizi zinatoka hapa nyingi sana. Sasa tukiletewa ndizi zingine huleta hapa inafanya Mkenya hapati faida ya mali yake kwasababu anaumizwa na mali zinazotoka nje ya nchi hii.

Halafu pili, ni rais awe anachaguliwa na wingi wa Wakenya wote apate zaidi ya asilimia hamsini ya kura zote za Wakenya alizopigiwa. Ili kuwe kuna rais aliyechaguliwa na wingi wa watu. Sio kama ilivyo saa hii ni- twenty-five percent kwa five provinces anakuwa rais unakuta amechaguliwa na watu wachache wakati wengi walipinga. Hayo ndiyo maoni yangu.

**Com. Salim:** Asante. Alferd Aman. Fraya Ramadhan. Josphine Ramosha.Florence Philip. Rose Patrick.Kina mama hawa tungependa sana kusikiza maoni yao ilitupate balance kati ya kina mama na ..Constance Mururi. Pia ameenda.Rose Kaba Mugathe. Busara Martin. Rose Mtaura. Linda. Joshua Kaleo. Annes Inde. Robert Mahali. Tengalo Ndao. Tandasi Katuta. Samson Metiaki. Huyo ni observer tu. Ndegesiai Kalu. Maloti Sangeno. John Kareri. Rosemary Nesabulu. Yuko. Nafikiri ameshatoa. (?). Joel Fundi. Karibu.

**Joel Fundi:** Mimi kwa majina naitwa Joel Fundi. Maoni yangu ni kama yafuatavyo Ningeliomba Katiba, napendekeza Katiba kwamba makabila yote ya Kenya madogo kwa makubwa yapewe haki zao sawa. Kwa mfano kama makabila madogo

Wataveta sisi Wataveta ni kabila ndogo na huwa tunaona shida nyingi kutoka kwa makabila makubwa makubwa yaani hii ina maana kwamba, sisi wakati wa uchaguzi either ni mdiwani ama mbunge, huwa tunachezewa mchezo mkali kwasababu ya uchache wetu. Sasa ningelipendekeza kwamba makabila yote yatanguliwe na kila kabila liwakilishwe bungeni.

La pili ningelipendekeza kwamba serikali iwajali sana wafanyikazi wake wadogo kwa wakubwa. Kwa mfano, waajiriwa wa serikali wale wadogo wadogo hupata mishara midogo midogo kana kwamba ukiwaona unafikiri kama ni wafungwa. Ni kama hawajiwezi kwa ujumla. Ningelipendekeza serikali iangalie mishahara yao.

La pili. Kuna hawa walinzi askari. Askari pia ni katika wale wafanyikazi wadogo wadogo.Inaonekena kwamba wakati huu serikali inawalipa hawa wafanyikazi kama askari, pesa dogo. Hawafananishi kun a askari wa mangereza, wa utawala kuna polisi, kuna wajeshi, na wote ni askari. Lakini utakuta wao wanalipwa mishahara tofauti tofauti wakiwa wote ni wafanyikazi wa serikali na ni askari. ningelipendekeza wapewe mishaara sari, ili tupunguze kitu inaitwa kitu kidogo.

Ya tatu ni waajiri .Ningelipenda waajiri pia ufanywe sawa kwa kila kabila. Hasa makabila madogo madogo. Kuna vikosi vingine ambazo ukitafuta makabila madogo madogo kuwezi kuona hata mtu mmoja ameajiriwa kazi kwasababu ya uchache wao ama kuonewa.

Ya nne ningelipendekeza serikali iwe ya majimbo.

Ya tano ningelipendekeza njama ipewe haki zao kamili za kuangalia sehemu yao kama vile kuteua mbunge kuchagua ma-chief na ma- assistant chief na kadhalika .

Ya sita, ningelipendekeza kwamba kuna watu wachochezi huwa wanachochea vita vya kikabila. Watu kama hawa kama serikali itawafuatilia vizuri wawapate na hatia hawa wahukumiwe hukumu ya kifo.

Ya saba ni kuhusu elimu. Mimi ningelipendekeza serikali isimamie elimu ya kuanzia pre-school mpaka darasa la nane. Halafu kuanzia sekondari iwe inalipisha kitu kidogo kidogo ili wale wananchi hawana pesa ama hawana mali waweze kuelimisha watoto wao. Na pia ningelipendeleza elimu ya ngubaru iondolewe kwasababu hatuoni manufaa yake. Ni hayo tu.

**Com Salim:** Asante Bwana Joel Fundi. Jumatatu Shamunge. Jumatatu shamunge. Kazere Mwazia, hayuko.Sifa Barnabas, Sifa Barnabas yuko ? Yuko? Ameondoka. Tuendelee, Peter Mwakio, Mwakio.

**Mr Peter Mwakio:** Kwa majina mimi ni Peter Mwakio mzaliwa Taveta, Mtaveta, napenda nchi yangu na nampenda rais. Mengi yamesemwa lakini pia mimi ningependa kuchangia kidogo. Kuna huu uraibu wa pombe, pombe za Kienyji.Watu ambao hawana pesa wana pesa kidogo wananyimwa haki zao kwasababu pia wao wangependa kunywa pombe. Sasa zile pombe za

kule kwa bar zinauzwa ghali. Sasa mi kwa maoni yangu , ningependekeza kwamba pombe za kienyeji ziruhusiwe lakini kwa kuwa na license ili hata watu wanyonge kwasababu wanajisikia na wao pia wajisikie pia serikali itapata ushuhuru hayo ni yangu. Asante.**(laughter)**

**Com Salim:** Asante Peter kwa maoni yako mafupi na wazi. Constance Mapenzi. Nyomo Mwachila, Sifa Barnabas, ashaondokaka. Ruth Fardinand, Penina Koleta, ametoka. Getrude Samson, ametoa. Mary Leonard, ametoka. Hellen Mshekerua. Okay ameandika hapa. Francis Matano, yuko? Ameondoka. Mary Mukuenina, ametoa. Felista Tumengai, ametoa labda. Nguru Maria Mekewila, Richard Nderegesu ? Cornel Mbayayi.

**Mr. Cornel Mbayayi:** Asante kwa kupata nafasi hii na hii inaonekana kama pengine katika makabila madogo madogo hii ni miaka arobaini kugeuza chapter yao. Maana walikuwa katika hali mbaya hasa Taveta. Hii sisi hapa ni kama tulikuwa na ugonjwa mwingine tofauti na huu tulikuwa tukonao hapa ambao unasumbua watu hii ni system moja ilikuwa imetusumbua sana. Kwa hivyo Katiba hii kuja inaweza kuwa pengine tutaokokea hapo nafikiri, tukikosea hapo basi tumeenda. Mimi langu Katiba ninaomba ijaribu kuangalia hasa hawa wazee hasa njama. Mimi katika umri huu nayo si mdogo sana lakini ninavyoelewa wale wazee tulivyozalika wakati huo na tukiwaona matendo yao ilikuwa ni watu ambayo walikuwa wame tusaidia sana. Hasa pia mambo kama huduma ya jamii, shida ikitokea katika family wale ni watu wanatibu hata nikiwa kama ni mjeuri nyumbani wanaweza niweka ki-family kama ile wazee naweza kunitibu na nitapona ile tabia ninayo. Kwa hivyo ninaomba Katiba ijaribu sana kuangalia hii issue ya hao waze ambao wanaitwa wazee wa njama. Wale pia wanajenga hata miji ya watu ambaye imeharibika baina ya family na family ambaye imeonekana wanavutana haki na haki wale wazee manapo wanapopata haki wale wazee wanajua. Kwa hivyo ningeomba hao watu waangiliwe hasa upande wa wazee, wawe wakipewa hiyo nafasi nafikiri Taveta mambo yote yale tumezungumza hiyo ni ugonjwa ambao tutapona. Kwa hayo machache na mengi hapo namalizia kwa hao wazee.

Pia katika sehemu ingine naongezea katika upande wa mmoja amezungumza kuhusiana na ile clan. Ile maombi ya kila sehemu kama kidoho, chala, wapi wapi nafikiri wametaja sehemu tano, na hizo sehemu tano zina-presentiwa na kila clan hapo na sehemu hizo zote lazima atoke representative wa hiyo clan. Ndio maana zimetajwa tano na hao wazee mbare zao pia ni tano. Kwa hivyo tunaomba iweze kusisitizwa ili tuweze kutibiwa hiyo shida maana tuwagonjwa. Asanteni.

**Com. Salim:** Asante Cornel Mbayayi, Wilfred Mwongotho.

**Mr. Wilfred Kavirondo:** Kwa majina naitwa Wilfred Sizini Kavirondo.
Kwa kuchangia hoja ya Katiba hii ni kwamba nchi yatakiwa itawaliwe na vyama viwili vya kisiasa.

Pili ni kwamba rais atakiwa achaguliwe kupitia asilimia sitini na tano au sabini nchini Kenya nzima.

Tatu, Mkuu wa sheria kwa maoni yangu, ingestahili achaguliwe na bunge.

Nne kwa maoni yangu ningependa utawala wa jimbo.

Tano kwa upande wa serikali ni kwamba serikali ingechukulia mikakati ya kwamba askari akitoka katika police station kwenda kijijini lazima awe na search-warrant.

Tano, miradi ile ambayo serikali inatoa kueneza vijijini inabidi iwe na viongozi wa kuiangalia kama ma engineers. Kwasababu, ile material inayopelekwa pale si zile ambazo za kudumu kama (?) zile za tumika saa hizi (?) na upa saa mbili saa kumi imepasuka. Kwa hiyo serikali itumie kwasababu mwananchi wa kawaida ndiye anaumia.

Sita ni kwamba mbunge achaguliwa akiwa kama mzaliwa wa sehemu hiyo anatoka.

Nane kuanzia chief, sub-chief, hawa wanataka wachaguliwe na raia wenyewe kwasababu ndio wanaojua matatizo yao huko vijijini.

**Com. Salim:** Tafadhali maliza maliza.

**Mr. Wilfred Kavirondo:** Namaliza maliza tu. Kwa upande mwingine wa serikali ni kwamba wakati wameahidi kitu inabidi wafuatilie kwamba mswada umefika Kijijini ambao umetolewa na serikali kuhakikisha umetimizwa au la. Kwa sababu hiyo inasababisha saa zingine watu kuvutana au mambo ya ukabila kutokea. Asante.

**Com. Salim:** Jacob Mwaiba. Jacob yuko? Ametoa. Peter Ngaluma hayuko. Lesabulu Kigati, hayuko. Simeon Siniando, karibu.

**Mr. Simeon Samiji:** Mimi kwa majina naitwa Simeon Samiji Siniando Nene. Ni mzaliwa wa Taveta na kisha ni mzee wa njama. Maoni yangu maoni ni mengi sana kuhusu njama lakini kitu naongeza kwa maoni yangu nikiwa na wazee wa njama wenzangu maoni yangu ni kwamba njama ipatiwe (inaudible) wa kumiliki ardhi na mashamba pia wawe wakiskiza kama zamani. Pia kesi ya kinyumbani kuna ingine ambacho (inaudible)

**Com. Salim:** Asante Bwana Simeon kwa maoni yako (inaudible).

**Mr. Nahashon Mukunde:** Asante sana Ma-commissioner, mimi naitwa Nahashon Mukunde, mzaliwa wa hapa mwenyeji Taveta. Kwanza, napenda kuunga mkono kwa dhati yale yoteambayo yametolewa na wenzangu kuhusu kwanza muundo wa serikali, umilikaji wa mashamba, uchaguzi, kwamba atakaye chaguliwa awe ni wa hapa hapa, mzaliwa wa hapa hapa. Na apitie, aidhinishwe rasmi na baraza la njama council of elders kama ilivyokuwa huko mbeleni tukipata uhuru kwasababu hata wakoloni

wenyewe walitambua njama, council of elders ndio kwasababu kwa kuteua mbunge wa kwanza aliyekuwa akiwakilisha Coast alitoka hapa Taveta. Mzee Jeremia na alipata approval kutoka Njama Council of elders. Lakini baada ya Uhuru kupatika heshima hiyo iliwekwa kwenye gunia. Tunaomba heshima hiyo ya Council of elders irudi si kwa Wataveta tu. Irudi kwa Kenya nzima. Tunajua kila jamii ina council of Elders wao kwa mfano Meru wana njuri njeke, Wagiriama wana kaya, Wataita wana eni mwana na wengine hata nafikiri Wakamba wanazo. Kwa hivyo hawa council of Elders, Katiba ijayo iwarudishie mamlaka maanake tuliona mfano juzi wakati wa tribal clashes watu walioenda ku-control tribal clashes country wide ni council of Elders, kwa hivyo tunaomba Katiba ijayo, haya mabaraza ya Jamii yapewe uwezo kikatiba. Hivi sasa wana function kwasababu President aliyoko sasa anayatambua, yamekuwa yakimsaidia sana kuleta amani. Je kesho, kama tutapata President ambaye hatatambua council of elders tutatokota. Kwa hivyo kwa heshima na taadhima naomba hili (?).

**Com. Salim:** (Inaudible.)

**Mr. Nahashon Mukunde:** Ndio! Ndio! Lakini naomba kidogo (?) kwani kutoka saa nne niko hapa. Eh pili, nakuja kuingia kwa uchumi. Ndugu Ma-Commissioner, kuna kitu nimeona kimesahauliwa na wenzangu sana. Kwamba, tumetoka mbali lakini hatuangalii tatizo linalotukabili kiuchumi. Chombo kikuu cha uchumi nchini Kenya, Kenya Revenue Authority, hatujazungumzia Kikatiba huyo anayesimamia hicho chombo. Kwa nini anatolewa kila siku na kuwekwa mtu mwengine. Katiba ijayo, impe uwezo, kama anafanya kazi nzuri aweze kuishikilia ofisi ile vilivyo. Pasije kuwa hiki kinachoendelea, ameguza pasipoguzika atolewe kwasababu ame-tax mapenzi ya kigogo, anatolewa anawekwa mwengine wakati mwananchi ndio anayeumia. Kwa hivyo jambo hilo liangaliwe na Katiba ijayo. Napendekeza kwamba KRA, Kenya Police Commissioner na Director of CID, hawa watu wapewe security of tenure na vote ya wabunge vile watakavyoona ifaavyo. Ni watu wazuri lakini wanashindwa kufanya kazi yao vilivyo kwasababu ya kuogopa untouchables, wasiogusika, vigogo.

**Com Salim:** Nafikiri kwa (?).

**Mr. Nahashon Mukunde:** Atachunguzwa!

**Com. Salim:** (?) nimwondoe?

**Mr. Nahashon Mukunde:** Atachunguzwa na baraza na kamiti inayohusika katika Bunge. Katika Bunge tuna kamiti zote hizo kama vile KRA vote ultimatum, kuna kamiti ya uchumi itamchunguza na ipendekeze (?). Hakuna ambaye yuko yuko aove the law. Ningeomba kusema mengi lakini naona sasa. Kwa ujumla, na ndugu zangu wote waliotoa maoni yao (?).

**Com. Salim:** Asante sana Bwana Nahashon Mukunde kwa maoni yako. Sasa namwita Bw. John Mtuta, Karibu. John Mututa Muruti.

**Mr. John Mututa:** Commissioners, mchango wangu kwa leo ni kama ifuatayo.

Kwa mambo ya mbunge ama wabunge. Kwasababu nyingi ambazo zimeelezwa hapa mwanzo, kuna haja kwamba kila kabila liweko bungeni. Tunataka kusikia sauti ya Mtaveta bungeni, tunataka Katiba ihakikishe ya kwamba sauti ya Ogiek iko bungeni, hata Katiba ihahakikishe kwamba sauti ya (?) pia iko bungeni. Makabila madogo yote yawekwe kule ili yachanganyike na yale makubwa manake hiyo ndiyo Kenya.

Mambo ya ardhi Makamishna, katika Taveta hii kuna watu watatu ambao wana asilimia tisini ya ardhi ya Wataveta. Nitawataja lakini si lazima muwaandike. Basil Criticos, Muhoho na National Park, wana over 90% asilimia tisaini ya ardhi ya Wataveta. Napendekeza kwamba katika Katiba inayokuja, yeyote yule ambaye atakuwa na asilimia inayozidi kumi lazima aje aomba wenye ile sehemu, maanake katika Kenya hii hakuna ardhi ambayo haina mwenyewe. Tuombwe, tuambiwe kwamba tunataka kufanya hili sehemu iwe National park. Tuelezwe manufaa yake, tukubali kama yatatufaa, tukatae kama hapatatufaa.

Maji pia ni rasilimali ya nchi na kuna kaburu moja alikuwa hapa, maji yametoka mtoni basi akawanyima wengine wasipeleke kwenye mashamba yao. Tunasema ya kwamba hiyo ni dhambi hata mbele ya Mungu. Maji ni rasilimali ya nchi na Katiba inayokuja iwe na vifungu ambavyo vitahakikisha kwamba kama kuna mtu lazima atumie maji ya mto sio yeye mwenyewe kwenda kufunga ule mto, lazima pia aje kwa wananchi awaambie kwamba kuna haya maji anataka kuyatumia kwa njia fulani wakubali ikiwa wataona haya ni manufaa ama kama hawayaoini, wakatae. Rais (?) asilimia hamsini na moja kwa duru moja basi kura zirudiwe hata kama ni mara mbili mpaka apatikane yule ambaye amechaguliwa na Wakenya wengi.

Napendekeza kwamba Katiba inayokuja pia iweke kifungu kinachosema kwamba mawaziri, mabalozi, maafisa wakuu wa serikali na mahakimu wachaguliwe na bunge. Hiyo itamaliza ufisadi. Ya sita bunge, wabunge pekee yao hawana ruhusa ya kubadilisha Katiba, warudi kwa wananchi.

Elimu na afya ni msingi wa nchi, ziwe bure, elimu mpaka chuo kikuu. Wataalamu wa nchi wanapatikana katika vyuo vikuu. Kule pia elimu iwe bure ili yule ambaye asiyejiweza awe na nafasi ya watoto wake kufika chuo kikuu. Katiba ifundishwe shuleni kuanzia shule za msingi. Na kwa kumalizia Katiba ilinde mila na tabia za makabila yote, makubwa kwa madogo. Asanteni sana.

**Com. Salim**: Asante Bwana John Mututa Murutu kwa maoni yako na memorandum yako. Na sasa ni Mariamu Nikaroya, ameenda. Daudi Luko, Masubuko, Edward Singia, ameenda. Samahani wengi wamekaa sana. Lakini kama muonavyo wenye kutoa maoni ni wengi. Mgoyazi Shauri, Mkamba Mbelanyi. Alfred Ng'ela Maganga, Irene Nginai,Uzindiliwe Nginai, Mayamu Mkonyozi, Mike Burton, Kolokolo Sowene. Yuko?

**Mr. Kolokolo Sowene:** Kwa majina naitwa Lologwa Kolokolo Sowene. Mimi ni mzalendo wa Taveta. Nimekuja hapa kuchangia Katiba mpya ya Kenya.

La kwanza mengi yameshazungumzwa lakini nitagusia gusia tu kidogo kwasababu yalikuwako mojawapo ya mchango wangu na mimi. Mali ya asili, natural resources. Katika Katiba mpya ambayo hii inayotengenezwa sasa na wananchi, sisi tungeomba eti kwamba Katiba mpya itakayotengenezwa, mali ambayo inaitwa kama madini, mito, maziwa national parks yawe chini ya serikali za mitaa. Hapo hapo (?) ni kwamba nitatoa mfano mmoja ambao hauwezi kuimarisha Kenya jinsi inavyokwenda tunaambiwa kwamba tuzuie mazingara na hali tunapotambua kwamba maji ndio uhai na kwetu yamewekwa katika kiwango cha miji mikuu , tungependa hivi, maji yale yanayotoka katika Njoro spring water, yawe katika rates za flat rates kwa wananchi wa Taveta, kusudi waweze kufurahia mali ya asili ambayo waliopewa na Mwenyezi Mungu.

Pia tungeomba kwamba ama tunataka kwamba katika Katiba mpya, National park iwe vile vile chini ya mamlaka ya serikali za mitaa. Kama ni serikali kuu iweze kupata robo katika mapato yale ambayo yatakayo kusanywa kupitia utalii, ama wanyama wa mbuga,vile vile na madini yaliyoko.

Ya pili tungependa serikali kuu iwe mbali na serikali za mitaa. Sababu tunapo, au wananchi wanapochagua kiongozi tuseme kwa mfano diwani wanapopitiza budget yao, pesa tunayo lakini ile njia ambayo inayotumika katika hali ku ya kuweza kupitisha miradi ile ambayo tulipitisha inachukua muda mrefu sana. Kwasababu budget inatoka Taveta town council iende Mombasa kwa P.L.G.O, itoke Mombasa iingie Nairobi kwa P.S, itoke kwa P.S ndio iingie tena kwa waziri. Sasa Kenya nzima, waziri ni mmoja wa local government ambapo anategemewa na mabaraza yote ya Kenya. Kwa hivyo tungeomba hivi, mamlaka yagawanywe yawe katika kiwango cha mikoa. Sababu yanapofika katika serikali kuu huchukua muda mrefu ambapo (?).

Bunge tungependa iwe katika lugha ya taifa ya Kiswahili ili na wazazi wetu manyumbani wanapofungua radio zao waweze kujua kwamba Bunge limezungugumza nini leo.

Shule: Shule tungependa katika Katiba hii inayotengenezwa sasa, ziwe za bure kuanzia za msingi hadi University. Kama ikishindikana katika kiwango cha university basi turudie mtindo ule ule tu watoto wapewe loan ili waweze kusoma lakini isiwe na interest yeyote.

**Com. Salim:** Uko karibu kumaliza?

**Mr. Kolokolo Sowene:** Namaliza nikisema walemavu. Walemavu katika Katiba hii ambayo inayotengezwa hivi Sasa tungeomba vile vile kwamba watoto wao wanapofanya mitihani nakupita kuanzia darasa la msingi, sekondari hadi university wasomeshwe bure.
La mwisho,wao wenyewe vile vile serikali ichukuwe jukumu la kuweza…

Kwamba tunapofika miaka kumi na minane, tumehitimu kuwa mali ya serikali.Tunaomba vijana wote wavulana kwa wasichana

wawekewe kiwango cha mashamba yanayokadiria hekari ishirini kulinda maisha yao. Asante.

**Com. Salim:** Asante sana. Tukiendelea mbele tumwite, Mariam Mburia, Mariam Mburia, Yuko? Lewanga Mgude, yuko? Hayuko? Sorry. Mary Nangondo, Sera Luwira, George Chikira, Sijaro Taliani. Wote hawako eh? Mfumwa Mwangumba.

**Mr. Mfumwa Mwangumba:** Nashukuru sana Makamishina. Yangu yalikuwa ni machache ingawa mengi yameshazungumuzwa. La kwanza ambalo ningeomba ni kwamba wagombea viti wanaotoka kutoka vyama vyao, ningeomba kwamba wasiruhusiwe kuingia kwa vyama vingine mpaka wamalize muda wa mwaka mmoja.

La pili ni kwamba, haya maeneo ya udiwani ambayo yanagawanywa bila wale wananchi wa lile eneo kujua. Tungeomba pia wale wananchi wa pale wahusishwe katika kugawanya yale maeneo ya udiwani.

La tatu ni kwamba, ma-mayor na wenyeviti, wachaguliwe moja kwa moja na wananchi .
La nne ni kwamba kamati ya kusikiza makesi ya mashamba, mahali kama hapa Taveta, ningeomba wachaguliwe na wazee wa njama ambao wanaojua mila na desturi za hili kabila lao. Kwa hayo machache mimi naunga mkono haya yaliyopendekezwa kuhusu wazee wa njama na wale wengine.

**Com. Salim:** Asante Bwana Mwangumba. Deris Nguyao, Godfrey Mwaroro. Yuko okey.

**Mr. Godfrey Mwaroro:** Majina yangu ni Godfrey Mwaroro.
Hoja yangu ya kwanza ni kwamba Bunge liwakilishwe na makabila yote.
Pili, ma-chief wawe wakipiwa kura kama vile wabunge.
Tatu, wananchi wawe na haki ya kumregesha nyumbani mbunge ambaye hafanyi lolote bungeni.
Nne, mishahara ya wabunge ipunguzwe.
Tano, Mgombea kiti cha ubunge akikosa kuteuliwa asikubaliwe kuhama chama na kuingia chama kingine bali angojee mpaka kipindi kingine.
Sita tuwe na viti vilivyotengwa kwa makundi maalumu, makundi hayo yawe ni yale ambayo yamezidiwa na makundi makubwa.
Saba Vagrant Act irudishwe. Nane Katiba izingatie mila na desturi. Asante nimemaliza.

**Com. Salim:** Asante bwana Godfrey Mwaroro. Na sasa namwita Fadhili Charo.

**Mr. Fadhili Charo**: Mimi kwa majina naitwa Fadhili (?) Charo. Mimi kwa maoni yangu ni Katiba. Ningeonelea kwamba itungwe kwamba Rais pale juu asiwe na mamlaka juu ya kifungo cha sheria (?). Lazima Rais awe chini ya Sheria si haki yeye awe juu ya sheria.

Pia kwa huyu anayeitwa Mkuu wa sheria asiwekwe, atoke kabisa, pasiwe na Mkuu wa sheria.
Nikiendelea ni kwamba hii Katiba ya sasa ambayo tunaitunga ijaribu sana kujali masilahi ya wanyonge. Budget siku ya mwanzo ilikuwa ikisomwa kushuka saa hii budget inasomwa ikipanda na hali ya uchumi ndiyo hii imezorota. Ijali pia hali ya wanyonge budget ya (?)

Katiba ya sasa ningeonelea ipinge huu mtindo wa mtu kwenda kuweka hazina kwa nchi ya nje. Huu mpango wa mtu tajiri fulani kuondoa pesa na kwenda kuhifadhi katia accounts za nchi za nje hiyo kitu ikome. Kama ni kuhifadhi waziri wa hapa nchini na kama ni ma-industries wafungue ili watu walioko nchini hapa wapate ajira.

Ya mwisho ningeonelea kwamba kwa maoni yangu, papitishwe sheria ya ku-deal na hawa wafisadi ambao unakuta mtu ameandikwa kazi ukienda kwa ofisi unakuta ni koti inafanya kazi mtu hayupo. Ama ikiwa ni hakimu ameshafika muda wa ku-retire au mtu amefikia muda wa ku-retire, bado anaingizwa tena kazini ilhali kuna watu wengine ambao hawana kazi.Mtu aki-retire atoke moja kwa moja si wa-retire na arudishwe tena kuajiriwa. Yangu ni hayo.

**Com. Salim:** Asante Bwana Fadhili Charo kwa maoni yako. Reverend HarrisonShikuku,ameondoka, Halowis Wawae, (?) Peter, hayuko, Mzee Solomon.

**Mr. Solomon:** Asante sana Makamishna. Kwa majina naitwa Mzee Solomon. Napenda kuchangia sana juu ya Katiba yetu ya Kenya wakati huu maana ile ingine ikiundwa au ikiumbwa nilikuwa nami bado sijaumbwa. Sana sana ni ningerudia tu kwa upande wa elimu, nilikuwa napendekeza, kwa maoni yangu, elimu ya msingi, kuanzia darasa la kwanza hadi la nane iwe ya bure. Halafu kuanzia form one, mpaka form four, ichangiwe na wazazi. Halafu kuanzia university, ichangiwe na serikali kwa kupewa mikopo kwani ndiyo itasaidia mwanafunzi yule ama kijana yule kupata kazi maanake sasa hivi.

**Com. Salim:** Hakuna haja ya kueleza.

**Mr. Solomon:** Juu ya hospitali, nafikiri nchi yetu ilipopata uhuru kulingana na historia ilituambia kwamba itakimbizana na magonjwa.

**Com. Salim:** Pendekezo.

**Mr. Solomon:** Sasa, hospitali ziwe bure.

**Com. Salim:** Ukiendelea…!

**Mr. Solomon:** Nikiendelea, juu ya wageni. Wageni sio kutoka nchi jirani kwasababu hata Wakenya unakuta mtu anatoka

huko kwao ameharibu anakuja hapa kazi ni kuzurura. Mtu yule amestahili ashikwe na ahukumiwe na arudishwe kwao, vagrant. Hiyo sheria naona, niliiona nikiwa mdogo lakini sasa hii...

Juu ya ardhi. Maeneo unakuta mtu ni mgeni katika eneo hili ana zaidi ya heka ishirini. Sijui aliipaa vipi.

**Com. Salim:** Pendekezo.

**Mr. Solomon:** Watu hawa wasiwe na zaidi ya heka moja, akiwa ni mgeni.

**Com Salim: (**Inaudible)

**Mzee Solomon:** Wasiwe na zaidi ya heka moja. Hapa Taveta.

**Com. Salim:** Na kwingineko.

**Mzee Solomon:** Huko kwingine sijui maanake inategemea na jinsi wanavyoishi wao.

**Com. Salim:** Kenya yote?

**Mzee Solomon:** Kenya yote sawa. Lingine ni mali ya asili. Mali ya asili tunayo kama vile maji, misitu, hifadhi ya wanyama wa pori, hivyo vitu hatuvioni faida yake. Sasa tulikuwa tunaomba katiba irudishwe chini ya local government pengine itatusaidia zaidi.

Ingine ni kuhusu mamlaka ya kisiasa kama bunge, udiwani na urais. Nilikuwa napendekeza kwamba rais achaguliwe na asilimia hamsini katika mikoa mitano, zaidi ya yote irudiwe. Tujue upendo wa watu na yule rais atakayechaguliwa.

Ingine ni kutokuwa na imani na mjumbe yule ambaye tumemtuma huko.Turuhusiwe atakapofanya makosa tukimkataa tukisema ndio arudi nyumbani.

Lingine ni mshahara wa madiwani.

**Com. Salim:** Maliza, maliza.

**Mr. Solomon:** Sawa, lingine ni mshahara wa madiwani. Huyu diwani ni mtu tuko naye karibu sana kwa muda mrefu na kisha unakuta mshahara wake ni wa kunyanyasika. Kwa hivyo aangaliwe.

**Com. Salim:** (Inaudible)

**Mr. Solomon:** Apate juu kidogo. Upande wa bunge ningependekeza kwamba kuwe na uwakilishi bungeni kwa makabila madogo yote ndani ya bunge la Kenya. Nikimalizia napenda kusema, ningependekeza serikali ya majimbo. Tupate huduma kwa karibu. Zaidi ya yote asanteni.

**Com. Salim:** Asante Mzee Solomon. Alhamisi Meja, yuko?

**Mr. Alhamisi Meja.** Kwa majina naitwa Alhamisi Meja. Naichangia kwa Katiba ya kwamba kuhusu ugomaji wa kazi kwa serikali. Mtu yeyote atakayegoma kazi ashtakiwe na afungwe miaka miwili na kisha aachishwe kazi. Kwasababu anatatiza serikali. Nikichangia tena kuhusu elimu ya bure kuanzia standard one mpaka la nane iwe bure. Huko sekondari, wazazi watachangia, na university iweze kuwapatia mikopo wazazi wale wanyonge, hata wale ambao si wanyonge.Kenya nzima.

Swala la tatu, ni kuhusu hospitali, ziwe bure.

Ya nne, ni kuhusu watu wa maji. Unakuta mtu ananunua mita. Halafu akinunua hii mita, kisha huyu mtu wa maji huyo huyo umenunulia, anaikata anaichukua na wewe ndiyo umeshainunua.Sasa hiyo sheria inatatiza wananchi. Yangu ni hayo tu.

**Com. Salim:** Asante Bwana Alhamisi Meja. Sasa tuna nusu saa tu iliyo bakia kabla ya kufunga kwa leo. Kesho tutakuwa hapa pia kwa hivyo sijui ni wangapi waliojiandikisha na ambao hawajatoa maoni?

**Com. Salim:** Kumi na tatu? Dakika moja moja tu, sawa. Samahani tungependa sana ku, lakini wakati hauko na sisi. Ngoja nimwite mtu kwa jina lake Ndalingoi Mashine, ameenda. Kenyatta Albert, ameenda.

**Crowd:** Ndiyo huyu.

**Com. Salim:** Yuko? Alright.

**Mr. Albert Kenyatta:** Maoni yangu ni kama yafuatayo.
Kitambulisho: Mkenya anapofikisha umri wa miaka kumi na nane na sababu ana haki ya kupewa kitambulisho hiyo ni haki pia apewe na passport akihitaji.
Ardhi, Mkenya yeyote anapofikisha umri wa miaka kumi na nane na hana shughuli ingine yeyote anaweza patiwa (?) akaitumia kwa miradi yake mwenyewe.
Mazingira, ziwe sheria kuwa kuwe na (?) mazingira kenya na watu wa serikali watoe miti watu wapande.
Maji, maji ya mito, chemichemi na maziwa, Wakenya waruhusiwe kuyatumia kwa kunyunyuzia mashamba yao na mahitaji mengine.

Mikopo kwa vijana.Vijana ambao hawana ajira ili waweze kujisaidia baadaye, inatakikana serikali iwatengee mfuko wao wakuwasaidia kwa mikopo midogo midogo.
Serikali isizuie wanawake kutahiriwa, (?).
Uchaguzi, Katiba ya nchi itoe tarehe kamili ya uchaguzi. Kura ziandikishwe mfululizo mwaka mzima.

**Com. Salim:** (Inaudible.)

**Mr. Albert Kenyatta:** Nifikishe pale? Haya.

**Com. Salim:** Jacob Nesili, hayuko.Josiah Luwolo, hayuko. Mkanirondo Sanitai, hayuko. Samuel (?), hayuko. Godfrey Jumamosi, hayuko. Regina Ngaa hayuko? Jackline Shodo, hayuko. Pauline Moyaka, hayuko. Sophia Mwanyalo, hayuko. Violet Ngutu, Samuel Ngui, Saidi Maingo, ashatoa,Constance Enock, Karibu. Dakika moja tu samahani.

**Constance Enock:** Naitwa Constance Enock. Naomba Katiba iangilie pande za watoto wetu wote duniani. Kwasababu, watoto wanapotiwa mimba na wanaachwa hapo hapo na shida zao zote.

**Com. Salim:** Pendekezo lako ni nini?

**Constance Enock:** Tunataka Katiba iangalie iwape adhabu kwa kuwa wawalishe wale wa (?) yule ambaye amemzaa yule mtoto amlishe na amsomeshe skuli. Kama zamani, zamani ilikuwa hivyo, ukiweka mtoto wa mtu mimba unahaki ya kumsomesha yule mtoto skulini.

**(Interjection Inaudible)**

**Mama Kitundulu:** (In Taveta dialect, through translator)

**Translator:** Mama anasema hiyo katiba ijaribu kwamba wazee wale wa njama wapewe mamlaka waliokuwa nayo tangu jadi ili waweze kufundisha hao watoto waweze (?).

**Mama Kitundulu:**

**Translator:** Wazazi waweke watoto wafike jandoni. Yani wawatahiri watoto wa kike ili wawe na heshima nzuri.

**Mama Kitundulu:**

**Translator:** Kama mtu anataka kugombea ubunge, lazima aidhinishwe na wazee wa njama.

**Mama Kitundulu:**

**Translator:** Hata kama ni chief pia, aidhinishwe na wazee wa njama.

**Mama Kitundulu:**

**Translator:** Hata madiwani pia wakitaka kugombea kiti hicho lazima waidhinishwe na wazee wa njama. Katiba ikizingatia mambo hayo, nchi (?) itajengeka.

**Com. Salim:** Asante sana. Samahani Mama ungekaa pale, samahani kidogo kuna Swala mwenzangu ataka kukuuliza.

**Com. Ratanya:** Ningetaka kumuuliza huyu mama Kitundulu, unaitwa Kitundulu ningetaka kumuuliza kama angekubali kina mama nao wachaguliwe wawe wanachama wa njama?

**Mama Kitundulu:**

**Translator:** Anasema hapana mwanamke hawezi kuwa mwana njama.

**Mama Kitundulu:**

**Translator:** Kina mama wanatosheka kina baba peke yao wakiwa kwa hiyo njama.

**Com. Salim:** Asante Mama, Asante sana. Vincent Melanyi, hayuko? John (?), hayuko. Gregon Sawerere, Andrea Mrugi, Okoyi Fundi, Lesareo Melanga, Sembu Jacob, Lesarae Sembu.

**Mr. Lesarae Sembu:** Katika majina yangu naitwa Lesarae Sembu, ambaye ni mzaliwa wa Taveta, nimezaliwa hapa Taveta, nimekuwa hapa Taveta. Katika maoni ya Katiba ningeomba Katiba isimamie katika mashamba kila mtaveta apate naye title deed ya kumiliki shamba.

La pili shule iwe ya bure kuanzia standard one mpaka la Nane.

La tatu, hospitali nayo iwe ya bure na clinic zikifungwa kwasababu ndizo zinasababisha hospitali kuuza madawa.

La tano. Mbunge achaguliwe na wazee wa njama na akiwa kama ni Mtaveta kama ni mtaveta awe ni Mtaveta pale pale anayesimamia, kama ni Mkamba asimamie Ukambani, kama ni Mgiriama asimamie Giriama, ili nayo makabila madogo yapate

nafasi katika bunge. Ni hayo tu.

**Com. Salim:** Asante sana. Jakok Ligayo, Mkota Miyale, Jacob (?), Joseph

**Mr John Sayeti:** Kwa majina naitwa John Sayetu. Serikali ningependekeza iwe ya majimbo tupewe wilaya yetu kama Taveta.

Bunge, mwenyeji au mzaliwa wa Taveta awe akiruhusiwa kupigania kiti tu. Bunge liwe live yaani liwe likisikika katika redio na televisheni live.

Serikali za mtaa. Ma-chief, Mayor na wenye viti wachaguliwe na raia.

Ardhi imilikiwe na jamii inapopatikana na kusiwe na sheria ya kuwa Mkenya ana haki ya Kumiliki ardhi mahali popote. Ardhi iwe ya wenyeji pekee.

Katiba ihakikishe kuwa sheria za njama zimeshehenewa katika Katiba hii mpya.
Lugha za kienyeji zifunzwe mashuleni mpaka darasa la tatu.

Sheria za Kenya zifunzwe mashuleni na kila mahali. Sheria ziwe katika vitabu ambavyo vinapeanwa bure na zitafsiriwe katika lugha zote za kienyeji.
Vitambulisho vipeanwe kwa Wakenya wanaoa mabibi kutoka nchi za nje tuseme kama Tanzania hapa jirani baada ya kuzaa naye watoto wawili.

Ajira. Ajira za kiserikali inatakikana tutumie quota system.
Education: vyuo vikuu viwe katika kila jimbo na kila wilaya iweze kuwakilishwa vyema. Wafanyi kazi wa serikali watangaze Mali yao hadharani. Asanteni.

**Com. Salim:** Asante John Msayeti kwa maoni yako. Bernard Muria, hayuko. Thomas Makange, hayuko, Zebedeyo Ndini, amepeana, Timothy Kurwa, hayuko,Lucas Kyelelo, John Nene, Skeva Melaji, hayuko, Mburia Mwasi, Peter Masulia, hayuko, Nethan Taraya, Daniel Kidodi, Samuel Ngeresani.

**Mr. Samuel Ngeresani:** Maoni yangu ni kama ifuatayo. Rais wa Jamhuri ya Kenya awe chini ya sheria za nchi. Hii itamnyima nguvu za kufanya maovu atakayo yeye. Kwa hivyo atafanya kulingana na sheria za nchi.

Pili kuwe na serikali ya majimbo.
Tatu, viongozi kama vile mbunge au diwani awe wa kabila lile ambalo anawakilisha watu wake katika bunge.

Nne. Rasilimali kama vile, mbuga za wanyama, migodi ya mawe na kadhalika iwanufaishe wakazi wa sehsmu hiyo angalau kwa asilimia hamsini.
Tano. Elimu hasa ya msingi iwe bure na pia syllabus ifanyiwe marekebisho hasa masomo yapunguzwe na vile vile pia walimu walindwe kwa kupewa mishahara mizuri.

Sita, askari wazuiliwe kuingia vijijini ovyo kwani huongeza ufisadi zaidi.Wakifanya hivyo wawe na sababu muhimu na ikiwezekana wawe na afisa mkubwa.Ni hayo machache.

**Com. Salim:** Asante Samuel Ngeresani, Joseph Jumapili, Josephine Sauka, Constance Othiano, Jackson Jarija, Florence Munyao,Lowin Kidongu, wamebakia nani na nani? Eh, hatutaweza kumaliza.
Tumepewa advice kwamba tu (?) lazima tuondoke tuwe njiani kuelekea Voi haraka kwa ajili ya kutembea usiku si....Tungependa sana kuwasikiza lakini tunaweza kuwapa nafasi ya kwanza kesho, mimi nafikiri itabidi tumalize sasa maana wakati

**(Interjections inaudible)**

**Com. Salim:** Haya, niletee tumpe nafasi, nyote mumekubali. Na hao wengine Mngojee mpaka kesho. Sawa mumekubali.

**Response:** Sawa.

**Com. Salim:** Haya karibu. Tafadhali ututaje majina asante.

**Mr. Stephen Kubo:** Jina langu ni Stephen Kubo Mazige.

**Com. Salim:** Stephen Kubo Mazige?

**Mr. Stephen Kubo:** Nitajaribu kutorudia mambo yaliyosemwa. Naunga serikali ya majimbo mkono. Tuwe na rais wa taifa la Kenya ambaye anaangalia mambo ya ulinzi na mambo ya nchi za nje. Lakini kila jimbo, liwe na waziri mkuu ambaye atachaguliwa na wenyewe, wenyeji. Na katika ngazi ya taifa tuwe na mabunge mbili ile tunaita lower house ambayo ni parliament (?) kwa wakati huu na ingine inaitwa Senate.

Senate ichaguliwe kulingana na makabila. Kwa mfano, katika Taita Taveta District, tuwe na viti vya Wataveta, cha Wasagala, Cha Wataita, viti tano. Kama ni Ukambani, tuwe na vile vya wanaoshikana, vitano hivi kulingana na makabila. Senate iwe ni ya makabila na hiyo ni kwa ngazi ya taifa.

Tukija kwa jimbo tutakuwa vile vile na Wabunge katika hiyo Jimbo na wabunge hao itategemea ukabila. Kila kabila kama ni hapa Taveta huwezi kwenda jimbo la Pwani na lazima tutambue kwamba makabila yana haki ya kuheshimiwa jambo hilo mimi nimekubali kwa dhati kwasababu lazima tutambue kila kabila na kila (?) kina mila zake na haki zake. Lakini ile inaitwa parliament, lower house, ikae kulingana na wananchi wote walio hapo wawakilishwe. Kwa hivyo, senate, kabila, ile inaitwa regional assembly au majimbo, kabila. Na councillors watakuwa vile vile (?).

Nitaongeza tu nikimaliza kwamba, ile inaitwa preamble kitangulizi, ikisema ya kwamba Katiba ya Kenya utangulizi wake ni kwamba Mkenya yeyote asibaguliwe kutegemea kabila,
au rangi au dini, au sex, jinsia au social status. Mkenya yeyote asibaguliwe (?). Kila Mkenya ana ruhusa ya kwenda kuishi katika jimbo lolote na apewe haki. Wale wa jimbo hilo ambao watatangulia waone wamejiandikisha kupiga kura hapo, lakini kila Mkenya ana ruhusa kama ni kutoka Taveta kwenda Nairobi, aende akakae Central Province n.k.

Na tukija kwa ile inaitwa mambo ya local government. Local government iendelee lakini ile kitu inaitwa provincial administration iondolewe. Kitu tutakuwa nacho ni kwamba waziri mkuu wa kile jimbo atachaguliwa na D.C, atachaguliwa kama tutamwita Katibu. (?). Kama tutamwita Katibu wa wilaya

The meeting ended at 5.55pm.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**